# Sauti ya Kweli Kimataifa
## (The Voice of Truth International)

### Toleo la 97

Mzalishaji (Producer):
**World Evangelism Team**

Nakala ya Kiswahili (Swahili copy):
**Swahili Gospel Team**

Mawasiliano:

+255 (0) 764 792 979
+255 (0) 765 098 981

Taarifa (Notice):

Kitabu hiki hakiuzwi, kinatolewa bure na kanisa la Kristo kupitia taasisi ya ***World Evangelism Team (WET).***
This book is not for sale, it is freely given by the church of Christ throuth the institution ***World Evangelism Team (WET).***

# Waandishi

George Akpabli
Felix O. Aniamalu
Rex Banks
Wayne Barrier
Paula Bates
Roy Beasley
Mike Benson
Ron Bryant
Charles Burch
Kyle Butt
Frank Chesser
Betty B. Choate
Glenn Colley
Lance Cordle
Sunny David
Hans Dederscheck
David Deffenbaugh
Clarence DeLoach, Jr.
Bill Dillon
Bobby G. Dockery
Hershel Dyer
Earl Edwards
Demar Elam
Raymond Elliott
Reuben Emperado
David Everson
Royce Frederick
Gary C. Hampton
Jack Harriman
Parker Henderson
John Kachelman, Jr.

Dayton Keesee
David R. Kenney
Dalton Key
Michael L. King
Robert C. Lupo
J. Randal Matheny
Cecil May, Jr.
Wes McAdams
Colin McKee
Stan Mitchell
Kevin L. Moore
Owen D. Olbricht
David Pharr
Neal Pollard
Mark Posey
Steve Reeves
Andy Robison
Martha Rushmore
Rebecca Rushmore
David A. Sargent
Darrell Surrette
David Tarbet
J.J. Turner
Ken Tyler
Allen Webster
R.H. Tex Williams
Nathan Wright
Ancil Jenkins
Jeff Jenkins
Gordon Hogan
Wayne Jackson




# Roho Mtakatifu: Kweli na Si Kweli

Louis Rushmore

Baadhi ya vitu leo hii vinamheshimu kweli Roho Mtakatifu katika maisha ya binadamu. Nyongeza, baadhi ya vitu hata vinafundishwa na baadhi ya washirika wa makanisa ya Kristo **ambayo hayana uthibitisho wa kibiblia na kimafundisho si ya kweli**. Bila kujali iwe mtu ana amini kwamba Roho Mtakatifu anakaa ndani ya mtoto wa Mungu kihalisia, kimwili na utu au badala yake anakaa kwa Mkristo kwa njia ya Neno la Mungu, baadhi ya mafundisho kuhusu Roho Mtakatufu ni ya **kweli**, na mengine ni ya **uwongo**.

Kwa ujumla, mtume Paulo aliandika kwa uvuvio Mtakatifu kwamba miujiza ilitakiwa kukoma pindi kusudi la kuleta ufunuo wa Maandiko utakapokamilika, yaani Agano Jipya (1 Wakorintho 13:8-12). Kusudi la miujiza daima lilikuwa ni kuthibitisha Neno (Marko 16:20) na kumthibitisha Kristo (Yohana 20:30-31). Mwandishi wa kitabu cha Waebrania aliyevuviwa alitambua kwamba miujiza katika karne ya kwanza ililithibitisha Neno la Mungu hususani kuhusiana na wokovu wa roho (Waebrania 2:3-4).

Kwa hiyo, shughuli za sasa za Roho Mtakatifu hazijumuishi mawasiliano ya leo kwa mtoto wa Mungu au kwa mtu mwingine yeyote. Kihistoria na katika kipindi cha miujiza ya kibiblia, Roho Mtakatifu alizungumza na manabii wa Mungu katika Agano la Kale na katika Agano Jipya (2 Petro 1:21). Katika wakati ambapo miujiza haipo bali kuna ukamilifu wa Agano Jipya, Roho Mtakatifu haongei moja kwa moja na mwana wa Mungu. Hata kama Mkristo akidai kuongea naye,

Mungu haongei na mtu yeyote sasa hivi kupitia Roho Mtakatifu kwa *"sauti ndogo"* (1 Wafalme 19:12)!

Zaidi sana, Roho Mtakatifu hamfanyii maamuzi mwana wa Mungu wala hamwongozi katika kufanya maamuzi yake. Badala yake, Roho Mtakatifu huwasukuma wale wanaojitahidi katika utekelezaji wa Neno la Mungu lililovuviwa katika maisha yao. Huu ndio ukweli kwa Wakristo watendao kweli.

Majaliwa ya Mungu na jinsi Roho Mtakatifu anavyohusika katika majaliwa hayo yanayofungamana na mazingiria ya historia ambayo yanatoa fursa na chaguzi ambapo wana wa Mungu wanaweza kufanya maamuzi yao wenyewe. Ingawa Roho Mtakatifu anahusika katika majaliwa Matakatifu, hilo halihusiani moja kwa moja na Mungu kwa njia ya Roho Mtakatifu kuzungumza na mtu yeyote leo hii. Pia, majaliwa ni pazia la nyuma la Mungu katika kujibu maombi, lakini majiliwa ya Mungu yasiyoonekana hayawezeshi mawasiliano ya moja kwa moja baina ya Roho Mtakatifu na Wakristo wa leo.

Wakati wowote Mungu alipowasiliana na mwanadamu huko kale kwa njia ya Roho Mtakatifu, mawasiliano hayo yalithibitishwa kwa miujiza (kwa mfano, fimbo ya Musa, Kutoka 4:1-5; Ngozi ya kondoo kwa Gideoni, Waamuzi 6:26-40; nk). Tangu nyakati za miujiza ya Biblia zilipoisha miaka mingi iliyopita, bado kuna ***"sauti ndogo"*** ambayo mtu anaweza kudhani kwamba anasikia hata leo bila ya kuthibitishwa na miujiza ya Biblia, badala ya kuchukulia kuwa ni hisia za kibinadamu tu. Bila ya miujiza kuthibitisha, hata kama ni kweli mtu alisikia ***"sauti ndogo,"*** basi hasingeweza kutambua kuwa sauti hiyo ilikuwa ni ya nani, ya Mungu au ya Shetani. Pekee mtu ataishia kubashiri chanzo cha sauti hiyo.

Uongozi wa moja kwa moja, dira au mawasiliano yanayosemwa kuwa yanatokana na Roho Mtakatifu leo hii **hayatokani na chanzo Kitakatifu**. Wala aina hiyo ya madai hayana ushahidi wa kibiblia (hususani Agano Jipya), badala yake yanaibuka kutoka katika mafundisho ya Kikarismatik na ya Kipentekoste, ambayo si ya kimaandiko na yanayokinzana na Maandiko.

Pamoja na hayo, makanisa ya Kristo yanaongozwa na Roho Mtakatifu pindi yanapokuwa na Wakristo "wanaoongozwa na Roho" (Warumi 8:14; Wagalatia 5:18). Makanisa na Wakristo wanapaswa kukubali kuongozwa na Roho Mtakatifu leo hii, lakini ili hilo lifanyike, ni lazima walitumie Neno la Mungu lililovuviwa na Roho Mtakatifu na kuthibitishwa kwa miujiza. Kwa nyongeza, tunapaswa kusema ***"kama mausia ya Mungu"*** (1 Petro 4:11) na kuepuka ***"lugha ya Ashdodi"*** (Nehemia 13:24).

## JE! UNAWEZAJE KUJUA KUWA UNA ROHO MTAKATIFU?

Shadrack S. Msambaza

Wapentekoste wanasema kuwa ili mtu athibitike kuwa ana Roho Mtakatifu basi ni lazima anene kwa lugha. Lakini Biblia iko kinyume kabisa na fundisho hilo. Yohana Mbatizaji alijawa na Roho Mtakatifu kabla hata hajazaliwa (Luka 1:15), lakini hakufanya ishara yoyote 10:41).

Maandiko yanaonesha kwamba hata katika karne ya kwanza si kila Mkristo alikuwa na uwezo wa kunena kwa lugha. Swali liliulizwa, ***"Wote wananena kwa lugha?"*** (1 Wakorintho 12:30). Mtume Paulo asingeweza kuuliza swali hilo ikiwa Wakristo wote walinena kwa lugha. Je, wale wasionena kwa lugha hawakuwa Wakristo? Hapana, walikuwa Wakristo, kwani alisema, ***"Kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho, wale waliotakaswa katika Kristo Yesu, walioitwa wawe watakatifu,"*** (1 Wakorintho 1:2). Wapentekoste wanasema kuwa mtu anaweza kuwa Mkristo bila ya kuwa na Roho Mtakatifu. Lakini katika Warumi 8:9, Paulo alisema, ***"Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake."*** Haiwezekani kuwa Mkristo kama huna Muhuri wa Roho Mtakatifu (2 Wakorintho 1:21-22; Waefeso 1:13; 4:30).

Katika Wagalatia 5:22-23 tunaambiwa kuhusu tunda la Roho. Katika matunda yaliyoorodheshwa, hakuna hata tunda moja la mwujiza kama vile kunena kwa lugha. Hivyo, ikiwa tunataka kujua kama tuna Roho Mtakatifu au la! Basi tunaweza kujipima au kuwapima wengine kwa kutumia orodha hiyo. Kuwa na Roho Mtakatifu, na kuwa uwezo wa kufanya miujiza ni vitu viwili tofauti kwa mujibu wa Biblia.



# Kufufuka kwa Yesu

Jerry Bates

Uthibitisho mkuu wa Uungu wa Yesu na ukweli wa Ukristo ni kufufuka kwa Yesu. Watu wengi wanatambua ukweli huu; hivyo, ufufuo pia ni moja kati ya mambo yanayo shindaniwa, yanayopatikana katika Biblia. Si jambo geni kusikia watu wakisema kwamba Yesu hakufufuka kutoka kwa wafu. Kwa kawaida, hutoa maelezo machache kutetea hoja yao; wanaposema hutegemea watu wakubaliane na hoja yao. Maelezo ya ufufuo katika Biblia mara nyingi huonekana kama hadithi ya kutungwa ya kanisa la awali ili kuongeza heshima na mamlaka kwa mwanzilishi wao, Yesu. Wasioamini mara zote hufikiri kwamba Wakristo wa awali walikuwa wakitafuta sababu ya kumwamini Yesu; kwa hiyo, walikuwa tayari na shauku ya kuamini chochote ambacho kingeunga mkono hadithi ya kufufuka ambayo ilikuwa imetungwa. Kuna maelezo ya kuvutia katika Luka 24:13-35 ambayo yanakinzana kwa uwazi na hoja hiyo.

Katika aya hizi, tunawaona wanafunzi wawili wa Yesu wakitembea kuelekea kijiji cha Emau, na Yesu akawatokea, lakini hawakumtambua. Walikuwa wakizungumza juu ya kile kilichotokea siku chache zilizopita, na walikuwa wamekatishwa tamaa (Luka 24:17). Mioyo yao ilijawa na uchungu wa kukatishwa tamaa na kupoteza matumaini. Mwokozi wao alikuwa amekufa si muda mrefu! Ndoto zao za ujio wa Masihi zilikuwa zimezimwa kwa kusulibiwa kwa Yesu.

Zaidi sana, wanafunzi hawa tayari walikuwa wamekwisha kusikia hadithi ya kwamba kaburi la Yesu lipo tupu. Huu ulikuwa ni wakati wa jioni pindi Yesu alipojiunga nao katika matembezi (24:29), na walikuwa

wamesikia kwamba baadhi ya wanawake walikwenda kaburini mapema asubuhi ile, wakaona maono ya malaika na wakakuta kaburi liko tupu. Pia walikuwa wamesikia kwamba baadhi ya wanafunzi wengine walithibitisha kisa hicho kuwa kaburi liko tupu. Watu hawa pia walikuwa wanajua kwamba Yesu alitabiriwa na manabii kuwa atafufuka katika siku ya tatu. Pamoja na hayo, lakini bado walikuwa hawajafikia katika hitimisho kwamba Yesu alikuwa amefufuka. Mpaka wakati huu, tunaweza kujisikia kuwagusa mabegani (mawazoni) na kuwaambia waamke na kuamini ushahidi. Tazama kwamba watu hawa hawakuwa na shauku ya kuamini madai ya ufufuo kama ambavyo wengi hujaribu kutufanya na sisi tusiamini. Kihalisia, kinyume chake ni kweli. Walikuwa wamekithiri kutotaka kuamini ufufuo, hata ingawa walikuwa wamesikia baadhi ya taarifa ambazo ziliashiria uwezekano wa ufufuo kuwa ni wa kweli.

Yesu aliwaambia watu hawa kwamba walikuwa wapumbavu. Kwa nini walikuwa wapumbavu? Walikuwa wakienenda kama wapumbavu kwa sababu hawakuamini au kuelewa kile manabii walichokisema kumhusu Masihi. Kisha Yesu akawakumbusha kwamba yote yaliyotokea yalikuwa ni lazima yatokee na ya kwamba ilikuwa ni sehemu ya mpango wa Mungu. Zaidi sana, Musa na manabii walitabiri mambo haya. Yesu aliwafafanulia kile Maandiko yalivyotabiri kumhusu yeye.

Sababu moja kwa nini watu hawa kutoka Emau hawakuamini taarifa za kaburi kuwa tupu ni kwa sababu walizibagua taarifa hizo na Maandiko. Wengi leo hii wanafanya vivyo hivyo. Wanayaondoa maelezo ya ufufuo kama hadithi za kutungwa na waandishi wenyewe, wakisahau kuwa maelezo haya yalikuwa ni sehemu tu ya mpango wote wa Mungu kama ilivyofunuliwa katika Biblia. Wanakataa unabii wa Agano la Kale kuhusu ulazima wa Yesu kuteseka na kufa msalabani. Hawazingatii unabii wa Yesu mwenyewe kuhusu kifo chake na kufufuka, sawa tu na watu hawa ambao hawakuyatilia maanani maneno ya Yesu.

Wakosoaji wanapuuza ushahidi mwingine kuhusu ufufuo wa Yesu na kuyachukulia maelezo haya kama hadithi ya kawaida tu. Dhana za kifikra mara nyingi huwafanya watu kuwa vipofu wasione ukweli. Kwa karne watu waliamini kwamba Aristotle (mwanafalsafa wa kale wa Kigiriki) alikuwa sahihi aliposema kwamba *kadiri kitu kinavyokuwa kizito, ndivyo kitakavyodondoka kwa kasi katika uso wa dunia*. Katika mwaka wa 1589, karibu miaka 2,000 baada ya kifo cha Aristotle, Galileo (mwanafalsafa) aliwaita maprofesa wenye mafunzo, katika Mnara wa Pisa. Kisha akapanda juu ya mnara na kuangusha chini vitu viwili kwa pamoja, kimoja kikiwa na uzito wa kilo 4.53592 na kingine chenye uzito wa kilo 0.453592. vyote viwili vilitua kwenye ardhi kwa pamoja. Nguvu ya imani ilikuwa imara sana, kiasi kwamba maprofesa walikataa walichokiona. Waliendelea kusema Aristotle alikuwa sahihi licha ya ushahidi uliotolewa mbele ya macho yao.

Tunapaswa kutenda kile Yesu alichokifanya kwa kuwatia moyo watu wale kutoka Emau wafanye, amini yote ambayo manabii waliyanena. Luka alionesha kwamba sababu ya wao kutokumtambua Yesu ni kwa sababu hawakuwa wameelewa vizuri Maandiko (Luka 24:25-26). Waliyaamini baadhi tu. Waliyapenda yale yaliyomwonesha Masihi kama mfalme na mtawala. Lakini hawakupenda sehemu zilizozungumzia kuteseka kwa Masishi; hivyo, walikataa.

Yesu aliwafundisha watu hawa kwamba msalaba ulikuwa ni wa lazima. Haukuwa makosa wala ushindi kwa Ibilisi. Masihi anayeteseka haikuwa ni jambo la ukinzani. Kusingekuwa na taji kama kwanza kusingekuwa na msalaba. Pasi na shaka mwanzoni hawakuelewa hilo. Waliona kifo cha Yesu kama janga baya sana na lisilorekebishika. Pindi Yesu alipozungumza nao wasaa huo wakazingatia, walijifunza kwamba mateso yale hayakuwa ajali ya kawaida. Badala ya kuwa janga kuu kati ya majanga, ilikuwa ni hitaji kuu. Upendo ulililia uhuru wa mwanadamu, wakati haki ya Mungu ilitaka ahadhibiwe. Je! Mgogoro wa matakwa haya uliwezaje kutatuliwa? Yesu alilipa deni kwa ajili yetu. ***"Yeye mwenyewe alizichukuwa dhambi zetu katika mwili wake juu***

***ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa”*** (1 Petro 2:24).

**Akili zao zilijawa na uchungu wa kuvunjika moyo na kupoteza matumaini. Mwokozi wao alikuwa amekufa muda si mrefu! Ndoto zao za ujio wa Masihi zilikuwa zimezimwa kwa kusulibiwa kwake Yesu.**

Maandiko yanasema kwamba macho yao yakafumbuliwa, na wakatambua kwamba Yesu alikuwa ndiye aliyekuwa akizungumza nao. Yesu alitoweka mbele ya macho yao. Sasa kila kitu kikawa wazi, nao wakaenda kuwaambia mitume kile kilichotokea. Nini kilikuwa cha tofauti? Walimwona Yesu! Hata hivyo, kabla Yesu hajajifunua kwao, aliwarudisha katika Maandiko. Inaonekana, alitaka waelewe vizuri Maandiko ili waone maelezo ya ufufuo katika muktadha wake. Hivyo ndivyo hasa tunavyopaswa kufanya. Hatuwezi kuyatenga maelezo ya ufufuo na muktadha wote wa Maandiko na mpango wa Mungu kana kwamba ni sehemu tu ambayo tunaweza kukubali au kukataa. Tunapoyazingatia Maandiko yote, kaburi lililo tupu na ushahidi mwingine unaolizunguka tukio lile, ukweli wa ufufuo ndio kitu pekee ambacho kinaleta maana.

## UPINZANI WA KUFUFUKA KWA YESU

Shadrack S. Msambaza

I. Watu wenye nguvu walijaribu kuzuia ufufuo (Mathayo 27:62-66).
   A. Walikumbuka maneno ya Yesu kuwa atafufuka (mst. 62-63).
   B. Waliweka askari walilinde kaburi (mst. 64-66).
   C. Walisiliba kaburi ili kusiwe na uwezekano wa kutoka (mst. 66).
II. Mpango huo haukufanikiwa (Mathayo 28:1-2).
   A. Malaika alitibua mipango yao ili ushahidi uwepo (mst. 2-4).
III. Mpango mwingine wa kuzuia habari za ufufuo (Mathayo 28:11-15).
   A. Rushwa yatumika kuwafumba midomo mashahidi maaskari.
IV. Pasipo ufufuo wa Yesu hakuna Ukristo (1 Wakorintho 15:14).



# Je! Mungu Anazungumza na Mtu Leo Hii?

J.C. Choate

Biblia ina Agano la Kale na Agano Jipya. Hivyo, Biblia, ni Neno kamili la Mungu, likiwa na Maandiko yote Matakatifu kama yalivyotamkwa na Mungu. Agano la Kale lilikuwa ni Neno lake kwa watu wake kabla ya kifo cha Kristo. Agano Jipya ni Neno lake kwa watu wake baada ya kifo cha Kristo. Ni Agano Jipya ndilo linalotuambia jinsi ya kuokoka, namna ya kuishi, na jinsi ya kwenda Mbinguni.

Tukiwa na mawazo endelevu akilini, unaweza kuuliza, "Je! Mungu anazungumza na mtu leo hii?" Jibu la swali hilo ni NDIYO. Kwanza kabisa, tunadhani kuwa Mungu yupo. Hilo si jambo gumu kulifanya pindi mtu anapoacha kuzingatia kwamba kila kitu kilichopo kinaweka ushuhuda wa uweza wa uumbaji wake. Kitu hakiwezi kutokea pasipo na kisababishi. Kwa hiyo, Mungu amekuwepo tangu milele, na kwamba aliumba mbingu na nchi, na vyote vilivyomo (Mwanzo 1:1). Hata hivyo, uumbaji wa Mungu wa mwanadamu, alikuwa na kusudi la kuwepo kwake (mwanadamu): kwamba ni kumheshimu na kumtukuza Muumba wake (Mwanzo 1:26-27, 31). Katika Agano Jipya, tunasoma maneno haya, ***"Sasa kwa Mfalme wa milele, asiyeweza kuona uharibifu, asiyeonekana, Mungu peke yake, na iwe heshima na utukufu milele na milele. Amina"*** (1 Timotheo 1:17). Pamoja na hayo, Mungu asingeheshimiwa kama mwanadamu angelazimishwa kumtii. Kwa hiyo, Mungu alimpa uhuru (Mwanzo 3). Angeweza kuchagua kutii au kutotii. Ili kumwezesha mwanadamu kufanya maamuzi ya busara, ilikuwa ni lazima kuweka mbele yake

vyote viwili **wema na ubaya**. Hivyo, Mungu akanena na mwanadamu ili kufunua mapenzi yake, na kisha akamwonya juu ya dhambi na madhara yake. Mwanadamu akaachwa afanye maamuzi ya mwisho.

Daima Mungu amekuwa akizungumza na mwanadamu. Katika Agano Jipya, mwandishi wa Waebrania alisema, ***"Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu"*** (Waebrania 1:1-2). Sehemu hii na Neno la Mungu inazungumza mengi. Kwanza, inatueleza kwamba Mungu alizungumza kwa nyakati tofauti na kwa njia tofauti. Zamani, kama ilivyoelezwa na Agano la Kale, alizungumza moja kwa moja na mababa au viongozi wa familia, nao wakalichukua Neno lake na kulipeleka kwa kaya zao. Mfano wa hili ni pale Mungu alipozungumza na Nuhu, Ibrahimu na wengine wa wakati huo. Kisha baadaye, Mungu alizungumza na watu kwa njia ya manabii kama vile Musa, Isaya, Yeremia na wengine wengi. Kwa wakati huo Neno lake lilikuwa katika mchakato wa kuandikwa ili kwamba mapenzi yake yatunzwe ili yadumu na hatimaye kuwawezesha watu kuyaendea na kuyasoma muda wowote.

Hatimaye, Mungu akanena kwa njia ya Mwanawe, Yesu Kristo, kama ilivyofunuliwa katika Agano Jipya. Mbele ya Kristo na wanafunzi wake, Mungu alinena toka Mbinguni akisema, ***"Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye"*** (Mathayo 17:5). Mtume Yohana, moja kati ya wanafunzi wa karibu na Kristo, alisema, ***"Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa; neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo"*** (Yohana 1:17). Kristo mwenyewe alisema, ***"Na mtu akiyasikia maneno yangu, asiyashike, mimi simhukumu; maana sikuja ili niuhukumu ulimwengu, ila niuokoe ulimwengu. Yeye anikataaye mimi, asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye; neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho. Kwa sababu mimi sikunena kwa nafsi yangu tu; bali Baba aliyenipeleka, yeye mwenyewe ameniagiza nitakayonena na nitakayosema. Nami najua ya kuwa agizo lake ni***

***uzima wa milele; basi hayo ninenayo mimi, kama Baba alivyoniambia, ndivyo ninenavyo."*** (Yohana 12:47-50).

Sasa tuna nini? Tunaambiwa kuwa Mungu daima huzungumza na mwanadamu. Kamwe hajawahi kumwacha mwanadamu gizani, asijue nini cha kufanya. Badala yake, amezungumza kwa kufunua mapenzi yake na kutuwezesha kufanya maamuzi ya busara. Katika kipindi cha kabla ya Kristo, Mungu alifanya agano na wanadamu, na baadaye na taifa la Israeli, agano lililoitwa "Sheria ya Musa." Kulingana na Wagalatia 3:19, 24-25, ***"Torati ni nini basi? Iliingizwa kwa sababu ya makosa, hata aje huyo mzao aliyepewa ile ahadi; iliamriwa kwa utumishi wa malaika kwa mkono wa mjumbe…Hivyo torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo, ili tuhesabiwe haki kwa imani. Lakini, iwapo imani imekuja, hatupo tena chini ya kiongozi."*** Kwa hiyo, Mungu alitoa Agano Jipya, akimtuma Mwanawe, Yesu Kristo, afe msalabani ili aliondoe lile agano la kwanza. tunasoma, ***"ndipo aliposema, Tazama, nimekuja niyafanye mapenzi yako. Aondoa la kwanza, ili kusudi alisimamishe la pili. Katika mapenzi hayo mmepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu"*** (Waebrania 10:9-10). Kutokea hapo unaweza kuona kwamba Kristo alijitoa dhabihu msalabani ili aliondoe agano la kwanza, kusudi alisimamishe agano la pili, ambalo tunaliita "Agano Jipya."

Linapokuja suala la kama Mungu anazungumza na sisi leo au la! Wengi hufikiri kitendo cha Mungu kuzungumza moja kwa moja na mwanadamu. Hata ingawa tuna mapenzi ya Mungu yaliyoandikwa katika mtindo wa Agano Jipya, lakini bado wapo watu wanaoshindana kwamba, mbali na Biblia, Mungu anazungumza kwa sauti ya wazi kwa njia ya maono, ndoto au kwa njia nyingine. Pamoja na hayo, Biblia haifundishi hivyo.

Kufupisha haya yote, wacha tuziweke vizuri hoja hizi zote: Mungu anazungumza leo hii; Anazungumza kupitia Mwanawe; na Kristo anazungumza kupitia Neno lililoandikwa. Neno hilo linapatikana katika vifungu vya Agano Jipya. Kwa hiyo, tunaposoma Neno kama lilivyoandikwa katika Agano Jipya, hapo ndio Mungu anazungumza

nasi. Neno lake ni roho na uzima, ***"Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo"*** (Waebrania 4:12). Ndilo kweli, ***"Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli"*** (Yohana 17:17). Litaishi na kudumu milele (1 Petro 1:23). Mwishoni, tutahukumiwa kwalo (Yohana 12:48).

Kile Mungu anachokisema, ni lazima kiachwe kama kilivyo. Hatuwezi kuongeza, au kuondoa lolote au kubadilisha kwa namna yoyote ile. ***"Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu ye yote akiondoa lo lote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki"*** (Ufunuo 22:18-19). Mungu amefunua mapenzi yake yote kwa mwanadamu katika Biblia. Kwa hiyo, kwa mtu yeyote leo hii kusema kwamba Mungu amemfunulia ujumbe fulani mpya, anajidanganya, na anatafuta kuwadanganya wengine.

## Je! Biblia Inamapungufu?

Shadrack S. Msambaza

Yesu alisema kuwa yeye ndiye aliyekuwa kiini cha Agano la Kale (Luka 24:44). Katika Agano hilo watu walifundishwa namna bora ya kuishi huku wakijiandaa kwa ujio wa Masihi. Kila alichokisema Mungu, manabii waliandika. Wakati Mungu alipoacha kuzungumza moja kwa moja watu walisoma vitabu ili kujua mapenzi yake.

Katika Agano Jipya, sehemu ya kwanza, inazungumzia maisha ya Yesu na mafundisho yake; sehemu ya pili, inazungumzia utekelezaji wa mafundisho yake kwa uanzishwaji wa kanisa; sehemu ya tatu, inafundisha jinsi ya kuishi maisha ya utakatifu na, sehemu ya nne, inazungumzia maisha ya ushindi wa kiroho. Je! Hayo hayatoshi? ***"Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa,"*** (2 Petro 1:3). Hivyo, hakuna haja ya ufunuo mwingine.

# Yaliyomo

Roho Mtakatifu: Kweli na Si Kweli……………………………………………………....3
Je! Unawezaje kujua kuwa una Roho Mtakatifu?................................5
Kufufuka Kwa Yesu…………………………………………………………………..….6
Upinzani wa Ufufuo wa Yesu……………………………………………………………9
Je! Mungu Anazungumza na Mtu Leo Hii?...........................................10
Je! Biblia Inamapungufu?..................................................................13
Vipi kama watu wangesema “Bado yupo hapa?”…............................16
Ofisi Tatu za Bwana Wetu…………………………………………………………….20
Mawaidha ya Mazishi……………………………………………………………………..22
Je! Umewahi kusikia juu ya miji ya kale iliyozama?…..........................23
Mungu Aliumba Asali  Moja ya Ndege………………………………………….27
ULAGHAI……………………………………………………………………………………….30
Neno Linaloishi…………………………………………………………………………….32
Ikiwa Unadai Kuwa Uliokolewa Kabla ya Ubatizo….…………………………..34
Toba……………………………………………………………………………………………35
Sauli Alikuwa Wapi Alipookolewa?.......................................................36
Wakati Gani Na Kivipi Mtu Huokolewa?...............................................38
Tafuta Aya: 1 Wakorintho 10:14-33……………………………………………...41
Dakika 5 za kujifunza Biblia……….……………………………………………….43
Sababu za Ukuaji wa Kiroho na Kiidadi…............................................44
Maswali Matatu Muhimu………………………………………………………………..45
Yesu ni kielelezo chetu…………………………………………………………………47
Wakristo na Kanisa……...……………………………………………………………..48
Tafuta katika Biblia………………………………………………………………………50
Kuketi Juu ya Nguzo ya Ukuta………………………………………………………51
Maoni ya Haraka katika Aya Muhimu (Ufunuo 6:9; 20:4-10)……………..53
Fursa ya Kufundisha………………………………………………………………………54
Pindi Marafiki Wanapokupa Kisogo…………………………………………………..56
Je! Umeacha Kitu Gani?...................................................................57
Mahubiri Chanya…………………………………………………………………………….58
Uimbaji Huathiri Ukuaji wa Kanisa……………………………………………….61

Sarafu za Kenney……………………………………………………………………………63
Pale Uimbaji Wetu Katika Kusanyiko Unapokuwa na Makosa…………..64
Je, Unapimaje………………………………………………………………………………67
Mtu na "Cocoon"…………………………………………………………………………68
"Na Mwe Wadhili Ninyi kwa Ninyi"………………………………………………70
Imani, Tumaini na Upendo; Maneno Matatu Yenye Nguvu Duniani….72
Masuala ya Kifamilia……………………………………………………………………74
Ndoa kwa Utaratibu wa Mungu……………………………………………………76
Hawauzwi……………………………………………………………………………………77
Wafanye Watoto Waende Kanisani……………………………………………..78
Hata hivyo Si Suala la Wokovu……………………………………………………..79
Sayansi ya Kawaida ya Kutafsiri Maandiko……………………………………84
Msaka Tonge……………………………………………………………………………….85
Mariamu na Martha……………………………………………………………………86
Njia Sita Anazozitumia Shetani Kutushambulia……………………………88
Yosia, Alimtafuta Bwana katika Ujana Wake…………………………………..89
Rubi za Robison……………………………………………………………………………93
Kwa Nini Mambo Mabaya Huwapata Watu Wema ?..........................94
Je, Mvinyo Yenye Kileo Inapaswa Kutumika Katika Meza ya Bwana?...97
Je, Mafarisayo Walikuwa Viongozi Vipofu wa Vipofu wa Mwisho?.....98
Imekwisha…………………………………………………………………………………..99
Mtazamo wa Huduma ya Gerezani ya Daryl Townsend…………………102



# VIPI KAMA WATU WANGESEMA, "BADO YUPO HAPA"?

J.J. Turner, Ph. D.

Wakiwa na macho yenye madoa ya machozi, mioyo mizito na kapu lililojaa manukato ya mazishi, Maria Magdalena na wanawake wengune kwa huzuni, mapema Jumapili asubuhi, walifika kwenye kaburi alimowekwa Yesu Kristo. Wao walikuwa wanatimiza tendo la upendo ili kumaliza mchakato wa kuutayarisha mwili wake kwa ajili ya mahali pake pa kupumzika katika kaburi la kuazima.

Luka ametuachia kumbukumbu ya tukio hili, kuhusiana na kile walichokikuta wanawake wale walipolifikia kaburi. **"Wakalikuta lile jiwe limeviringishwa mbali na kaburi, wakaingia, wasiuone mwili wa Bwana Yesu. Ikawa walipokuwa wakifadhaika kwa ajili ya neno hilo, tazama, watu wawili walisimama karibu nao, wamevaa nguo za kumetameta; nao walipoingiwa na hofu na kuinama kifudifudi hata nchi, hao waliwaambia, kwa nini mnamtafuta aliye hai katika wafu? Hayuko hapa amefufuka. Kumbukeni alivyosema nanyi alipokuwa akaliko Galilaya"** (Luka 24:2-6).

Je! Umeshawahi kujiuliza kama mimi, kwamba kungetokea nini kama wale watu wangewaambia wale wanawake kuwa **"BADO YUPO HAPA?"** Inachukua muda machache kutafakari wazo hili lenye changamoto na kuja na mawazo mengi yasiyo sahihi. Kwa kweli, majibu yanaweza kuondoa msingi wa ukweli wa Ukristo - **KUFUFUKA KWA KRISTO**.

## MAMBO 12 YA KWELI KAMA YESU ANGEBAKI KABURINI

Licha ya orodha ndefu ya matokeo ikiwa watu wale wangesema kuwa, BADO YUKO HAPA, lakini hizi ni baadhi ya matokeo:

1. **Kama Yesu bado yupo kaburini, inamaanisha kuwa alidanganya:** *"Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi"* (Mathayo 12:40). *" Tangu wakati huo Yesu alianza kuwaonya wanafunzi wake ya kwamba imempasa kwenda Yerusalemu, na kupata mateso mengi kwa wazee na wakuu wa makuhani, na waandishi, na kuuawa, na siku ya tatu kufufuka"* (Mathayo 16:21).
2. **Kama Yesu bado yupo kaburini, basi hakuna uthibitisho kuwa ni Mwana wa Mungu mwenye nguvu**: Mtume Paulo aliandika, *"habari za Mwanawe, aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili, na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho*

*ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu;"* (Warumi 1:3-4)

3. **Kama Kristo bado yupo kaburini, basi hakuna habari njema – injili - ujumbe wa kuhubiri:** *"Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; 4 na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko;"* (1 Wakorintho 15:3-4; Zaburi 16:9-11)

4. **Kama Kristo bado yupo kaburini basi hakuna msingi wa Imani inayookoa:** *"tena kama Kristo hakufufuka, basi, kuhubiri kwetu ni bure na Imani yenu ni bure"* (1 Wakorintho 15:14).

5. **Kama Kristo bado yupo kaburini, basi Yeye sio limbuko lao waliolala, kuthibitisha kufufuka mara moja na kwamba hapatakuwa na mauti tena:** *"Kama katika maisha haya tu tumemtumaini Kristo, sisi tu maskini kuliko watu wote. Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala"* (1 Wakorintho 15:19-20).

6. **Kama Kristo bado yupo kaburini, basi wanafunzi wa karne ya kwanza walilaghaiwa na mtu aliyedai kuwa ndiye Kristo.** Soma Yohana 20:19-31 uone jinsi wanafunzi walivyodanganyika ikiwa Yesu alibaki kaburini; ulimwengu ulidanganywa. Soma Kitabu cha Matendo ya mitume.

7. **Kama Kristo bado yupo kaburini, basi ubatizo kwa ajili ya ondoleo la dhambi utakuwa hauna maana:** *"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyo fufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima"* (Warumi 6:4).

8. **Kama Kristo bado yupo kaburini, basi tunaposhiriki meza ya Bwana tunamkumbuka mtu aliyekufa ambaye yupo kaburini:** *"mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo"* (1Wakorintho 11:26), ambayo inamaanisha kuwa yuko hai, kwa sababu alifufuka kutoka wafu na kaburi lilikuwa tupu siku ile ya Jumapili asubuhi.

9. **Kama Kristo bado yupo kaburini, basi hatuna tumaini la kuwa na mwili wa ufufuo kama mwili wake:** *"Kwa maana sisi, wenyeji wetu uko mbinguni; kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo; atakayeubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa uweza ule ambao kwa huo aweza hata kuvitiisha vitu vyote viwe chini yake"* (Wafilipi 3:20-21; 1 Yohana 3:2).

10. **Kama Kristo bado yupo kaburini, basi kusingekuwa na kanisa ambalo ni kusanyiko la walioitwa na injili** (2 Wathesalonike 2:14). *"Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda"* (Mathayo 16:18).

11. Kama Kristo bado yupo kaburini, basi unabii kupitia Daudi utakuwa ni uongo ambao Petro aliueleza siku ya Pentekoste: *"Basi kwa kuwa ni nabii, akijua ya kuwa Mungu amemwapia kwa kiapo, ya kwamba katika uzao wa viuno vyake atamketisha mmoja katika kiti chake cha enzi; yeye mwenyewe akitangulia kuyaona haya, alitaja habari za kufufuka kwake Kristo, ya kwamba roho yake haikuachwa kuzimu, wala mwili wake haukuona uharibifu. Yesu huyo Mungu alimfufua, na sisi sote tu mashahidi wake"* (Matendo 2:30-32).

12. **Kama Kristo bado yupo kaburini, basi ahadi iliyohubiriwa na mtume Paulo ya kurudi kwa Kristo, na roho za wale waliokwenda kuwa pamoja naye ni uwongo mwingine:** *"Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu"* (1 Wathesalonike 4:14).

Tumshukuru Mungu kwa kuwa maneno hayakuwa, BADO YUPO HAPA, BALI, ***"HAYUPO HAPA, AMEFUFUKA."*** Ukweli huu unaibua swali: KUFUFUKA KWA YESU kutoka kwa wafu kunaleta tofauti gani katika maisha yako na kukuhakikishia ufufuo wako kutoka katika wafu?

# OFISI TATU ZA BWANA WETU

Rodney Nulph

Yesu Kristo hakika alikuwa mwanadamu, mh, ni zaidi ya mwanadamu! Yesu alikuwa Mungu na mwanadamu kamili. Kielelezo hiki cha ubinadamu na Uungu kinajulikana miongoni mwa wanatheolojia kama muungano wa hali ya juu. Ni dhahiri, hakuna mahali pengine ambapo asili mbili ya aina hii imewahi kuwepo zaidi ya ile ya Yesu Kristo. Kwa kuwa Yesu alifanyika mwanadamu kwa ajili yetu, na wakati huohuo akiwa Mungu, inamfanya awe na sifa za kipekee za kufanya kazi fulani kwa wale waliokombolewa kwa damu yake. Kulikuwa na ofisi kuu tatu ambazo zilikuwa muhimu ili kuziba pengo kati ya mwanadamu mwenye dhambi na mwenyeenzi Mungu. **Manabi**i walinena kwa niaba ya Mungu, **makuhani** walimtolea Mungu dhabihu, na **wafalme** waliongoza chini ya uongozi wa Mungu. Yesu alitimiza ofisi hizi zote tatu kikamilifu!

## YESU KAMA NABII

Nabii wa Mungu ni yule ambaye anamfunua Mungu, ananena kwa niaba ya Mungu na anawasilisha ukweli wa Mungu kwa watu. Manabii wa Mungu walitabiri (walihubiri hali halisi iliyokuwepo kwa wakati husika) na kutabiri (Kusema mambo yajayo). Bila shaka, Yesu bila dosari alifanya haya alipokuja ***"kutufunulia Baba"*** (Mathayo 11:27) na kuwafahamisha mapenzi ya Mungu (Yohana 8:28; 12:49-50). Mungu alimfunulia Musa kuwa siku zijazo unabii wa Musa hautakuwa na mamlaka, lakini ***"atakuondokeshea nabii"*** (Kumbukumbu 18:15). Angekuwa nabii ambaye wanadamu wangemsikiliza. Miaka kadhaa baadaye, Roho Mtakatifu alimwongoza Petro kumnukuu Musa na kutumia unabii ule kwa Yesu Kristo. Kwa nyongeza, Yesu anajirejelea

kama nabii (Mathayo 13:57-58; Luka 13:33). Hakika, hakuna nabii aliye zungumza kama nabii Yesu (Yohana 7:46)!

## KRISTO KAMA KUHANI

Makuhani walikuwa ni wale ambao katika Agano la Kale walikuwa na jukumu la kutoa dhabihu kwa Mungu kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Hata hivyo, kila kuhani hadi wakati wa Yesu, ilikuwa ni lazima kwanza atoe dhabihu kwa ajili ya utakaso wa kuhani na baadaye ndipo atoe kwa ajili ya watu wengine (Waebrania 4:15; 7:27). Yesu alitoa dhabihu moja tu kwa ajili ya mwanadamu, na dhabihu hiyo ndiyo ilikuwa ya mwisho! Kama Kuhani wetu Mkuu, Yesu anasimama kati yetu na Baba kama Mpatanishi (1 Timotheo 2:5). Inaweza kusemwa kwamba wote wawili nabii na kuhani wanasimama kati ya Mungu na mwanadamu mwenye dhambi. Ukizungumzia nabii, aliwasilisha Neno la Mungu kwa mapana yake. Kuhusu kuhani, alitoa dhabihu ya watu kwa Mungu kama ilivyompasa. Kwa hiyo, Yesu ni Nabii ambaye aliwasilisha Neno la Mungu kwa mwanadamu, na pia ni Kuhani aliyetoa dhabihu yake kwa Mungu Baba, kwa niaba yetu.

## KRISTO KAMA MFALME

Mfalme ni mtu ambaye ana mamlaka ya kutawala kundi la watu. Cha kuvutia, Yesu anatajwa kama Mfalme katika Maandiko Matakatifu. Ushuhuda wa ukweli wa kinabii kuhusu Masihi wa jambo hili ni (Isaya 9:6-7). Mungu kupitia Danieli aliahidi kuwa Yesu atakuwa Mfalme atakayetawala ufalme wake (Danieli 7:14). Wakati mamajusi walipokuwa wakiulizia kuhusu mtoto mchanga Kristo, walitambua ufalme wake waliposema ***“Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi?”*** (Mathayo 2:2). Yesu mwenyewe alitambua ofisi yake mbele ya Pilato alipo kiri kuwa ***“Naye Yesu akasimama mbele ya liwali; liwali akamwuliza, akasema, wewe ndiwe mfalme wa Wayahudi? Yesu akamwambia, wewe wasema”*** (Mathayo 27:11). Ufalme wa Yesu unatangaza mambo kadhaa muhimu: Kwanza, ana ufalme, kanisa (Mathayo 16:18-19; Wakolosai 1:13). Pili, ana mamlaka

ya kutawala na kuhukumu (Matendo 17;31; Ufunuo 19:11). Tatu, ni mkuu juu ya vitu vyote (Wakolosai 1:18). Inashangaza kidogo Paulo anapomzungumzia Yesu kama ***"…Yeye aliyehimidiwa, mwenye uweza peke yake, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana;"*** (1 Timotheo 6:15).

Kazi ya Masihi, kwa njia nyingi, imekamilika alipokuwa hapa duniani. Hata hivyo, Yesu bado anatenda kazi katika kanisa lake na katika uumbaji wake (Wakolosai 1:13-18). Kama Nabii, Yesu anazungumza na mwanadamu kupitia Neno lake. Kama Kuhani, Yesu alitoa dhabihu kwa ajili ya roho zetu (Waebrania 9:12; Ufunuo 5:9). Kama Mfalme, Yesu anatawala katika ufalme wake wa milele, kanisa. Hakuna maswali kuhusu hilo. Alikuwa mwanadamu, ah zaidi ya mwanadamu. **Ni Nabii, Kuhani na Mfalme**.

## MAWAIDHA YA MAZISHI

Marafiki watatu walikuwa wanajadili kuhusu kifo. Mmoja akawauliza wengine, *"mnataka watu waseme nini kuhusu wewe kwenye mazishi yako?"* Wa kwanza akasema, *"nataka waseme 'alikuwa ni mtu mwenye utu aliyejali jamii yake.'"* Wapili akasema *"alikuwa mume mwema na baba ambaye ni mfano mzuri wa kuigwa na wengine."* Wa watatu akasema, *"nataka waseme, 'tazama, anakwenda!'"* Siku moja tuta "kwenda" vilevile wakati tutakapopitia ufufuo wa jumla wa wafu. (Yohana 5:28-29).

# JE! UMEWAHI KUSIKIA JUU YA MIJI YA KALE ILIYOZAMA?

Betty Bulton Choate

Sisi tunaoisoma Biblia tunafahamu ya kwamba Mungu alimwumba mwanadamu kwa mfano na sura yake, akampa uwezo wa kuishi na kufanyakazi katika dunia aliyomweka. Bila shaka, ndani ya vichwa vyetu kumezikwa picha ya "Sokwe Mtu" ambao wanaonekana kuwa wamebakisha hatua chache kufikia hatua ya ubinadamu kutoka katika kipindi cha kuwa Sokwe. Tumekuwa tukisoma sana mashuleni kuhusu hilo kiasi kwamba hata Waamini wengi wa Neno la Mungu hawawezi kutilia shaka wakiona kuwa ni picha ya kweli ya maendeleo ya historia ya ulimwengu.

Nakusihi utofautishe baina ya Mwanzo 3 ambapo Adamu na Hawa walipofukuzwa watoke katika Bustani ya Edeni na Mwanzo 6 pale Mungu alipomwambia Nuhu aitengeneze safina kwa sababu anakwenda kuiangamiza dunia kwa maji. Kuna maelezo machache sana yaliyotolewa kuhusu jinsi hali ilivyokuwa katika kipindi hicho. Nashawishika kuamini kwamba wanadamu, wa wakati huo walikuwa wako vizuri kimwili kuliko sisi. Tunaweza kudhani kuwa sisi ni watu wenye afya zaidi na watu wenye akili zaidi kuwahi kuishi, lakini historia ya kibiblia inakana hilo.

Adamu alikuwa na umri gani alipokufa? Miaka 930! Wazee wote waliotajwa kabla ya Nuhu walikuwa na uwiano wa ukomo wa maisha unaofanana na huo. Hili linatuambia kwamba, kimaumbile, hakukuwa na mlingano wa kiafya baina ya wao na sisi. Tunaweza kupata picha kuwa hata akili zao zilifanya kazi sana kuliko sisi.

Tunasoma nini kuhusu uwezo wa watu hawa wa awali? Tunajifunza katika Mwanzo 4:17 kwamba Kaini alijenga mji!

Katika aya ya 21 tunaambiwa kuwa Yubali alikuwa baba wa hao wapigao kinubi na filimbi! Aya hii inathibitisha ukweli maarufu kwamba muziki umewekwa ndani ya kila kiumbe hai (Ameumbwa kwa sura yake? Sefania 3:17 inatuambia kuwa hata Mungu hushangilia kwa kuimba kwa sababu ya furaha kwa ajili ya watu wake!)

Katika aya ya 22 tunaambiwa kuwa Tubal-kaini alikuwa mwalimu! Kazi yake ilikuwa kufua shaba na vyuma! Wanahistoria wa leo wanasema kwamba wafua vyuma katika Uturuki mashariki walijua jinsi ya kutengeneza shaba mapema katika miaka ya 3000 K.K (Muda mfupi baada ya gharika), lakini ni katika mwaka wa 20 K.K hadi mwaka wa 20 B.K ndipo walipoijua shaba na chuma. Cha kushangaza, kulingana na Maandiko, watu wale wa kale walikuwa tayari wanajua jinsi ya kutengeneza vyuma zamani hata kabla ya gharika.

Maelezo haya yanaelezea ufanikishaji wa awali katika historia ya mwanadamu. Kadiri karne zinavyopita, ndivyo wanadamu wanavyozidi kuondokana na utauwa, tunaweza kuona kwamba mwanadamu aliendelea kukua katika mafanikio yake. Hata leo, itakuwa changamoto kwa mtu na wanawe watatu kutengeneza meli (safina) yenye urefu wa futi 450, upana wa futi 72 na kimo cha futi 45, yenye uwezo wa kustahimili nguvu kubwa ya gharika. Hata hivyo, wapo walioweza.

Uvumbuzi wa wachunguzi wa mambo kale (Wanaakiolojia) unakinzana na mitazamo ya dhana za mageuko (evolution). Hii inaonesha kwamba tangu nyakati za kale, wanadamu walikuwa wabunifu na wenye akili kama tulivyo, na huenda kutuzidi.

Je! Umewahi kusikia juu ya ugunduzi wa miji ya kale iliyozama? Katika miaka kadhaa ya hivi karibuni kuna miji kadhaa iliyogunduliwa. Mji mmowapo, ni katika Ghuba ya Cambay pwani ya magharibi ya India, wenye kipimo cha maili tano urefu na upana maili mbil! Graham Hancock alisema, *"Miji kwa kiwango hiki haifahamiki katika rekodi ya akiolojia hadi takribani miaka 4,500 iliyopita wakati miji mikubwa ya kwanza ilipoanza kuonekana huko Mesopotamia. Hakuna miji mingine ya Cambay iliyoko chini ya maji inayofahamika. Miji ya kwanza katika kipindi cha kihistoria iko mbali na miji hii kama tulivyo leo kutoka*

*katika piramidi (vichuguu vikubwa vya kale vilivyojengwa kwa mawe) za Misri."*

Katika mwaka wa 1995, muundo wa mji uligunduliwa karibu na Okinawa, nchini Japan. Maelezo yaliyotolewa ni: *"Uko karibu futi 60 kwenda chini, muonekano wa juu ulionekana kuwa ulitengenezwa na wanadamu. Ugunduzi ulishitua ulimwengu wa akiolojia. Piramidi za Japani zilizo chini ya maji au zilizo katika hali ya uharibifu kama zilivyokuja kufahamika zimekuwa ni kitu cha ajabu. Katika maeneo yote nane yaliyogunduliwa."*

Je! Tarehe na gunduzi hizi zinatuambia nini? Maelezo ya kitabu cha Mwanzo ni ukweli halisi! Maelezo ya kwamba hakuna miji ya aina hiyo katika rekodi za akiolojia iliyoonekana hadi katika miaka ya 4500 K.K. Tarehe za mabaki yake zinaonesha kuwa ni miongoni mwa majengo ya kwanza kabisa baada ya gharika. Piramidi za Misri zinaangukia katika miaka hiyohiyo. Je! Majengo haya hayatuambii kwamba kulikuwa na maarifa makubwa na uwezo miongoni mwa wanadamu wa kale? Je! Maarifa ya watu walioishi kabla ya gharika hayakurithishwa kwa wazao wa Nuhu na watoto wake?

Gharika ilibadilisha dunia kabisa. Maili kwa maili ya maji yaliweka matabaka ya udongo katika ulimwengu wote ili kuthibitisha ukweli usiopingika kwamba wakati fulani huko nyuma kulikuwa na gharika ulimwengu mzima. Sio tu kwamba uso wa dunia ulibadilishwa, bali pia ardhi nyingi zilivunjwa na kutenganishwa. Wanaakiolojia walikisia kwamba mji uliotajwa hapo juu karibu na pwani ya Japani ulijengwa juu ya ardhi kubwa ambayo hapo awali ilikuwa ikiunganisha Japan na Taiwan. Ukweli ya kwamba miji yote kwa sasa iko chini ya bahari, sio kwamba iliangamizwa kwa vita, ni ushahidi mkubwa, kwamba ustaharabu ulistawi sana ambao sio tu ulistawi kutoka nyakati za zamani bali pia kwamba gharika ambalo lilifika katika vilele vya milima mirefu ya dunia iliyokuwepo na kufunikwa yote. Kusudi la Mungu halikuwa tu kuanza upya na familia bali kufuta kila kitu ambacho kiliwaharibu wanadamu kadiri vilivyoendelea kuzama zaidi na zaidi kwenye machafuko ya uovu.

Nina wahamasisha wasomaji wafanye utafiti zaidi katika "Mabaki" na miji iliyozama. Maarifa yaliyoongezeka ya mabaki ya kale yatakusaidia kuthamini kikamilifu zaidi aina ya ulimwengu ambao Nuhu aliishi na pia zaidi sana kukuimarisha imani kwamba maelezo ya Biblia katika Mwanzo kuhusu Gharika ni kweli.

Utafiti kama huo, na kuangalia dhamiri ya wanadamu inayozorota kuhusu upambanuzi wa mema na mabaya, pia utatumika kama onyo lenye nguvu. Yesu alisema kwamba hakuna mwanadamu ajuaye siku ya kurudi kwake: ***"Kwa maana kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya Gharika watu walivyokuwa wakila, na kunywa, wakioa na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina, wasitambue, hata Gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu"*** (Mathayo 24:37-39).

Je! Hali ya mwanadamu ilikuwaje kabla ya Gharika? ***"Bwana akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu siku zote"*** (Mwanzo 6:5). Kama watu wasioamini katika Mungu na watu wanaojitumainia wenyewe wanavyozidi kuongeza ushawishi wao, wakitawala ujumla wa ujumbe katika mifumo yetu ya kielimu, wanaomwamini Mungu sio tu kwamba wanapoteza vita katika dunia, bali katika maeneo mengi watoto wetu wenyewe wanatolewa kafara katika madhabahu ya wasioamini. Tazama pote: **Ni asilimia ngapi ya watoto waliozaliwa na wazazi wa Kikristo wanaobaki waaminifu baada ya kutoka shule ya sekondari ngazi ya juu, vyuo na ndoa? Ni wangapi wameacha imani zao, na kuoana na watu wasio Wakristo na kamwe hawatakuwa na imani ya kuwaambukiza watoto wao?**

Maandiko ni ya kweli. Gharika katika kitabu cha Mwanzo ni kweli lilitokea, na ni kweli Bwana wetu atarudi tena siku moja. **Je! Tutakuwa tayari?**

## Ushahidi

# MUNGU ALIUMBA ASALI MOJA YA NDEGE

**Dave Everson**



Moja kati ya wanyama wa ajabu aliowaumba Mungu ni ndege aliye na ufahamu wa kuhusu jinsi ya kuwatumia wanadamu na wanyama wengine ili awapeleke katika chakula chake pendwa. Kiumbe tunachokwenda kukizungumzia ni ndege, ndege wa asali wa Afrika (kwa majina mengine wanaitwa: kiongozi, vijumbe au walembe). Ndege hawa wana uwezo wa kushangaza wa kupata chakula kwa kuwaongoza wanadamu na wanyama (kama Nyegere) mpaka katika masega ya nyuki. Halafu, pindi sega linapofunguliwa, ndege huyu ndipo hupata chakula.

Ndege wa asali anatokana na ukoo wa ndege wanaoitwa kwa kitaalam *Indicatoridae*, jina linalotokana na uwezo wa ndege hao kutoa ishara ya mahali ambapo sega la nyuki linapoweza kupatikana. Ukoo huu hasa ufahamika kwa nasaba *Mwashiriaji*, ambapo ndege wa asali hutokea. Makabila ya watu wenyeji wanajua ya kwamba ikiwa watawasikiliza na kuwafuata ndege hawa kwa maili ndani ya poli au msitu, watapata asali nyingi.

Ndege wa asali wanaweza kukumbuka mahali ambapo sega la nyuki linapoweza kupatikana katika eneo kubwa la poli. Pindi ndege hawa wanapohitaji chakula,  humtafuta mtu wamwongoze kwenye chakula. Kwa kutoa sauti kubwa, na kuvuta umakini kwa kutoa ishara huku akirukaruka karibu na watu kwa tahadhari, ndege huyu hutoa ishara ya hitaji la mwanadamu kumfuata. Hapo ndege huyu huruka chinichini, juu kidogo ya mtu na kutoa sauti kubwa; pindi mwanadamu anapotambua, ndege huyo uenda mbele ili kutoa mwongozo, mchakato huo utaendelea mpaka ndege huyo atakapofika eneo sega lilipo. Kisha, ndege huyo atabadilisha mlio wake na kusimama sehemu ya karibu na sega. Mara baada ya mtu huyo kulifungua sega na kupata asali, ndipo ndege huyo atakaposogea na kula vibuyu pamoja na nta za sega la asali. Pia wanafahamika kwa kula mishumaa ya nta. Ndege hawa pia hujaribu aina hiyohiyo ya tabia kumwita Nyegere. Kumekuwa na hisia kuhusu kama nyegere hufuata kwa sababu anajua chakula kitapatikana kwa kumfuata ndege huyu, au labda ndege humfuata nyegere apatapo sega la nyuki.

Ndege wa asali ana ngozi nene ambayo humlinda kutokana na kung’atwa na nyuki wenye hasira baada sega kuwa limevamiwa. Ndege hawa pia wana tabia ya ajabu ya kuzaliana ambayo inategemea ndege wengine, lakini humpendelea zaidi ndege anayeitwa Keremkerem kuwalisha na kuwalea makinda yao.

Tabia hii inaitwa “vimelea vya uzazi.” Mama wa ndege hawa hutafuta kiota cha ndege mmoja kutoka katika aina kadhaa za ndege wengine. Kisha huingia katika kiota hicho na kutaga yai moja tu. Ndege huyu pia anaweza kuchanganya yai lake na yai au mayai ya ndege mwenyeji wa kiota hicho. Hutoboa tundu dogo kwenye ganda ambalo hupunguza kasi au kuzuia maendeleo ya yai alilolikuta. Ikiwa yai lolote kati ya mayai aliyoyakuta katika kiota litaendelea na kutotolewa, kinda la ndege wa asali atawachafua wenzake kwa mdomo wake uliochongoka. Atarudiarudia kitendo hiki na hatimaye kusababisha kifo cha makinda hayo wenyeji. Mama mwenyeji atamlea kinda wa ndege wa asali, ambapo hata atazalisha miito ambayo inaiga mwito wa

makinda ya Karemkarem. Hii inaonekana kuwa ni kichocheo chenye nguvu kwa mama mwenyeji kuleta chakula cha ziada kwa ajili ya mtoto, ambaye baadaye hukua kwa kasi kubwa sana.

Kwa hakika, Mungu ameumba wanyama wa ajabu wanaoshirikiana katika sayari hii tunayoiita dunia, na ndege huyu ni moja kati ya mifano mizuri. Ni vigumu sana kufikiri ni kwa jinsi gani ndege huyu angeweza kujifunza kwamba kumvutia mwanadamu au nyegere angeweza kupata chakula chake kama Mungu hakuumba tabia hii ndani ya ndege wa kwanza. Hata hivyo, inaonekana kwamba watu wengi wanachagua kutoamini kile kilichoumbwa na kudhirishwa mbele ya macho yao.

***"Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uweza wake wa milele na Uungu wake; hata wasiwe na udhuru; kwa sababu, walipomjua Mungu hawakumtukuza kama ndiye Mungu wala kumshukuru; bali walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza. Wakijinena kuwa wenye hekima walipumbazika; wakaubadili utukufu wa Mungu asiye na uharibifu kwa mfano wa sura ya binadamu aliye na uharibifu, na ya ndege, na ya wanyama, na ya vitambaavyo"***

(Warumi 1:20-23)

# ULAGHAI

**Donald R. Fox**

Niishipo katika ulimwengu huu, ni lazima nikiri kwamba nimekuwa nikihadaiwa na kudanganywa mara kadhaa katika maisha yangu. Sio mara nyingi sana, lakini nilikubari mambo fulani yasiyo sahihi wakati nikidhani kwamba yalikuwa sawa. Kwa hiyo, nilipotoshwa. Ni jambo baya kudanganywa. Ni vema na haki kujua ya kwamba daima ukweli utamweka mtu huru***. "Tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru"*** (Yohana 8:32).

Kadiri ninavyotafakari kuhusu udanganyifu na njia isiyo sahihi ya kufikia mafanikio. Najua kwa hakika kuna vitu vichache ambavyo kwa hivyo siwezi kudanganywa. Siwezi kudanganywa kuhusu herufi za maneno ya Kiingereza. Herufi za maneno zimepangwa kwa kipimo maalum. Sasa, sisemi kwamba naweza kuandika herufi zote za maneno ya Kiingereza bila kukosea, hapana, lakini hata hivyo, kwa wakati fulani, naweza kutafuta herufi sahihi kutoka katika historia ya maneno husika. Zaidi sana, katika kamusi kuna orodha ya fafanuzi za maneno.

Hivyo, siwezi kudanganywa katika kile kilicho cha kweli kibiblia na ukweli ambao hautokani na Mungu. Kwa miaka mingi sasa, nimekuwa nikiliamini Neno la Mungu, Biblia. Je! Najua kila kitu kilichomo katika Biblia? Hapana, sijui. Pamoja na hayo, daima naweza kugundua ukweli kwa kutumia kipimo kilichowekwa, Biblia. Je! Unaweza kujua lipi ni jema na lipi ni baya? Kanuni na vipimo vya kibiblia vimekuwa mwongozo wa serikali zilizostaharabika na sheria zao. Zingatia "Sheria ya Dhahabu" ***"Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii"*** (Mathayo 7:12). Hii inatangaza ukweli pekee wa kipimo cha matendo cha ulimwengu. Pilato aliuliza ***"kweli ni nini?"***

(Yohana 18:38). Jibu rahisi ni, ***"Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli"*** (Yohana 17:17).

Tunatambua kuwa kuna siri na mambo yasiyojulikana ambayo yako nje ya uwezo wa ufahamu wa mwanadamu. Ni heri niamini Neno la Mungu kuliko falsafa za wanadamu zilizovurugika na kukinzana. ***"Mambo ya siri ni ya Bwana, Mungu wetu; lakini mambo yaliyofunuliwa ni yetu sisi na watoto wetu milele, ili tuyafanye maneno yote ya sheria hii"*** (Kum. 29:29).

Tutakuwa tunakosea ikiwa tutatafuta majibu ya kibiblia kwa njia za miongozo ya imani za kidini zilizoandikwa na kuthibitishwa na wanadamu wa kawaida. Kuhusu miongozo ya wanadamu, Philip Schaff, katika toleo lake la tatu la kitabu aliandika, *"Kanuni za imani za Kikristo zenye Historia na Maelezo Muhimu"* maelezo haya yanapatikana katika ukurasa wa 4 wa kitabu chake. *"Zinadumisha mizozo ya kimadhehebu na uadui."* Kwa maoni chanya Bw. Schaff anaendelea, *"…lakini pia zinafichua mapatano ya msingi, na zinaonesha uwezekano wa maelewano kwa siku zijazo."* Nathamini matumaini ya Schaff. Hata hivyo, inasikitisha, miongozo ya imani daima italeta "migogoro ya kimadhehebu."

Usidanganywe na taasisi za kidini au kanuni mbalimbali za kitheolojia na kudhani kwamba zina mamlaka ya kutunga sheria katika masuala ya imani au maadili. Chombo hicho cha sheria na viwango vya maadili vilikamilika pindi mwandishi wa mwisho aliyevuviwa alipoandika, ***"Neema ya Bwana Yesu na iwe pamoja nanyi nyote. Amina"*** (Ufunuo 22:21). Ni jambo la kawaida sana kwa siku za leo kusikia tangazo kwamba tunaishi katika kawaida mpya na maadili yake mapya. Huu ni ulaghai mkubwa. Kuna msukumo wa kutengeneza ulimwengu, wa jamii isiyokuwa ya kidini. Jamii yetu inaporomoka kwa sababu tumesahau urithi wetu na kwa sababu ya kukataa viwango vya maadili vilivyowekwa na Mungu. ***"Kwa mausia yako najipatia ufahamu, Ndiyo maana naichukia kila njia ya uongo"*** (Zaburi 119:104).

## Neno la Mungu

# NENO LINALOISHI

Patrick Morrison

Wapo wale wasemao kuwa Biblia si chochote bali ni waraka mfu, kwamba haina nguvu yoyote ya kushawishi au kutia hatiani, kwa kuwa, haina uzima. Wengi wanadai kwamba Maandiko hayaeleweki bila ya uingiliaji kati wa Mungu juu ya Neno au mwanafunzi wa Neno kulihuisha na kulifanya kuwa hai. Kuna mengi yanayosemwa kuhusu jinsi ambavyo Roho wa Mungu anavyotembea miongoni mwa watu au anavyowasaidia watu kuelewa Neno la Mungu. Je! Madai haya ni ya kweli? Je! Neno la Mungu, Biblia, si chochote bali ni waraka mfu, na ya kwamba inamlazimu Mungu kufanya jambo kwa njia fulani za ajabu (miujiza) ili mradi Neno lake liweze kuzungumza nasi leo hii?



Kitu kinachokosekana katika mjadala huu ni ukweli ya kwamba Mungu, tayari amefanyia kazi Neno lake na kulifanya liwe hai na kutenda kazi. Paulo alimkumbusha Timotheo kwamba, ***"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu"*** (2 Timotheo 3:16). Hiyo ina maanisha kwamba Neno la Mungu linatoka katika pumzi ya Mungu mwenyewe. Pumzi ya Mungu ndiyo iliyosababisha udongo uliofinyangwa kwa umbile la mtu asiye na uhai kuwa nafsi hai (Mwanzo 2:7). Mungu alimpa mwanadamu na Neno lake uzima katika njia moja: Alipulizia pumzi ya uhai kwa wote wawili! Mungu, kwa njia ya Roho Mtakatifu, aliyapa uhai mapenzi yake yaliyofunuliwa kwa mwanadamu. Petro aliandika, ***"Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na***

***Roho Mtakatifu"*** (2 Petro 1:21). Roho Mtakatifu ndiye aliyelileta Neno la Mungu lenye thamani kwa mwanadamu! Aliwaongoza watu hawa waliovuviwa walipokuwa wakiandika Neno hilo kwa ajili ya vizazi vya baadaye. Licha ya yote, ni, ***"upanga wa Roho"*** (Waefeso 6:17). Hakuna neno litokalo kwa Mungu, Kristo au Roho Mtakatifu lisilokuwa na uzima! Yesu alisema, ***"Roho ndiyo itiayo uzima, mwili haufai kitu; maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima"*** (Yohana 6:63). Je! Hatupaswi kutarajia kwamba Neno litaleta ujumbe ulio hai utokao kwa Baba, utendao kazi na kuokoa?

Wale walioagizwa kuandika kwa uaminifu Neno la Mungu waliongozwa kuandika kuhusu nguvu ya ufunuo wa mapenzi ya Mungu. Roho mwenyewe alikuwa akitumia mikono ya watu waliovuviwa kuzielekeza nafsi zote kwa Bwana kwa njia ya Injili. Aliweka nguvu katika ujumbe ili kwamba watu waweze kuokolewa kwa kulisikia na kutii. Watu hawa waliovuviwa wasingepewa kazi hii ya uandishi ili kwamba Neno la Mungu likose nguvu au kwamba liwe waraka mfu. Kinyume chake! Yakobo aliandika, ***"Kwa hiyo wekeeni mbali uchafu wote na ubaya uzidio, na kupokea kwa upole neno lile lililopandwa ndani, liwezalo kuziokoa roho zenu"*** (Yakobo 1:21). Paulo alielewa kwamba ujumbe wa Injili una nguvu sana; ***"Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia"*** (Warumi 1:16). Alielewa kwamba nguvu iliyopo kwenye ujumbe iliwekwa na Mungu aliye hai! Mwandishi wa kitabu cha Waebrania pia alitambua nguvu ya Maandiko, ***"Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo"*** (Waebrania 4:12). Neno la Mungu li hai! Roho wa Mungu alitenda kazi juu ya Neno pindi alipowaongoza wale waandishi waliovuviwa. Neno la uzima linatokea katika chanzo cha uzima. Daima litakuwa na uzima ndani yake, kwa ajili ya Mungu aliye hai aliyelitoa. Kamwe halitakufa!

# Ikiwa Unadai Kuwa Uliokolewa Kabla ya Ubatizo...

Alvin Jennings

1. **Uliokoka kabla dhambi zako hazijasamehewa**. *“Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu”* (Matendo 2:38).
2. **Uliokoka kabla dhambi zako hazijaoshwa.** *“Simama ubatizwe, ukaoshe dhambi zako,”* (Matendo 22:16).
3. **Uliokoka kabla hujazaliwa upya.** *“Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia katika ufalme wa Mungu”* (Yohana 5:3).
4. **Uliokoka kabla hujaunganishwa na Kristo.** *“Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo”* (Wagalatia 3:27).



5. **Uliokoka kabla hujaokolewa.** *"..ni ubatizo, unaowaokoa ninyi"* (1 Petro 3:21).

6. **Uliokoka kabla ya muda ambao Bwana aliahidi kuokoa.** *"Aaminiye na kubatizwa ataokoka…"* (Marko 16:16).
7. **Uliokoka kabla hujakombolewa kutoka katika dhambi.** *"Lakini Mungu na ashukuriwe, kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake; na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki"* (Warumi 6:17-18).
8. **Uliokoka kabla hujaingia ndani ya Kristo na bila ya damu yake.** *"Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake"* (Waefeso 1:7).
9. **Uliokoka kabla roho yako haijatakaswa.** *"Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli"* (1 Petro 1:22a).
10. **Uliokoka kabla hujampokea Roho Mtakatifu na bila ya kumilikiwa na Mungu.** *"…Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wamtiio"* (Matendo 5:32; pia 2:38). *"Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake"* (Warumi 8:9b).
11. **Uliokoka bila ya roho yako kuwa na thamani yoyote, kabla ya kutenda kazi kwa upendo.** *"…bali imani itendayo kazi kwa upendo"* (Wagalatia 5:6).
12. **Uliokoka bila ya utii, ambao Yesu aliuhitaji kwa wote wapokeao wokovu.** *"8 na, ingawa ni Mwana, alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata; naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii;"* (Waebrania 5:8-9).

## Toba

Cecil May, Jr

Toba ya kweli huleta matokeo ya mabadiliko ya mwenendo (Yohana Mbatizaji, Luka 7:7-8). Hata hivyo, kutumbukia katika dhambi tena (na tena, na tena) haimaanishi kuwa toba haikufanyika ***"mpaka 7 mara 70"*** (Yesu, Mathayo 18:21-22).

## Wokovu

# Sauli Alikuwa Wapi Alipookolewa?

Royce Frederick

Mmoja kati ya maadui wabaya kabisa wa Yesu alikuwa Sauli wa Taso. Bila huruma alilitesa kanisa lililokuwa Yerusalemu na kuwatawanya (Matendo 8:1-4). Kisha, akawafuata Wakristo katika miji mingine, akitumaini kuitokomeza imani yao (Matendo 26:11). Pia, ***"…akamwendea Kuhani Mkuu, akataka ampe barua za kuenda Dameski zilizoandikwa kwa masinagogi,*** (Eneo la Kiyahudi la kuabudia) ***ili akiona watu wa Njia hii, waume kwa wake, awafunge na kuwaleta Yerusalemu"*** (Matendo 9:1-2).

Hata hivyo, ujumbe ambao Sauli aliuwasilisha katika masinagogi huko Dameski ulikuwa **tofauti sana** na ule alioukusudia: ***"Mara akamhubiri Yesu katika masinagogi, kwamba yeye ni Mwana wa Mungu"*** (Matendo 9:20)!

Ni nini kilchobadilisha **akili** na **ujumbe** wa Sauli ? Akiwa njiani kuelekea Dameski, Yesu alimtokea katika mwangaza mkali, na akaanguka chini. Baada ya Yesu kuzungumza naye, Sauli akasimama, akafungua macho yake lakini hakuweza kuona. Kwa msaada wa washirika wake, akaenda Dameski. Akiwa katika mji hakuweza **kuona**, **kula** au **kunywa** kwa siku tatu, bali **alikuwa akiomba** (Matendo 9:3-9, 11). Baadaye, katika nyaraka zake, alijijumuisha yeye mwenyewe pamoja na watu wote "waliookoka" (1 Timotheo 1:15-16; 2 Timotheo 1:8-9; Tito 3:5).

**Kwa hiyo, Sauli alikuwa wapi pindi alipookolewa?** Watu wengi wanafundisha kwamba Sauli aliokolewa "kwa imani pekee" wakati wa tukio lile kubwa alipokuwa **njiani kuelekea Dameski**. Mhubiri mmoja hata aliwahi kusema kwamba Sauli aliokolewa wakati alipokuwa akianguka kutoka katika mgongo wa farasi, kabla hata hajagusa ardhi! Pamoja na hayo, Biblia haitaji uwepo wa farasi hata kidogo. Kwa kweli, Sauli na washirika wake walikuwa wakitembea. Baada ya Bwana kumpiga kwa upofu, washirika wa Sauli ***"…wakamshika mkono***

***wakamleta mpaka Dameski"*** (Matendo 9:8; 22:11). Wazo la kuongeza farasi katika kisa hiki lilitokea kwa wanadamu, na wala si kwa Mungu. Vivyo hivyo, na wazo la Sauli kuokolewa akiwa **barabarani** linatoka katika mawazo ya wanadamu, wala sio kutoka katika ufunuo wa Mungu.

Kwa kweli, Biblia inatuambia kuwa Sauli aliokolewa baada ya kwenda Dameski, sio alipokuwa njiani. Sauli kipofu alikuwa akisubiri ndani ya nyumba huko Dameski pindi Yesu alipomtuma Anania kwake. Anania alimponya, akazungumza naye kuhusu Yesu na kumalizia kwa kusema, ***"Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake"*** (Matendo 22:16). Hii inaonesha wazi kwamba Sauli **hakuwa tayari ameokolewa** alipokuwa njiani. **Bado alikuwa na dhambi zake** pindi Anania alipozungumza naye **siku ya tatu** baadaye huko Dameski. Baada ya Anania kuzungumza, Sauli hakuhitaji kusubiri zaidi. Kwa njia ya imani katika Kristo, aliitii Injili siku hiyo; ***"…akasimama, akabatizwa"*** (Matendo 9:18). Dhambi zake zilioshwa kwa damu ya Yesu pindi alipobatizwa katika Kristo. Sauli aliokolewa kwa **neema** ya Mungu, kwa njia ya imani, **pindi** alipobatizwa.

Yesu awatokei watu leo hii kama alivyofanya kwa Sauli. Hata hivyo, Yesu **bado anatubariki** kupitia tukio lile kubwa katika maisha ya Sauli, ambaye baadaye aliitwa "Paulo" (Matendo 13:9). Akawa mtume wa Kristo aliyejitoa sana na kuwaongoza Mataifa na Wayahudi wengi katika wokovu!

Kupitia Paulo, Bwana alituambia kuwa sehemu ya wokovu ni ***"katika Kristo"*** (Warumi 8:1; 2 Wakorintho 5:17; 1 Wathesalonike 4:16; 1 Petro 5:14). Aliwakumbusha Wakristo wa Galatia jinsi walivyoingia katika Kristo, ***"Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo"*** (Wagalatia 3:26-27). Aya hizi, na aya nyingine nyingi, zinaonesha kwamba mwenye dhambi anayemwamini Kristo anaokolewa kutoka katika dhambi zake **wakati wa ubatizo** (Yohana 3:16; 3-5; Warumi 6:3-5; Wakolosai 2:12).

## Wokovu

# WAKATI GANI NA KIVIPI MTU HUOKOLEWA?

Sunny David

Kinyume na mafundisho na maoni ya wanadamu kuwa mtu anaokoka mara tu anapomwamini Kristo au mtu anapoongozwa sala ya toba, Biblia kwa uwazi inafundisha kwamba kuokolewa katika Kristo mtu ni lazima asikie ujumbe wa Injili yake na kuiamini, kutubu dhambi zake, kumkiri Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu na kubatizwa katika Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Hii haimaanishi kwamba haya ndiyo yote ambayo mtu anastahili kufanya ili kuokolewa na kwenda mbinguni, lakini kila mmoja lazima afuate hatua hizi za awali ili aanze safari ya Ukristo.

Wakati Kristo alipokuwa akienda Mbinguni, aliwaagiza wanafunzi wake, ***"enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; Asiyeamini atahukumiwa"*** (Marko 16:15-16). Kristo hakuishia kwenye ***"aaminiye"*** lakini alisema ***"aaminiye na kubatizwa ataokoka."*** Wahubiri wanaotoa wokovu kwa **"imani peke yake"** wanawadanganya watu (Warumi 16:17-16).

Hivyo, kuna wale ambao wanasisitiza kwamba ni lazima mtu awe na nguvu zisizo za kawaida ili aokolewe au **"kuzaliwa mara ya pili"** wazo ambalo halina mantiki na sio la kimaandiko. Mtazamo huu, hutetewa kwa namna mbalimbali, inadhaniwa kwamba wakati fulani fulani, akiwa na hisia bora kuliko kuambiwa, katika kujibu maombi, chini ya msukumo wa kihisia wa uamsho au katika hali nyingine za ajabu, mwenye dhambi hupata imani ghafla. Wakati huo, inadaiwa kwamba dhambi zake zote zinakuwa zimesamehewa, anabadilishwa kiroho, amezaliwa mara ya pili na kuokolewa milele. Baadhi wanadai kupitia hali hiyo wakati wakiwa wamelala, ghafla wanaona maono,

kama vile wanavyosema, mbingu zinafunguka na kusikia mtu akizungumza nao na kuwahakikishia kuwa wameokolewa. Hii kwa ujumla ni upuuzi! Hakuna agizo la kibiblia au mfano hata mmoja unaodokeza jambo kama hilo. Katika matukio yote ya uongofu kama ilivyoelezwa kwenye kitabu cha Matendo ya mitume, hakuna aliyemjia Kristo au kufanyika Mkristo kwa dhana potofu kama hiyo.

Kwa upande mwingine, hakuna hali ambayo mtu yeyote amekumbana nayo ambayo ingeshinda ile ya Sauli (Paulo) katika barabara ya Dameski. Kwa hakika alimwona Bwana. Hata hivyo, siku tatu baadaye, kama tunavyosoma, alikuwa bado mtu wa maombi na mwenye dhambi na mwenye huzuni, kwa hiyo, alibakia hivyo hadi alipozingatia amri ya Mungu aliyopewa kupitia Anania ***"Simama, ubatizwe, ukaoshwe dhambi zako" (***Matendo 22:16), Matendo 9:18 inasema ***"akasimama, akabatizwa."*** Ukweli wa jambo hili ni kwamba mtu anapaswa kuamini na kutii ili kuokolewa sio kuamini pekee (Yakobo 2:24,26).

Kuna mifano mingine mingi inayopatikana katika kitabu cha Matendo ambacho kwa kawaida kinakubalika kama kitabu cha uongofu, ambacho kinaonyesha matukio yote ambapo watu wliokolewa kutoka dhambini na kufanyika Wakristo, wote waliamini na kuitii Injili. Kwa mfano, mkusanyiko mkubwa wa watu ,baada ya kuisikia Injili ya Kristo, waliwauliza Mitume ***"tutendeje ndugu zetu?"*** Jibu walilopewa ni, ***"Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu"*** (Matendo 2:37-38).

Tena, mwinjilisti Filipo alipoingia Samaria na kumhubiri Kristo huko, tunasoma katika Matendo 8:12 kwamba ***"wakabatizwa, wanaume na wanawake."*** Kitambo kidogo baadaye, katika sura hiyohiyo, tunasoma kuhusu uongofu wa kanisa. Pale tunasoma kuanzia aya ya 35, Filipo anamhubiri Kristo kwa Towashi walipokuwa wakisafiri kwenye gari lake ***"wakafika mahali penye maji, yule Towashi akasema, tazama maji haya; ni nini kinanizuia nisibatizwe? Filipo akasema ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana. Akajibu***

***akanena, Naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu. Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi; naye akambatiza”*** (Matendo 8:35-38). Kwa uwazi mtu anaweza akaona kutokana na mifano hii yote ya uongofu kwamba kuna muundo unaotolewa na Biblia ili kujifunza juu ya lini na kivipi mtu anaokolewa.

Pale mtu anapomwamini Kristo hubadili mawazo yake. Mtu anapotubu dhambi zake, hubadili matakwa yake. Halafu, anabatizwa, kwa kuzamishwa kwenye maji kwa ajili ya ondoleo la dhambi au kuoshwa dhambi, anabadili uhusiano wake au sehemu yake ya kuwa mtu wa dunia, na kwa sasa yuko ndani ya Kristo. Wakati wa ubatizo mtu anashiriki kifo cha Kristo kwa kuungana na damu ya Kristo inayookoa, ambayo ilimwagika katika kifo chake kwa ajili ya wenye dhambi.

Kwa hiyo, Maandiko yanafundisha ***“Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima”*** (Warumi 6:3-4). Kwa kubatizwa, mtu anazamishwa kwenye maji mengi, na maji yanamfunika mwili mzima. Kama vile maiti inavyozikwa, ndivyo mtu anavyozikwa kwenye ubatizo. Halafu, anainuliwa juu kutoka kwenye kaburi la maji ili atembee katika maisha mapya ya Ukristo. Yote haya yanaonyesha kuwa mtu huyo alikufa katika aina moja ya maisha na kufufukia katika aina nyingine ya maisha. Alikwenda chini kwenye maji mtu wa dunia na kuibuka akiwa mtu wa Kristo, mtu tofauti, mtu mpya (2 Wakorintho 5:17). Njia ya Mungu Ndiyo Njia pekee ya uhakika.

***“Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima”***

## Tafuta Aya




1. "Kikombe cha Baraka" alichokirejerea Paulo ni nini? (mst. 16).
2. Mkate unaashiria nini? (mst. 16)
3. Ingawa Wakristo ni washirika wengi, tunaunda _________mmoja na _____________ (mst. 17).
4. Wakristo hawakutakiwa kuwa na ushirika na kitu gani? (mst. 20).
5. Wakristo walipotoa dhabihu kwa sanamu, walikuwa na hatia ya kujaribu kukinywea kikombe cha _________ na kikombe cha ________ (mst. 21).
6. Je, ni faida ya nani wanayopaswa Wakristo kuitafuta? (mst. 24).
7. Kwa nini Wakristo wangeweza kula chochote kilichopatikana masokoni bila ya kuuliza? (mst. 25).
8. Je. Wakristo walipaswa kufanya nini ikiwa walikwenda kula katika nyumba ya mtu mwingine? (mst. 27).
9. Je, wangepaswa kufanya nini ikiwa wangeambiwa kuwa chakula hicho kilitolewa kafara kwa sanamu? (mst. 28).
10. Je, ni kwa ajili ya dhamiri ya nani ambayo Paulo aliijali pindi alipotoa amri ya zuio hapo juu? (mst. 29).
11. Chochote tunachokifanya, kula au kunywa, inatakiwa kufanyika kwa ajili ya ____________ (mst. 31).
12. Je, Paulo alikuwa akitafuta faida ya nani? (mst. 33).

***14*** Kwa ajili ya hayo, wapenzi wangu, ikimbieni ibada ya sanamu.
***15*** Nasema kama na watu wenye akili; lifikirini ninyi ninenalo. ***16*** Kikombe
kile cha baraka tukibarikicho, je! Si ushirika wa damu ya Kristo? Mkate ule
tuumegao, si ushirika wa mwili wa Kristo? ***17*** Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi
tulio wengi tu mwili mmoja; kwa maana sisi sote twapokea sehemu ya ule
mkate mmoja.

***18*** Waangalieni hao Waisraeli walivyokuwa kwa jinsi ya mwili; wale
wazilao dhabihu, je! Hawana shirika na madhabahu? ***19*** Basi niseme nini? Ya
kwamba kile kilichotolewa sadaka kwa sanamu ni kitu? Au ya kwamba
sanamu ni kitu? ***20*** Sivyo, lakini vitu vile wavitoavyo sadaka wavitoa kwa
mashetani, wala si kwa Mungu; nami sipendi ninyi kushirikiana na mashetani.
Hamwezi kunywea kikombe cha Bwana na kikombe cha mashetani.
***21*** Hamwezi kushirikiana katika meza ya Bwana na katika meza ya mashetani.
***22*** Au twamtia Bwana wivu? Je! Tuna nguvu zaidi ya yeye?

***23*** Vitu vyote ni halali; bali si vitu vyote vifaavyo. Vitu vyote ni halali;
bali si vitu vyote vijengavyo. ***24*** Mtu asitafute faida yake mwenyewe, bali ya
mwenzake.

***25*** Kila kitu kiuzwacho sokoni kuleni, bila kuuliza-uliza, kwa ajili ya
dhamiri; ***26*** maana, Dunia ni mali ya Bwana na vyote viijazavyo.

***27*** Na mtu asiyeamini akiwaalika, nanyi mnataka kwenda, kuleni kila
kitu kiwekwacho mbele yenu bila kuuliza-uliza, kwa ajili ya dhamiri. ***28*** Lakini
mtu akiwaambia, Kitu hiki kimetolewa kiwe sadaka, msile, kwa ajili yake yeye
aliyeonyesha, na kwa ajili ya dhamiri. ***29*** Nasema, dhamiri, lakini si yako, bali
ya yule mwingine. Maana kwa nini uhuru wangu uhukumiwe na dhamiri ya
mtu mwingine? ***30*** Ikiwa mimi natumia sehemu yangu kwa shukrani, kwa nini
nitukanwe, kwa ajili ya kitu nikishukuriacho?

***31*** Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote
kwa utukufu wa Mungu. ***32*** Msiwakoseshe Wayahudi wala Wayunani wala
kanisa la Mungu, ***33*** vile vile kama mimi niwapendezavyo watu wote katika
mambo yote, nisitake faida yangu mwenyewe, ila faida yao walio wengi,
wapate kuokolewa.

**UJUMBE**: Kifungu hiki kinahusu ulaji wa nyama zilizotolewa kafara kwa sanamu. Ingawa tatizo hilo halipo katika sehemu nyingi za ulimwengu leo hii, lakini kanuni yake bado inafanya kazi. Tunatakiwa kujali faida za kiroho za wengine kuliko haki zetu. Ingawa tendo lenyewe si baya, lakini inabidi tuliepuke ili tusimkwaze ndugu Mkristo. Tufanye yale yanayojenga.



# Dakika 5 Za Kujifunza Biblia

**Paula Bates**

## Kumkufuru Mungu

1. "Nami namshukuru Kristo Yesu Bwana wetu, aliyenitia nguvu kwa sababu aliniona kuwa mwaminifu, akaniweka katika________; ingawa hapo kwanza nalikuwa______, mwenye kuudhi watu, mwenye jeuri, lakini nalipata _______ kwa kuwa nalitenda hivyo kwa ujinga, na kwa kutokuwa na imani." (1 Timotheo 1:12-13).
2. "uwe mwenye imani na _______njema, ambayo wengine wameisukumia mbali, wakaangamia kwa habari ya Imani. Katika hao wamo Himenayo na Iskanda, ambao nimempa _______watu hao, ili wafundishwe wasimtukane Mungu." (1 Timotheo 1:19-20).
3. "________walio chini ya kongwa, hali ya utumwa, na wawahesabie bwana zao kuwa wamestahili_______yote, jina la Mungu lisitukanwe wala ________yetu." (1 Timotheo 6:1)
4. "Akafunua _______ chake amtukane Mungu, na kulitukana_____, na maskani yake, nao wakaao__________." (Ufunuo 13:6)
5. "Basi, wale waandishi na Mafarisayo wakaanza ______wakisema, Ni nani huyu asemaye maneno ya________? Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa ________ peke yake?" (Luka 5:21)
6. "Naijua ________ yako na umaskini wako, (lakini u tajiri) najua na matukano ya hao wasemao ya kuwa ni Wayahudi, nao ____, bali ni sinagogi la Shetani. Usiogope mambo yatakayokupata; tazama, huyo Ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili _______, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe __________ hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima." (Ufunuo 2:9-10)

1. utumishi wake, mtukanaji, rehema
2. dhamiri, Shetani
3. Wo wote, heshima, mafundisho
4. Kinywa, jina lake, mbinguni
5. Kuhojiana, kukufuru, Mungu
6. Dhiki, sio, mjaribiwe, mwaminifu

**Majibu:**

# Sababu za Ukuaji wa Kiroho na Kiidadi

Ronald D. Reeves

Miaka michache iliyopita, ndugu walijitoa kupata ufahamu mzuri wa mambo ambayo huleta mchango mkubwa katika ukuaji wa kanisa. Nyaraka za utafiti pamoja na juhudi kubwa zilituhamasisha kusonga mbele na kufanyia kazi yafuatayo:

1. **Uaminifu katika maisha ya kila siku ya Kikristo:** Washirika wanafahamika kwa wema kadiri wanavyoziongoza familia zao katika utauwa.
2. **Uthabiti wa kujitoa kwa Kristo:** Washirika waoneshe kujitoa kwao kwa dhati katika masuala ya kiroho.
3. **Kushughulika kwa bidii katika ufalme wa Mungu:** Washirika hawapaswi kuridhika kwa kuwafuata wachache wanaofanya karibu kazi zote za kanisa.
4. **Ukuaji halisi wa kiroho wa mtu binafsi:** Washirika wawe na njaa na kiu ya haki.
5. **Dhabihu ya maisha ya Kikristo:** Washirika wasisite kujitoa dhabihu kwa ajili ya Kristo.
6. **Upendo wa kanisa la Agano Jipya:** Washirika walijali kanisa kama wanavyozijali familia zao binafsi.
7. **Upendo kwa ajili ya roho za watu:** Uzingatiaji wa jamii na maadili visiwe kikwazo cha kutafuta na kuokoa waliopotea.

Mambo haya saba yatatusaidia sana kwa kadiri tunavyopigana vita vizuri (2 Timotheo 4:7). Basi na tukue katika kila eneo mojawapo ya haya.

# Maswali Matatu Muhimu

Jimmy Clark

***"Je! Kristo amegawanyika? Je! Paulo alisulibiwa kwa ajili yenu? Au je! Mlibatizwa kwa jina la Paulo?"*** (1 Wakorinto 1:13). Maswali haya matatu yamewekwa dhidi ya usuli ufuatao. ***"Basi ndugu, nawasihi, kwa jina lake Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja. Kwa maana, ndugu zangu, nimearifiwa habari zenu na wale walio wa nyumbani mwa Kloe, ya kwamba iko fitina kwenu. Basi, maana yangu ni hii, ya kwamba kila mtu wa kwenu kusema, mimi ni wa Paulo, na, mimi ni wa Apolo, na mimi wa Kefa, na, mimi ni wa Kristo"*** (1 Wakorintho 1:10-12). Ombi lililotolewa na Paulo katika mstari wa 10 linaungwa mkono kikamilifu na maswali haya matatu. Maswali yote matatu ni maswali balagha yenye majibu hasi. Fikiria mawazo yanayotoka katika maswali haya matatu muhimu.

**Swali kuhusu mgawanyiko:** *"Je! Kristo amegawanyika?"* Ulimwengu wa kidini umegawanyika sana na wengi wana amini kuwa hilo linakubalika kwa Mungu. Yesu aliomba kwa ajili ya umoja ( Yohana 17:20-21). Yesu alikufa ili waamini waweze kuungana katika kanisa lake (Mathayo 16:15-23; Matendo 20:28). Mitume walitenda kazi ili wote waliotii injili wawe na ushirika mmoja ambao wao walikuwa nao na Bwana (1 Yohana 1:1-3). Ni hekima ya kibinadamu iliyoleta tatizo la mgawanyiko wa kidini. Uvumbuzi wa kanuni za Imani nje ya Biblia, mashirika yasiyoungwa mkono na Biblia na mafundisho yanayopingana na mafundisho ya wazi ya Biblia ambayo yameunganisha madhehebu. Kwa kuwa kuna Bwana mmojatu (Waefeso 4:5), basi kutakuwa na mwili mmoja tu (Waefeso 4:4).

**Swali kuhusu ibada**: ***"Je! Paulo alisulibiwa kwa ajili yenu?"*** Paulo alitoa maombi binafsi katika swali ili kuondoa wazo lolote la kujitolea kwake (au kwa mtu mwingine yeyote). Utukufu na heshima

zote zinapaswa kutolewa kwa Bwana pekee. Dhabihu ya Yesu msalabani inaweka ibada yote kwa Bwana. Paulo aliandika katika barua ya pili kwa Wakorintho, ***“Maana, upendo wa Kristo watubidisha; maana tumehukumu hivi, ya kwamba mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi walikufa wote; tena alikufa kwa ajili ya wote, ili walio hai wasiwe hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao”*** (2 Wakorintho 14:15). Paulo alitoa maoni hayo binafsi pale aliposema, ***“na uhai nilionao sasa katika mwili, ninao katika Imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu”*** (Wagalatia 2:20). Paulo aliokolewa kwa ajili ya Kristo na sio kwa ajili ya mwanadamu.

**Swali kuhusu uwanafunzi: “Je! Mlibatizwa kwa jina la Paulo?”** Yesu aliwaambia mitume, ***“Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu”*** (Mathayo 28:19). Wakati Wakorintho wengi walipobatizwa kama ilivyonukuliwa kwenye Matendo 18:8, hawakufanyika wafuasi wa Paulo, bali walifanyika wafuasi wa Kristo. Bwana mwenyewe alimwambia Paulo kuhusu yeye kubaki huko Korintho ***“Usiogope bali nena, wala usinyamaze, kwa kuwa mimi ni pamoja nawe, wala hapana mtu atakayekushambulia ili akudhuru; kwa maana mimi nina watu wengi katika mji huu”*** (Matendo 18:9-10). Kila kitu katika ubatizo kinawaunganisha waamini waliotubu pamoja na Kristo, na sio mwingine. Wakati utu wa kale unapokuwa umesulibiwa pamoja na Kristo (Warumi 6:6). Mtu anazikwa pamoja na Kristo katika kifo chake kupitia ubatizo katika kifo (Warumi 6:4). Mtu anafufuka na Kristo kutoka kwenye kaburi la maji (Warumi 6:4-5). Ubatizo unamsogeza mtu kwa Kristo (Wagalatia 3:27).

***“Maana, upendo wa Kristo watubidisha; maana tumehukumu hivi, ya kwamba mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi walikufa wote; tena alikufa kwa ajili ya wote, ili walio hai wasiwe hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao”***

# Yesu ni Kielelezo Chetu



Greg Tidwell

Ukristo sio mfumo baridi usioonekana. Badala yake imani ya Kikristo inatengeneza uhusiano wa mtu binafsi na Mungu aliye hai kupitia Mwanawe, Yesu Kristo. Mwana wa Mungu ndiye njia yetu, kweli yetu na uzima wetu. Kanisa la Bwana ni lazima litunze makubaliano yake katika kweli ya Bwana. Watu wa Kristo ni lazima watunze makubaliano yao kwa Kristo.

Mapenzi ya Bwana yamewasilishwa katika kanisa katika njia mbili ambazo ni, kwa amri za moja kwa moja na kwa njia ya mfano wake. Yesu, Mwana wa milele wa Mungu, ndiye kielelezo chetu halisi kwa ajili ya utauwa. Kuondoka kwa aina yoyote kutoka katika aina hii ya mafundisho ni hatua ya kuangukia katika uzushi.

Kupitia kielelezo chake, Yesu alituonesha jinsi wafuasi wake wanavyopaswa kuishi katika maisha yao. Maisha ya Kristo yameelezwa katika vitabu vinne vya Injili vikitoa kielelezo thabiti cha upendo, imani na utii kwa kanisa la Bwana. Tumeitwa kufuata kielelezo cha Yesu katika kila nyanja ya maisha.

Imani ya kweli na utiifu wa kweli ni kitu kimoja. Imani si hisia za kawaida, na utiifu sio tu kuenenda kwa kawaida. Ujumbe wa Injili unahusisha mambo yote katika maisha. Yesu alituonesha njia. ***"Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi"*** (Yohana 14:6).

### Kanisa

# Wakristo na Kanisa

Dan R. Owen

Je! Kanisa la Bwana lina umuhimu kiasi gani kwako? Je! Unalipenda kanisa, na kuliombea mara kwa mara na kulisaidia kwa fedha na huduma yako? Utafiti wa hivi punde uliofanywa kupitia shule ya dini ya Chuo Kikuu cha Duke ulifunua kwamba Wamarekani wengi wanathamini uhusiano wao na Mungu, lakini wana shauku kidogo na kanisa. Asilimia hamsini na tatu ya Wamarekani walioishi kabla ya vita walikuwa wakiudhuria katika kanisa fulani wakati wa ukuaji wao. Kiwango hicho kimeshuka hadi asilimia 45 na kuendelea zaidi hadi asilimia 35 kwa kizazi cha leo. Watu leo wanasema kwamba wamejitoa kwa Mungu, lakini si kwa kanisa. Nalipenda kanisa la Bwana, kwa sababu kanisa ndiyo sababu ya Yesu kuja ulimwenguni.

Kusudi la Yesu kuja katika ulimwengu huu lilikuwa ni kuanzisha kanisa lake. Aliitazama siku ya hatima yake huko Yerusalemu, Yesu aliwambia wanafunzi wake, ***"...juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda"*** (Mathayo 16:18). Petro alikuwa ametoka kumkiri Yesu kuwa ni Kristo. Katika siku ya Pentekoste, kilele cha ujumbe wa Injili illikuwa ya kwamba Mungu alimfanya Yesu ***"kuwa Bwana na Kristo."*** Walikuwa ni watu wale waliomtambua Yesu Kristo kama Bwana na Mfalme wa maisha yao, wale ambao ***"walipokea ujumbe wake kwa furaha"*** na kufanyika kuwa washirika wa kwanza wa kanisa. Ni kwa kujianzisha mwenyewe kama Bwana wa ulimwengu hivyo, Yesu akaanzisha kanisa, kwa sababu kanisa linaundwa na wale ambao wamejisalimisha kwake kama Bwana na Mfalme.

Yesu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea (Luka 19:10). Wanadamu ***"wamepotea"*** kwa sababu ya dhambi zao. Hatia ya dhambi inawatenga watu na Mungu wao kwa hiyo, watu hao ni ***"wafu kwa sababu ya makosa na dhambi," "wametengwa na Kristo"*** na ***"hawana tumaini wala Mungu duniani."*** Watu waliopotea hawana

chochote cha kutazamia isipokuwa kumiminwa kwa ghadhabu ya Mungu (Warumi 1:18; 2:7-8). Ni kwa njia ya kuhesabiwa haki pekee kwa damu ya Yesu ndipo watu wanapoweza ***“kuokolewa na ghadhabu ya Mungu”*** (Warumi 5:8-9). Pindi Yesu alipokufa msalabani kama dhabihu isiyokuwa na hatia, alifanya hivyo ili awaokoe waliopotea. Hata hivyo, ni wale pekee wanaosikia mahubiri ya upatanisho kwa njia ya kifo cha Yesu na kuitikia wito wa Injili hiyo kwa imani, kutubu na kubatizwa ndio wanaookolewa na dhambi, na ghadhabu ya Mungu. Bwana anawazidisha wote waliookolewa katika kanisa (Matendo 2:41, 47). Kwa hiyo, kusema kwamba Yesu alikuja kutafuta na kuokoa waliopotea ni sawa na kusema kwamba alikuja kuanzisha kanisa.

Yesu alikuja kutoa maisha yake kama fidia kwa ajili ya wengi (Marko 10:45), fidia ni malipo ambayo kwayo mtu huachiliwa huru kutoka katika deni lisilolipika. Ni katika Kristo tu ndio tunapata ***“ukombozi kwa damu yake”*** (Waefeso 1:7). Kwa njia ya damu ya Yesu deni letu la hatia lisilolipika limelipwa lote. Jeshi la mbinguni linamsifu Yesu ambaye ***“alimnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa”*** (Ufunuo 5:9). Paulo aliwaambia wazee wa Efeso ***“kulichunga kanisa lake Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe”*** (Matendo 20:28). Hivyo, kusema kwamba Yesu aliyatoa maisha yake kama fidia kwa ajili ya roho zetu ni sawa na kusema kwamba alikuja kulijenga kanisa lake. Kanisa linahusu usuluhishi baina ya mwanadamu na Mungu. Ni kiini cha mpango wa milele wa ukombozi wa Mungu.

Kwa kuwa haya yote ni kweli, kanisa linapaswa kuwa ndio kitu muhimu zaidi kwetu hapa duniani. Tunapaswa kulipenda, kulitumikia, kuliwezesha na kuliombea daima. Tunapaswa kufanya mabo haya kwa sababu kwa kufanya hivyo ndipo tunapomtumikia Bwana wetu Yesu Kristo ambaye ***“alijitoa nafsi yake kwa ajili ya kanisa”*** (Waefeso 5:25). Kama tunampenda Yesu, basi tutalipenda na kanisa lake.



# Tafuta Katika Biblia

Martha Rushmore

## Filemoni

1. Je! Ni kwa babu gani Paulo alikuwa na ujasiri kuhusu Filemoni? (mst. 2)

2. Paulo alihitaji nini kutoka kwa Filemoni? (mst. 20).

3. Erasmo alikuwa nani kwa mtume Paulo? (mst. 16).

4. Ni nani aliyekuwa mfungwa mshirika pamoja na Paulo katika Kristo? (mst. 23).

5. Ni nani aliyeandika waraka kwa Filemoni? (mst. 1).

6. Je! Paulo alisema kitu gani kiwe pamoja nao katika Bwana? (mst. 25).

7. Paulo aliandika waraka huu kwa kitu gani chake? (mst. 19).

8. Ni nani mwingine aliyemsalimia Filemoni? (mst. 24).

9. Je! Ni nani ambaye Paulo alisema kuwa ana faida kwa Filemoni? (mst. 11).

10. Onesmo alikuwa nani? (mst. 15, 16).

11. Paulo alikuwa nani katika Kristo? (mst. 9).

# Kuketi Juu ya Nguzo ya Ukuta

Ernest S. Underwood

Kusema machache, Habakuki alikuwa amekanganyikiwa kwa kile alichodhani kuwa ni kutojali kwa Mungu kuhusu matatizo ya wakati wake. Katika kilio chake alisema: ***"Ee Bwana, nilie hata lini, wewe usitake kusikia? Nakulilia kwa sababu ya udhalimu, ila hutaki kuokoa. Mbona wanionyesha uovu, na kunitazamisha ukaidi? Maana uharibifu na udhalimu u mbele yangu; kuna ugomvi, na mashindano yatokea. Kwa sababu hiyo sheria imelegea, wala hukumu haipatikani; kwa maana watu wabaya huwazunguka wenye haki; kwa sababu hiyo hukumu ikipatikana imepotoka"*** (Habakuki 1:2-4).

Badala ya kumkasirikia nabii huyu, Mungu alimpa maelezo ya kina kufafanua baadhi ya vitu ambavyo hakuwa anavijua. Kwa kweli, Bwana alimwambia ***"Angalieni, enyi mlio kati ya mataifa, katazameni, kastaajabuni sana; kwa maana mimi natenda tendo siku zenu, ambalo hamtaliamini hata mkiambiwa. Kwa maana, angalieni, nawaondokesha Wakaldayo, taifa lile kali, lenye haraka kupita kiasi; wapitao katikati ya dunia, ili wayamiliki makao yasiyo yao"*** (1:5-6).

Mungu aliendelea kumwonesha nabi huyu nguvu na utisho wa Wakaldayo. Nabii huyo kisha akaonekana kulalamika kuhusu hukumu hiyo kali, lakini mwishowe alisema, ***"Mimi nitasimama katika zamu yangu, nitajiweka juu ya mnara, nitaangalia ili nione atakaloniambia, na jinsi nitakavyojibu katika habari ya kulalamika kwangu"*** (2:1).

Kwa msisitizo naamini kwamba majaliwa ya Mungu yalihusika wakati wa kuanzisha taifa la Marekani. Ukuu wake unaweza kuhesabiwa kwa kukubali ukweli kwamba Mungu amelibariki taifa hili kwa baraka nyingi. Hata hivyo, kama ilivyokuwa kwa Habakuki, pindi mambo yanapokwenda mlama, tunaanza kufikiri kwamba Mungu ametusahau, na labda ametuacha. Pamoja na hayo, kama kweli tunamwamini Mungu, kuamini kwamba yeye ndiye msimamizi wa

ulimwengu, basi tutajaribu kuachana na "fikra mbadala" kumhusu yeye na utawala wake. Iwe yeye ndiye msimamizi, au nguvu za giza ndizo zinazosimamia, na ya kwamba Mungu hana nguvu ya kubadilisha hilo. Ni ndugu yupi au dada yupi ambaye anamwamini Mungu kweli ambaye ataegemea upande huo?

Kama ilivyo kwa Habakuki, tunauwezo wa kutambua uovu mkubwa katika ulimwengu na katika nchi, uovu ambao umeongezeka katika maisha  na matendo ya wale walio katika nguvu za kisiasa, na wale wanaofadhili nguvu za namna hiyo. Ni wazi kwamba wengi wa wale walio katika tasnia ya burudani, serikali, vyombo vya habari vingi na wengi katika baadhi ya watu wa kidini wanakanaji Neno la Mungu Mwenyezi. Inaonekana kwamba kila siku tunajifunza matendo ya kishenzi ya dini zisizofaa. Tumesukumwa na nguvu hizo katika mambo kama ya "ushoga" na kitu kingine kinachoitwa "ndoa ya jinsia moja." Watoto wetu ambao hawajazaliwa wanauawa kwa hidhini ya serikali, na msichana anaweza kununua vidonge vya kuzuia mimba bila wazazi kuhusika.

Kama roho zile zilizokuwa chini ya madhabahu, wale waliokuwa wamekatwa vichwa kwa sababu ya Kristo, wakati mwingine tunataka kulia, ***"Hata lini ee Bwana."*** Wengi huenda wana fikra za kisasi binafsi dhidi ya watendao maovu wa siku zetu za leo. Pamoja na hayo, Mungu bado anasema, ***"Kisasi ni juu yangu."*** Labda itakuwa bora kwa sisi sote kuwa na tabia ya Habakuki na kwenda "kuketi juu ya nguzo ya ukuta" na kutazama na kuona kile Mungu afanyacho. Licha ya yote, huenda anafanya kazi katika nyakati zetu ambapo itakuwa ngumu kwetu kuamini hata kama tutaona.

## SULUHU YA UTATA

Shadrack S. Msambaza

Nabii Habakuki alitatizika baada ya kumsikia Mungu kuwa ataliadhibu taifa lake kwa kutumia taifa ovu kuliko wao (1:12-13). Jibu la Mungu likawa ***"mwenye ataishi kwa imani yake"*** (2:4). Wokovu wetu unatokana na imani yetu katika neno la Mungu (Rum. 1:17; Gal. 3:11; Ebr. 10:38).

# *Maoni ya Haraka katika Aya Muhimu*

**(Ufunuo 6:9; 20:4-10)**

**Na alipoifungua muhuri ya tano, nikaona chini ya madhabahu roho zao waliochinjwa kwa ajili ya neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda waliokuwa nao.**

**Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu; nami nikaona roho zao waliokatwa vichwa kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu, na kwa ajili ya neno la Mungu, na hao wasiomsujudia yule mnyama, wala sanamu yake, wala hawakuipokea ile chapa katika vipaji vya nyuso zao, wala katika mikono yao; nao wakawa hai, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu. Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu. Huo ndio ufufuo wa kwanza.** [Angalia: ufufuo huu wa kwanza hauwezi kuwa ufufuo kutoka katika ubatizo, kama wengine wasemavyo, maana baadhi ya waliobatizwa watahukumiwa katika "mauti ya pili" kwa sababu ya kutokuamini kwao].

**Heri, na mtakatifu, ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu ya hao mauti ya pili haina nguvu; bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu.**

Inaonekana kana kwamba wale waliouawa kwa ajili ya Kristo katika Ufunuo 6 na 20 kwa sasa wanaishi na kutawala naye, wakati wa kipindi hiki ambapo Neno la Mungu limemfunga Shetani, ili asiwe huru kudanganya mataifa.

Kutajwa kwa "utawala wa miaka elfu" haraka sana inaingia kwenye akili za wengi fundisho potofu la "utawala wa Yesu miaka elfu katika dunia hii halisi" – Milenia. Hata hivyo, ukichunguza vizuri kifungu hicho kinaonesha kuwa utawala huo ni wa ulimwengu wa kiroho na sasa tayari upo. Imetajwa kuwa "wafu waliosalia" ambao hawataona ufufuo mpaka utawala wa Kristo utakapofikia mwisho. Utaisha lini? Kulingana na 1 Wakorintho 15, **Atatawala mpaka kifo kitakapokuwa kimeshindwa, na kisha ataukabidhi ufalme kwa Mungu.**

Pamoja na wale wanaotawala pamoja naye sasa, walio na sehemu katika "ufufuo wa kwanza," hukumu ya "mauti ya pili" katika moto haitawezekana kwao kwa sababu tayari walikwishapitia ufufuo na utukufu pamoja na Kristo.

Aya ya 7-10 zinafunua kwamba kwa namna fulani, Ibilisi atafunguliwa kwa muda mfupi na kwa mara nyingine atasababisha udanganyifu mkubwa. Uovu kwa mara nyingine utatapakaa, kama katika siku za Nuhu, kabla ya kurudi kwa Kristo pamoja na watakatifu wake wote ili kuhukumu ulimwengu.

# Fursa ya Kufundisha

Emanuel Daugherty

Kufundisha Biblia ni fursa nzuri sana, iwe unafundisha watoto au watu wazima. Ni njia ya Mungu ya kupanua mipaka ya ufalme. Kuna tofauti kati ya Ukristo wa kweli na dini nyingine katika heshima hiyo. Uislamu ulienezwa kwa upanga, Ukatoliki na Uprotestanti ulitawala mataifa mbalimbali kwa ulaghai na wakati mwingine mabavu. Lakini, upanga wa Mkristo ni Neno la Mungu (Waefeso 6:17). Maagizo kwa Kanisa ni ***“enendeni mkafundishe mataifa yote”*** (Mathayo 28:19). Yesu alisema ***“Wote watafundishwa na Mungu…”*** (Yohana 6:44-45). Nehemia alieleza lengo la kila Mwalimu ***“Nao wakasoma katika kitabu katika torati ya Mungu kwa sauti ya kusikilika wakaeleza maana yake hata wakayafahamu yaliyosomwa”*** (Nehemia 8:8)

Ni fursa kuwa mwalimu wa Biblia, kwa sababu si kila mtu anaweza kufanya hivyo kwa sababu nyingi, ikiwa ni pamoja na kukosa uvumilivu, ukosefu wa maarifa, mbinu, kutokuwa na uwezo wa kutekeleza kwa vitendo kile anachokihubiri na ukosefu wa shauku ya kufanya kazi. Miongoni mwa mambo hayo kwa kutaja machache, Yakobo 3:1 anasema ***“Ndugu zangu msiwe walimu wengi mkijua ya kuwa mtapata hukumu kubwa zaidi.”*** Walimu ni watu maalum wapende, waheshimu, simama pamoja nao na wasaidie kwa kutoa msaada kwa ajili ya kazi yao. Kufundisha ni fursa kwa sababu ya yule tunayemfanyia kazi. Mungu ndiye msimamizi wa Shule ya Biblia. Tunafundisha kile anachokitamani. Ni jambo jema ajabu kwamba Mungu mara nyingi anawatumia wanadamu kutimiza majukumu makubwa katika dunia. Kuwafundisha wengine kwa ajili ya wokovu wa roho zao ni fursa. Ni jambo zuri ajabu kuwa ***“watenda kazi pamoja na Mungu”*** (1 Wakorintho 3:9).

Ni fursa kuwa mwalimu kwa sababu ya kile tunachojitahidi kukitimiza. Ni lengo la mwalimu kumpatia Kristo mioyo, akili na roho za wanaume, wanawake, vijana wa kiume na wa kike. ***“Yesu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea”*** (Luka 19:10). Hili pia ndilo jukumu letu (2

Timotheo 2:2). Walimu hubadili jamii zetu na jinsi watu wanavyoishi. Mifano na mafunzo yao huonyeshwa katika darasa, katika nyumba zetu na katika jamii zetu na katika maisha ya watu. Mungu amependa iwe hivyo. Hivi ndivyo tunavyoweza kuonyesha nuru yetu ikiangaza na chumvi yetu ikiwashawishi wale waliotuzunguka (Mathayo 5:1316).

**Kila mwalimu anapaswa kukumbuka kwamba lengo kuu ni kuzileta roho za watu nyumbani mwa Mungu**. Chumba cha darasa ni mimbari yako. Matokeo ya mwisho ya juhudi yako ni wokovu. Maisha yaliyotumika katika kuwafundisha wengine darasani, mimbarini au nyumbani ni lazima yaishie katika kuongeza ufalme. Hatupaswi kuridhika kama walimu, mpaka tutakapoona wanafunzi wetu wanaishi katika amri ya kwanza na ya pili ***"Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote' na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote na mpende jirani yako kama nafsi yako"*** (Marko 12:29-31).

**Kufundisha ni fursa kwa sababu ya tuzo zake kubwa**. Miongoni mwa tuzo hizo ni amani ya ndani. Unapigana upande wa Bwana katika vita vikubwa kati ya vita vyote. Ni furaha ya pekee kujua kwamba umewaandaa wengine kupigana, kushughulikia majeraha yao na kuwasaidia kupata ushindi dhidi ya Ibilisi. Pia kuna ufahamu kwamba unafanya unachoweza kufanya ili kuifanya dunia iwe sehemu salama na kuleta amani, matumaini, usalama na utulivu kwenye dunia ambayo inajaribu kujiangamiza yenyewe. Halafu, kuna malipo yaliyo makuu zaidi kwa yule aliyemwaminifu, ***"Bwana wake akamwambia, vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya Bwana wako"*** (Mathayo 25:21). Walimu wa neno la Mungu, msihofu, jukumu lenu ni kuu duniani. ***"Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho"*** (Wagalatia 6:9). Endelea kusonga mbele. Kama G.P. Bowser, mhubiri maarufu, alivyosema kuhusu umuhimu wa wanafunzi wake, "Angeweza kuwa almasi katika hali isiyo nyololo, na usafishaji mdogo wa almasi".

***"Bwana wake akamwambia, vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya Bwana wako"***

# Pindi Marafiki Wanapokupa Kisogo

Cliff Hlmes

Nyakati za huzuni mara nyingi huja pale marafiki wanapotugeuzia migongo na kututelekeza. Yesu alikutana na jambo hilo na limewekwa kuwa kumbukumbu katika Yohana 6:67-68 ***"Basi Yesu akawaambia wale Thenashara, je! Ninyi nanyi mwataka kuondoka? Basi Simoni Petro akamjibu, Bwana! Twende kwa nani? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele"***

Furaha ilikuwepo katika kuwalisha watu mikate michache na samaki wawili. Pia furaha ilikuwepo katika tukio la Yesu kutembea juu ya maji. Pia furaha ilikuwepo pale Bwana wetu alipoleta utulivu kwa kuondoa hofu iliyoonyeshwa na wafuasi wake alipoingia katika mashua na kuwaleta salama ufukweni.

Baadaye tunamwona Yesu akiwafundisha watu kuhusu mkate halisi wa uzima ambao, Mungu amewapelekea wanadamu wote. Ingawa Wayahudi walinung'unika juu ya hilo, na hata wengi wa wanafunzi wake walirudi nyuma na hawakuandamana naye tena.

Fikiria kuhusu huzuni na maumivu ya Bwana wakati watu hao walipokuwa wakiondoka na kuacha zawadi ya Mungu ya bure. Alikuwa amefundisha vizuri sana, kwa bidii sana na kwa upole sana, lakini bado walimwacha. Unaweza kusikia maumivu ya moyo pale Yesu alipowauliza wale waliobaki, "***Je, ninyi nanyi mwataka kuondoka***?" Hapo hapo Simoni Petro akamjibu akisema ***"Bwana! Twende kwa nani? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele nasi tumesadiki, tena tumejua, ya kuwa wewe ndiwe mtakatifu wa Mungu***." Kila siku tunapaswa kufanya upya maamuzi yetu kwamba **hatutamwacha Yesu kwa sababu tunajua kwamba ana maneno ya uzima na Yeye ni Mkate wa uzima.**

# *Je! Umeacha Kitu Gani?*

Gary C. Hampton

Yesu aliacha kuwa sawa na Mungu akaja duniani na kuishi kama mwanadamu, akiishi kwa hiari kama mtumwa (Wafilipi 2:6-7). Paulo alilielezea jambo hili kwa maneno rahisi pale alipoandika,***"Maana mmejua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, jinsi alivyokuwa maskini kwa ajili yenu, ingawa alikuwa tajiri, ili kwamba ninyi mpate kuwa matajiri kwa umaskini wake"*** (2 Wakorintho 8:9).

Yesu aliacha Mbingu kwa ajili yangu, lakini nina hofu kuna nyakati nimeacha huduma kwa ajili ya Kristo ili kutimiza tamaa zangu za ubinafsi. Kulala badala ya kuhudhuria darasa la Biblia ungekuwa mfano mzuri wa kushindwa kufuata hali ya kutokuwa na ubinafsi ya Kristo. Mfano mwingine ungekuwa ni kushiriki katika mambo ninayopenda badala ya kupiga hodi katika milango ya watu ili kuwaalika kuhudhuria mikutano ya kiroho au mimi mwenyewe kushiriki katika mikutano hiyo.

Paulo aliona umuhimu wa kuacha mambo ambayo ni muhimu kwake ili kufuata ufufuo wa wafu (Wafilipi 3:8-11). Alikuwa tayari kuteseka hata kufikia hatua ya kutaka kuuawa ili aweze kukamilisha mbio zilizo muhimu sana (Matendo 20:22-24). Alitangaza***, "Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika Imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu"*** (Wagalatia 2:20).

Ninahitaji kuweka moyoni ombi la Paulo kwa Watakatifu waliokuwa kule Rumi ***"Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu"*** (Warumi 12:1-2).

Njia pekee ya kufuata nyayo za Mwokozi ni kuacha tamaa zetu ili kutafuta mapenzi ya Baba. Kila mmoja wetu anahitaji kujiuliza, **"Je, nimeacha nini ?"**

# MAHUBIRI CHANYA

Neal Pollard

Mungu anataka mahubiri chanya, si ndivyo? Kiukweli wahubiri wanapaswa kuthibitisha ukweli wa Injili. Wanapaswa kwa uwazi kabisa kuonyesha kile Mungu anachosema. Mahubiri yao hayapaswi kuwa ya kutia shaka au ya kubuni. Ni lazima yawe ya hakika na halisi yenye uthibitisho wa wazi na hakika na ujasiri kuhusu Biblia, utamthibitisha mhubiri kuwa ni mhubiri wa mahubiri chanya. Je, Mungu anapendezwa na kitu kingine chochote? Tafadhali niruhusu nikupe mambo matatu yanayoonyesha mahubiri ambayo si chanya.

**Mahubiri chanya si kuhubiri mambo yanayokwepa masuala fulani fulani!** Baadhi ya washirika wa kanisa wamekuwa watu wazima na wamezeeka bila kusikia masomo ya maadili kuhusu utofauti wa Wakristo katika mavazi, masuala ya mahusiano katika tendo la ndoa, kauli, mahusiano yasiyokubalika na mambo mengine kama hayo. Iwe ni suala la ushoga, kuvaa vibaya, kumsaidia mtu kufa, kushirikiana na madhehebu, wokovu katika imani pekee, uimbaji kwa kutumia vyombo vya muziki au tatizo la dhambi au kosa lingine lolote, mhubiri wa Mungu anapaswa kutaja na kuchukua msimamo wa kibiblia dhidi ya mambo hayo. Mtu anaweza kumpendeza mwenzake katika mahubiri ya kimaadili na ya kimafundisho ambayo hayaegemei upande wowote, lakini hawezi kupata kibali kutoka kwa Mungu. Kwa kweli jambo hili linapaswa kufanywa kwa uvumilivu (2 Timotheo 2:24-26) na upendo (Waefeso 4:15). Hata hivyo, asiwepo mhubiri yeyote mwenye kulionea aibu jambo lolote la siku hiyo.

**Mahubiri chanya si kuhubiri pasipo kutaja majina**. Katika kusanyiko lililojawa na hao walioukimbia uchafu wa dunia (2 Petro 2:20-22), mafundisho ya wanadamu (Mathayo 15:6-9), na makundi ya kidini ambayo Kristo hakuyafia (Waefeso 4:4), kuna hotuba na hoja za hotuba ambazo zimewekwa wazi (maana yake zilizo chanya) pale mtu

anapotoka katika hali ya dhahania kwa kutoa mifano halisi. Kuna wakati ambapo madhehebu yanahitajika kutajwa kwa majina, namna yoyote ya huduma maalum inayoendeshwa kimadhehebu inapaswa kukemewa au mtu yeyote anayetambulika kama mwalimu wa uongo (2 Petro 2:1). Jambo hilo hilo linapaswa kufanyika kama kuna makosa katika kanisa hususani kama ni tatizo linaloleta uharibifu katika kusanyiko husika. Kuna wakati ambapo majina, mawazo na matendo yanapaswa kushughulikiwa kwa wazi kabisa.

Je, kila wakati? Hapana! Je, kwa kuyatenga masomo yanayofariji? Hapana. Hata hivyo, mhubiri ambaye anaogopa kutaja jina katika hotuba atakuwa ni mwoga sana (Ufunuo 21:8). Akili za kawaida zitamsaidia mhubiri kujua pale hitaji lilipo la kutaja jina la mtu, kusanyiko au kundi la kidini.

**Mahubiri chanya si kuhubiri yale tu ambayo wasikilizaji wanataka kuyasikia.** Wajumbe wa Mungu wameonywa ***"Maana utakuja wakati ambapo watayakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia walimu makundi makundi kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo"*** (2 Timotheo 4:3-4). Kuna watu hawaridhiki na mahubiri mpaka pale watakaposikia mahubiri ***yatakayowafanya wajisikie vizuri***. Kuna baadhi ya makusanyiko ambayo hayawakaribishi wahubiri isipokuwa yule anayehubiri maneno yanayowapendeza. Manabii na makuhani wakati fulani waliwahakikishia watu kwamba kuna amani hata pale hasira ya haki ya Mungu ilipowaka dhidi ya njia zao za dhambi (Yeremia 8). Wale wanaomsikia mhubiri akitangaza kusudi lote la Mungu (Matendo 20:27), wanaweza wasijue kwamba kuna baadhi ya masomo ambayo ni magumu kwa mhubiri kuhubiri kuliko masomo mengine.

Kama kila mhubiri angeulizwa kwamba, kama angependelea kuhubiri kuhusu mbinguni au kuzimu, wengi wangechagua kuhubiri kuhusu mbinguni. Ni vigumu kusimama mbele ya kundi la watu na kudhihirisha ukweli ambao watu hawaupendi. Ni jambo linaloumiza kuhubiri kuhusu somo linalohusu hisia za watu ambazo zinaathiri

baadhi ya washirika katika kusanyiko. Panahitajika upendo na kujali ili kumwonya mtu aliyelala katika njia ya gari moshi kuliko kutabasamu na kumpungia mkono wakati hatari iko mbele yake. Yakupasa usiogope kamwe wala usichukie kusimama na kweli. Hata hivyo, mtu anayeogopa kukabiliana na Ibilisi na jeshi lake katika vita vya kiroho ni mtu asiyetegemewa na ni askari msaliti (Waefeso 6:10). Paulo alitoa mfano kwa Wakristo ambao pia unaweza kutumika kwa wahubiri,***"Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho"*** (Wagalatia 6:9).

> Wahubiri wa Bwana wana jukumu la kuhubiri ***"habari ya kusudi lote la Mungu"*** (Matendo 20:27), "tuishike kweli katika upendo" (Waefeso 4:15). ***"Tena ole wangu nisipoihubiri Injili"*** (1 Wakorintho 9:16).
>
> ***"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli"*** (2 Timotheo 2:15).
>
> ***"Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu"*** (1 Petro 3:15).
>
> ***"Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake; lihubiri neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho. Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo. Bali wewe, uwe na kiasi katika mambo yote, vumilia mabaya, fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiliza huduma yako"*** (2 Timotheo 4:1-5).

# UIMBAJI HUATHIRI UKUAJI WA KANISA

E. Cloude Gardner

Ndugu G.C. Brewer, mhubiri maarufu wa kizazi kilichopita aliinua uimbaji katika kanisa pale aliposema kwa sauti kuu "Tunaimba vizuri zaidi kuliko tunavyohubiri" jambo hilo linaweza lisiwe kweli leo. Ukweli ni kwamba uimbaji na mahubiri vyote vinapaswa kuboreshwa.

Tunaimba kama Kristo, ***"Katikati ya kanisa"*** (Waebrani 2:12). Uimbaji huchangia katika ukuaji wa kusanyiko. Uimbaji mwingine hauchochei ukuaji wala ubora wa ibada.

Kusudi la uimbaji kwa kifupi linaweza kuwekwa katika mambo mawili, ambayo ni **kusifu** na **kufundisha**. Vifungu viwili vya Maandiko vinavyoelezea mambo hayo ni, Waefeso 5:19 na Wakolosai 3:16. Viongozi wa nyimbo, wale wanaopanga utaratibu wa ibada na Wakristo wote wanapaswa kuzingatia mambo haya katika mioyo yao. ***"Mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu"*** (Waefeso 5:19). ***"Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu"*** (Wakolosai 3:16).

Ukifanya uchunguzi miongoni mwa nyimbo nyingi zinazoimbwa ni nyimbo za kumsifu na kumtukuza Mungu. Nyimbo zinazofundisha, zinazowapeleka watu kwenye utendaji huwa mara nyingi haziimbwi. Mtu akiambiwa aweke orodha ya nyimbo na azitofautishe na mafundisho, itakuwa changamoto na itashangaza.

Nyimbo za kusifu zinaweza kuimbwa kwa upendo na msisimko bila kuweka hitaji la kujitoa katika kufanya kazi ya Bwana. Kiukweli,

inafariji zaidi kuimba nyimbo hizi na kujiona "***kirahisi mko Sayuni***" kuliko kuimba nyimbo za mafundisho na kuwekea mkakati jambo mlilolipanga.

Ukuaji wa kanisa ni tatizo miongoni mwa ndugu. Baadhi ya sehemu na jamii zinapoteza waumini, huwa zinatolewa sababu fulani za kutokukua na baadhi ya sababu hizo zina uhalisia. Hata hivyo, hapa kuna tatitizo la kushindwa kuimba **nyimbo za zamani zenye mafundisho**. Tunakwepa lile jibu "Mimi hapa Bwana nitume mimi." Tukiimba nyimbo hizi tutatamani kuwa na shauku ya kuitenda kazi ya Bwana. Hatutachagua kuwa wanafiki wala hataimba uongo. Tukiimba nyimbo zinazotuita kuitenda kazi ya Bwana, tutajitahidi kumfundisha rafiki, kumkaribisha jirani katika ibada na kumrejesha aliyerudi nyuma. Jambo hili litasaidia ukuaji wa kanisa.

Vivyo hivyo, kukosa uwiano katika nyimbo kunakosababisha kuacha mafundisho kutasababisha kuacha vipengele vingine vya ibada. Sala, madarasa ya Biblia na hotuba yanaweza kuonekana kama matendo yasiyo na ulazima na ni hali ya uwajibikaji wa mtu binafsi tu. Hiki kinaweza kuwa kizuizi cha ukuaji wa kanisa.

Vitabu vya nyimbo vinaweza kushindwa kuzipa uhai nyimbo zinazochochea uwajibikaji katika kufanya kazi ya Bwana. Nyimbo nyingi za muhimu za zamani zimeondolewa, badala yake zimewekwa nyimbo za kisasa zinazopendwa na vijana. Ni nyimbo ngapi katika hizi zitakazosikika miaka 25 ijayo kama hazitaonekana ni nyimbo za zamani tena zinazochosha? Katika makundi ya vijana, nyimbo nyingi za kimaadili na kiroho hazifahamiki, na hawawezi kuziimba.

Nyimbo za sifa ni kwa ajili ya Bwana. Tunapofundisha na kuona matokeo tunampa Mungu shukrani na sifa. Nyimbo za sifa zina sehemu muhimu katika ibada. Tunasogezwa karibu na Mungu tunapoimba nyimbo hizi. Tunatoa shukrani na kicho kwa Mungu. Nyimbo za sifa zina nafasi muhimu katika ibada. Tunasogezwa karibu zaidi na Mungu kwa nyimbo hizi. Nilipokuwa mwanafunzi katika chuo cha kikristo cha Abilene, nilifurahishwa na Leonard Burford ambaye alikuwa kiongozi wa nyimbo na mwana-muziki. Katika ibada ya asubuhi, aliongoza

nyimbo nyingi za sifa alizoziingiza katika kitabu chake cha nyimbo. Ninayo nakala ya kitabu ambacho alisaini ili nipewe na mjane wake, Mary Delk Burford. Baadhi ya nyimbo hizo zinasema, "Msifuni Bwana" enyi mbingu, Mcheni yeye," "Bwana Mungu na Baba wa wanadamu" pamoja na kusifu nguvu zote za Jina la Yesu."

## Mambo ya Kuzingatia

1. Wakristo wote wanapaswa kuimba. Hakuna anayeimba zaidi kuliko wengine bali kila mtu "anamwimbia Bwana" kwa kadiri ya uwezo wake.
2. Tunapaswa kuimba nyimbo zote zilizotolewa [maadam ziwe sahihi], zinawasilisha ukweli wa Biblia. Tunatakiwa tuiimbe 'kweli' kama inavyohubiriwa.
3. Uwiano katika nyimbo zinazotumika utaleta faida kwa kusanyiko zima.
4. Tunapaswa kujua kile tunachokiimba. ***" Imekuwaje, basi? Nitaomba kwa roho, tena nitaomba kwa akili pia; nitaimba kwa roho, tena nitaimba kwa akili pia"*** (1 Wakorintho 14:15).

## Sarafu za Kenney

***"Amri yangu ndiyo hii, mpendane, kama nilivvyowapenda ninyi. Hakuna aliye na upendo kuliiko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake. Ninyi mmekuwa rafiki zangu, mkitenda niwaamruyo."*** (Yohana 15:12-14). Kwa kweli ni dhabihu ya mwisho iliyotolewa kwa ajili ya wanadamu. Kwa huzuni, kuna watu katika siku zetu ambao hawamheshimu. Kumpenda Yesu Kristo ni kumtii. Kumheshimu ni kumtambua yeye kuwa ni zaidi ya mtu mwadilifu, mwalimu mzuri au mmoja wa manabii kadhaa. Heshima ya kweli inamtambua Yesu kuwa alikuwa nani: Masihi, Kristo, Mpakwa mafuta na Mwana wa Mungu.

**David R. Kenney**

# Pale Uimbaji Wetu Katika Kusanyiko Unapokuwa na Makosa

Wes McAdams




Ninaamini kwamba uimbaji wa kusanyiko katika mkusanyiko wakati wa ibada ni suala la kibiblia, na ninaamini kwamba linafaida. Hata hivyo, ninaamini pia uimbaji wetu katika kusanyiko unaweza kuwa na makosa kama hatutakuwa makini. kama tunafikiri kwamba tuko sahihi kwa sababu tu tunaimba kila siku ya Jumapili basi tunapaswa kuchunguza tena kile ambacho Agano Jipya linakisema. Haya ni baadhi ya matukio yanayoonekana katika uimbaji wetu katika kusanyiko pindi unapokuwa na makosa.

Uimbaji wetu unakuwa na makosa pale mioyo yetu isiposhirikishwa. Wazo tunalolipata katika Agano Jipya ni kwamba muziki wa Mkristo unapaswa kutoka moyoni. Ukweli ni kwamba inaonekana wazi katika Waefeso 5:19 kuwa moyo ndicho chombo cha muziki ambacho kwa hicho Wakristo wanamfanyia Bwana muziki. Lakini pale midomo yetu inapohusika na uimbaji wakati mioyo yetu

haihusiki, ibada yetu inakuwa ya bure. Kwa maneno mengine ibada inakuwa haina maana.

Ninajua nimekuwa na hatia mara nyingi kuhusu uimbaji wa wimbo kutoka kwenye kumbukumbu na kutambua baadaye kwamba huwa sizingatii kile tunachoimba. Akili zangu na moyo wangu vinaelekezwa kwenye mambo mengine. Ninathubutuje kuja mbele ya kiti cha enzi cha Mungu na kuimba "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu" wakati ninafikiria jambo lingine? Tunapaswa kuwa na bidii na kwa hiari yetu kushirikisha mioyo yetu pale tunapomwimbia Mungu sifa. La sivyo, uimbaji wetu utakuwa hauna maana.

Uimbaji wetu unakuwa na makosa pale unapokuwa ni suala la kutimiza ratiba. Kwa bahati mbaya baadhi ya watu wamejenga tabia kwamba ibada ni suala la kutekeleza vipengele vya ibada. Mtu anasema, "niliyekwenda naye kanisani wiki hii." Tunaonekana tunasema "nilitoa kiasi fulani cha hela, nikasikiliza hotuba, nikashiriki meza ya Bwana nikainamisha kichwa wakati wa kusali na nikaimba nyimbo. Nilitimiza wajibu wangu." Ni huzuni kubwa sana kwetu kama tutaiendea ibada kwa mtazamo huo.

Ni kweli, hayo ni mambo tunayopaswa kuyafanya, lakini si jambo jema kabisa kuitazama ibada kama suala la kutimiza wajibu kuliko kuiona kama jambo la furaha na lenye baraka. Jambo hilo ni sawa na mimi kula chakula cha jioni nyumbani kwangu, halafu baadaye nikasema, "Sawa, nimefanya kile ninachopaswa kufanya. Nilihudhuria kwenye chakula cha jioni. Nikala chakula na familia yangu. Nilitimiza wajibu wangu." Sidhani kwamba mke na watoto wangu watapendezwa na kauli hiyo.


Muda wetu wa uimbaji wa pamoja unapaswa kuwa na uchambuzi wa wiki yetu. Ni wakati wetu wa kukusanyika pamoja kama familia na kumtangazia Baba yetu wa mbinguni ni kiasi gani tunampenda na jinsi tulivyopendezwa na pendo lake kwetu. Kauli inayosema "Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu" ni kweli katika maeneo mengi kuliko kuweka hela katika chombo cha

kukusanyia tu. Mungu hapendezwi pale tunapomtolea “katika hali ya kujisikia au kwa kulazimishwa”. (2 Wakorintho 9:7).

Uimbaji wetu unakuwa na makosa pale inapokuwa ni suala kuhusu muziki tu. Hili linaweza kuwa geni lakini mimi kwa uaminifu kabisa sifikiri kwamba uimbaji katika kusanyiko ni kuhusu sauti tu. Ukweli ni kwamba ukifikiri kwamba uimbaji ni kuwa na sauti tu zinazopendeza tutakuwa tumepoteza maana nzima ya uimbaji wa pamoja. Ninapenda maneno ya rafiki yangu mmoja aliyoyasema hivi karibuni, “Sauti ya muziki inapaswa kuhabarisha mioyo yetu kuhusu maana ya maneno. Kwa maneno mengine ni kwamba, tunaimba taratibu pale tunapoimba nyimbo zinazogusa moyo. Tunaimba kwa haraka pale tunapoimba nyimbo za furaha. Hata hivyo, pale ninapomsikia mtu akisema ‘nimechoka na nyimbo hizi zote za taratibu’ au ‘ninapenda nyimbo hizi za haraka’, huwa najiuliza kama mtu huyu anaelewa maana ya nyimbo.”

Mafundisho ya Agano Jipya juu ya uimbaji daima yanahusu maneno, na sio sauti au mirindimo. Uimbaji wenyewe unaweza ukatufanya tuwe na hisia na msisimko, lakini hilo si kusudi la uimbaji wa Mkristo. Kusudi mojawapo la uimbaji wa Mkristo ni kuonyesha hisia zake (Yakobo 5:13), wala si kuunda hisia. Makusudi mengine ya uimbaji ni kuonyesha shukrani na kufundishana sisi kwa sisi (Waefeso 5:19; Wakolosai 3:16). Hisia tunazozipata wakati tunapoimba ni malipo, lakini kamwe zisiwe ndilo kusudi.

Jambo la msingi ni kwamba, uimbaji katika kusanyiko unaweza kuwa wakati mzuri sana wa kujengana sisi kwa sisi pamoja na kumtukuza na kumsifu Mungu. Hata hivyo, tusipokuwa makini kuhusu jambo hili, tunaweza kuufanya uimbaji wetu kuwa ni tendo la ibada lisilo na maana isipokuwa kufurahia sauti zetu. Tuwe makini tuweke msisitizo pale msisitizo unapopaswa kuwekwa na ***“tumpe Mungu dhabihu ya sifa”*** *(*Waebrania 13:15).



# Je! Unapimaje?

Ee Mungu, unirehemu, Sawasawa na fadhili zako. Kiasi cha wingi wa rehema zako, Uyafute makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, Unitakase dhambi zangu. Maana nimejua mimi makosa yangu Na dhambi yangu i mbele yangu daima.

Nimekutenda dhambi Wewe peke yako, Na kufanya Maovu mbele za macho yako. Wewe ujulikane kuwa una haki unenapo, Na kuwa safi utoapo hukumu. Ee Mungu, uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu Usinitenge na uso wako, Wala roho yako mtakatifu usiniondolee. Unirudishie furaha ya wokovu wako; Unitegemeze kwa roho ya wepesi.

Nitawafundisha wakosaji njia zako, Na wenye dhambi watarejea kwako. Ee MUNGU, Mungu wa wokovu wangu, Uniponye na damu za watu, Na ulimi wangu utaiimba haki yako.

Zaburi 51:1-4, 10-13, 14

# MTU NA "COCOON"

Gene Clemons

Ifuatayo ni hadithi ya hali ya asili inayoonyesha ukweli kwamba mapambano ni sehemu muhimu ya ukuaji na maendeleo kwa Mkristo katika maisha haya. Mungu huweka mapambano haya au majaribu mbele yetu ili kutuandaa kwa ajili ya yale makazi yaliyo makamilifu kule mbinguni pamoja naye.



Siku moja tundu dogo lilitokea kwenye cocoon (kijumba cha mdudu kama buibui, nondo n.k. kinachotengenezwa kwa nyuzi). Mtu mmoja aliketi na kumwangalia kipepeo kwa saa kadhaa akipambana kulazimisha mwili wake kuingia

katika lile tundu dogo. Baada ya muda kipepeo akaacha kupambana. Inaonekana kipepeo alipambana kwa kadiri alivyoweza baada ya kushindwa akaacha. Yule mtu aliamua kumsaidia kipepeo, hivyo, alichukua mkasi, akanyata na kukata sehemu iliyobakia ya tundu. Ndipo yule kipepeo akaingia kirahisi, lakini alikuwa na mwili uliovimba na mabawa madogo yaliyosinyaa. Yule mtu akaendelea kumtazama yule kipepeo kwa sababu alitarajia kwamba, wakati wowote mabawa yake yangeongezeka na kutanuka ili kuweza kuusaidia mwili wake. Lakini hakuna lililotokea! Ukweli ni kwamba yule kipepeo alitumia muda wa maisha yake uliobaki akitambaa na mwili uliovimba na mbawa zilizosinyaa. Hakuweza kupaa kamwe. Kitu ambacho yule mtu katika wema wake na haraka yake hakuelewa ni kwamba ile cocoon na yale mapambano vilihitajika kwa kipepeo ili kuweza kuingia katika lile tundu, ilikuwa ni njia ya Mungu ya kulazimisha ute kutoka kwenye mwili wa kipepeo kwenda kwenye mbawa zake ili kumwezesha kupaa wakati atakapopata uhuru wake kutoka kwa cocoon. Kama Wakristo, mapambano (majaribu) ndiyo kile haswa tunachohitaji katika maisha yetu ili tukue na kuendelea vyema. Kama Mungu angeturuhusu kupita katika maisha yetu ya Kikristo bila vikwazo vyovyote ingetufanya kuwa walemavu kiroho. Kama ilivyokuwa kwa kipepeo, tusingekuwa na nguvu ambazo tungepaswa kuwa nazo. Tusingeweza kupaa kamwe.

# Hitimisho

Ndugu, tumshukuru Mungu kwa ajili ya mapambano (majaribu) ya kila siku na kuonyesha hali ileile ya kukabili majaribu kama mtume Petro alivyofanya. Mtume alisema katika 1 Petro 4:12-13, ***“Wapenzi, msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho lakini kama mnavyoyashiriki mateso ya Kristo, furahini ili na katika ufunuo wa utukufu wake mfurahi kwa shangwe”***

# Maisha ya Kila Siku ya Kikristo

# “NA MWE WAFADHILI NINYI KWA NINYI”

Raymond Elliott

Mtume Paulo baada ya kutoa maelekezo ya ***“kuvua ‘utu wa kale”*****,** yaani njia za zamani za maisha ya mtu yaliyopita na ***“kuvaa utu mpya ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli,”*** aliendelea kuorodhesha dhambi fulani ambazo hazipaswi kuwa sehemu ya maisha ya Mkristo (Waefeso 4:22-31). Paulo alihitimisha sehemu hii ya barua yake kwa ndugu wa Efeso kwa kuwapa nasaha hizi chanya, ***“Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi wenye huruma mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi”*** (Waefeso 4:32).

Ni neno ***“fadhili”*** ambalo ninatakiwa kusisitiza. Hiki ni kivumishi kinachoelezea moyo na matendo ya Mkristo aliyejitoa. Paulo alieleza kwamba **“*upendo hufadhili*”** (1 Wakorintho 13:4). Katika 2 Petro 1:7, tunahimizwa katika ukuaji wetu wa kikristo kuongeza imani, wema, maarifa, kiasi, saburi, utauwa na ***“katika utauwa upendano wa ndugu,na katika upendano wa ndugu upendo”.*** Katika Wagalatia 5:22



tunasoma kwamba ***"fadhili"*** ni miongoni mwa ***"tunda la roho"*.** Mtume Paulo katika Wakolosai 3:12 alielekeza kwa kusema, ***"Basi kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao jivikeni moyo wa rehema utu wema unyenyekevu upole, uvumilivu."***

Albert Barnes katika kitabu chake cha *"Barnes Notes on the Bible,"* alilizungumzia neon **"ufadhili"** kama linavyopatikana katika Waefeso 4:32: *"Hakuna dini katika hali ya uchungu, hasira ya kuchukia watu; katika hali ya kiburi, ugumu wa moyo, na hali ya kurudisha nyuma; wala katika uasi wa sheria za uzao mzuri. Kwa kweli kuna upole katika moyo ulio wazi, ambao Mkristo hapaswi kuukusudia wala kuuiga. Upole wake unapaswa kusimama kwenye* ***"ufadhili";*** *adabu yake iwe ni matokeo ya upendo, mapenzi mema, na shauku kwa ajili ya furaha ya wengine wote; na hii itahamasisha aina ya hali ambayo itapelekea mazungumzo yake na wengine yawe ya kukubalika na yenye faida."*

Moja ya sababu zilizo muhimu sana kwa nini tufadhiliane sisi kwa sisi zinapatikana katika Neno lenyewe. Yesu alisema, **"*Bali ninyi msiitwe Rabi, maana mwalimu wenu ni mmoja, nanyi nyote ni ndugu*."** (Mathayo 23:8). Anasema kwamba, hatupaswi kujiinua, ndugu mmoja kwa mwigine, maana sisi sote ni ndugu, wake na waume kwa kiwango kile kile. Ni namna gani tulifanyika kuwa 'wanaukoo', tukizungumzia hali ya kiroho?

Jibu linapatikana katika Wagalatia 3:26-29, fungu ambalo linasomeka, ***"Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmevaa Kristo. Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mtu mmoja katika Kristo Yesu. Na kama ni wa Kristo, basi mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi."***

Kuwa "mwanafamilia" kwa kila mmoja pia tutakuwa na mioyo safi na wasamehevu. Sisi ni ndugu waume na wakike katika Kristo Yesu. Sisi ni familia ya Mungu (Waefeso 3:14-15).

# IMANI, TUMAINI NA UPENDO; MANENO MATATU YENYE NGUVU DUNIANI

J. Randal Matheny

**Kamba ya nyuzi tatu si rahisi kukatika** (Muhubiri 4:12). Hakuna nguvu za kidunia zinazoweza kushinda dhidi ya maneno hayo matatu hapo juu. Kwa kutumia hayo, Neno la Bwana litaendelea kukua na kushinda (Matendo 19:20). Yeyote aliye na maneno hayo atahesabika kama aliyebarikiwa na atasimama kinyume na maadui wote na hali ya kukatishwa tamaa.

Sisi tulio katika nuru tunapaswa kuyavaa maneno hayo tunapoutazamia ujio wa Bwana (1 Wathesalonike4:13-5:11). Maneno hayo yanatuhakikishia ushindi, ***"Lakini sisi tulio wa mchana, tuwe na kiasi, hali tukijivika kifuani imani na upendo na chapeo yetu iwe tumaini la wokovu"*** (1 Wathesalonike 5:8).

## Imani, Tumaini, Upendo

Katika siku za giza maneno hayo yanatufanya tustahimili, yanaweka uaminifu, ahadi na upendo wa Mungu katikati ya maono yetu. Tunayahitaji sasa zaidi kuliko wakati mwingine wowote. Changamoto zilizo mbele ya familia ya Mungu zinaonekana kuongezeka tu kadiri muda na nyakati zinavyosonga mbele. Wengi wanaacha imani kwa sababu ya dini zilizo maarufu. Wengine wanakumbatia uchungu na kinyongo. Wengine wamegeukia miradi ya kidunia wakiacha kuangalia tumaini la wokovu wa milele.

Watakatifu wanapaswa kujizamisha katika imani, tumaini na upendo. Si wakati wa kutia hofu. Si wakati wa kusalim amri. Majira

yanatutaka tuwe na ujasiri katika utamu wa Habari njema za Yesu Kristo.

Miaka 10 tu iliyopita, katika swala la ***Upanga wa Kiroho*** ambao maudhui yake yalikuwa "***Endelea",*** mwandishi Alan Highers alihitimisha uandishi hivi "Tumehangaishwa, tumetiwa wasiwasi na tumepata hofu kuondoka na kuasi kwa watu dhaifu na wakaidi. Ni lazima tuendelee kupinga makosa na ukengeufu kutoka kwenye imani lakini si kwa gharama ya kupoteza maono yetu na akili zetu za kazi tulizonazo kwa ulimwengu ***"Enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe"*** (Marko 16:15), (Highers 2007,2).

Katika makala iliyotangulia ya suala hilohilo, Phil Sanders aliwakumbusha wasomaji, *"Katika kila utamaduni, kitu ambacho watu wanakihitaji zaidi ni Injili. Watu bado wanahitaji ili wapate kuishi kwayo, tumaini ili kuishi kwalo na upendo ili kuishi katika huo"* (Sanders 2007, 3).

Mtume Paulo mara nyingi alipenda kuunganisha imani, tumaini na upendo. Aliyaona maneno haya matatu kama chemchemi ambazo katika hizo watakatifu wanaweza kuchota uzima na mafanikio.

Imani huamini kwamba Mungu anaweza na atatenda. Tumaini humtegemea Mungu kuleta haki, wokovu na tunda la haki. Upendo hujenga madaraja ya ushirika ambayo huunganisha mipaka ya vitu vya juu na duniani. Kwa maneno haya matatu tuliumbwa.

Katika haya tunapata utoshelevu. Tukiwa na haya hatuwezi kushindwa.

Katika siku ya mwisho imani itaonekana, tumaini litapokea shauku yake na upendo utabaki katika ufalme wa milele na wema wa kimungu. Mpaka hapo, hebu tukumbatie maneno haya matatu yatakayodumu hadi mwisho na kutuacha na upendo wa Mungu wa kudumu.

> ***"Lakini sisi tulio wa mchana, tuwe na kiasi, hali tukijivika kifuani imani na upendo na chapeo yetu iwe tumaini la wokovu"***

# Masuala ya Kifamilia

Derek Broome

Kuna maamuzi mengi ya kufanya na mambo mengi ya kuzingatia pale linapokuja suala la familia. Ebu tuchukue muda kidogo tuangalie Biblia inatufundisha nini kuhusu familia.

**Tunapaswa kuanza na watu wawili tofauti kabisa:** Mwanaume na mwanamke. Hawa ni watu wawili, roho mbili na wenye historia mbili tofauti za maisha. Wana dhambi, wana changamoto na wanamwitaji Mwokozi kama wanadamu wengine wote (Warumi 3:23). Je, watatii neno la Mungu (Matendo 2:38)? Je, watakuwa waaminifu kwake daima (Ufunuo 2:10)?

**Sasa tunawaona wanandoa:** Wale waliokuwa wawili wamekuwa mmoja (Mwanzo 2:24). Waume wanapaswa kuwapenda wake zao kama Kristo alivyolipenda kanisa (Waefeso 5:25). Wake wanapaswa kuwatii waume zao kama kanisa limtiivyo Bwana (Waefeso 5:22). Mume anapaswa kuwa kichwa cha familia kama vile Kristo alivyo kichwa cha kanisa (Waefeso 5:23). Je, watakuwa waaminifu kila mmoja kwa mwingine (Waebrania 13:4)? Je wataachana na kupeana talaka (Mathayo 19:9)? Je, watapendana na kuheshimiana?

**Wanandoa wanaamua kupata watoto:** Familia inapaswa kuhudumiwa na kupewa mahitaji yanayofaa (1 Timotheo 5:8). Bado baba ni kichwa cha familia na anapaswa kuwafundisha watoto ili wawe na nidhamu na kuwapa maelekezo ya Bwana (Waefeso 6:4). Wazazi wote wanapaswa kuwatunza na kuwalea watoto wao katika njia sahihi (Mithali 22:6). Nidhamu inapaswa kutumika nyumbani kwa sababu watoto wanapendwa na ni muhimu kwa ajili ya malezi yao (Mithali 13:4). Je, wazazi watawatunza, watawalea na kuwaadibisha watoto kama Bwana anavyotaka?

**Sasa, tuna watoto:** Watoto wanapaswa kuwatii na kuwaheshimu wazazi wao (Waefeso 6:1-2). Wanapaswa kuchukua mafunzo waliyoyapata na kuwa mfano kwa waaminio (1 Timotheo 4:12). Watoto, kama ilivyo kwa wazazi wao au mtu mwingine yeyote, wanaweza kuanguka katika dhambi (Warumi 3:23). Mwishowe itakuwa ni maamuzi yao wenyewe wanayofanya kama watu wengine ikiwa wataamua kufuata Neno la Bwana au la. Je, watachagua nini?

Neno la Mungu liko wazi kabisa pale linapozungumza kuhusu familia. Daima Mungu amekuwa na mpango kwa ajili ya familia. Biblia hutuonyesha kwamba familia ni muhimu kwa sababu nyingi: Imani, upendo, mafunzo n.k. Biblia hutufundisha kwamba ni juu ya kila mmoja wetu kuchagua kumfuata Mungu na kutekeleza majukumu yake katika familia. Uhalisia na ukweli ni kwamba kuna familia moja tu kamilifu na hiyo ni familia ya Mungu. Tunavyoishi poishi na kufanya kazi katika familia zetu nyumbani na kanisani, tutakuwa na uchaguzi. Hata watu wanaotuzunguka wanapochagua njia za kidunia, sisi daima tuchague njia ya Mungu. Mungu atusaidie daima tuishi kama watoto wake.

# FAMILIA NA UONGOZI

Shadrack S. Msambaza

Wakati fulani tunaweza tusione umuhimu wa familia. Lakini unapojifunza Biblia vizuri unaweza kufumbuliwa macho kuhusu umuhimu wa familia katika nyanja mbalimbali katika maisha.

Katika uongozi wa kanisa Mungu alisema, ***"Basi imempasa askofu awe…mume wa mke mmoja…mwenye kuisimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu"*** (1 Timotheo 3:2,4). Hii ina maanisha kwamba, kama hakuna familia, basi hakuna uongozi wa kanisa. Pamoja na hayo, kuwa na familia pekee hakumfanyi mtu kuwa kiongozi wa kanisa, ***"mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje kanisa la Mungu?"*** (1 Timotheo 3:5). Kiongozi mzuri ni yule anayeitunza familia yake kimwili na kiroho.

# NDOA KWA UTARATIBU WA MUNGU

Denny Petrillo

Ni ukweli kwamba ndoa nyingi ziko katika matatizo leo hii. Pia ni ukweli kwamba watu wa Bwana hawana kinga juu ya aina hii ya matatizo. Vyanzo vya matatizo haya ni vingi. Wanandoa wanabishana juu ya fedha, watoto, wazazi, muda wa kuwa pamoja, muda wa kutokua pamoja, vipaumbele, tendo la ndoa na mengine mengi.

Mungu alimvuvia Sulemani aweze kutoa ushauri mzuri kuhusu ndoa.Alisema, ***"Uishi kwa furaha pamoja na mke umpendaye, siku zote za maisha yako ya ubatili, ulizopewa chini ya jua; siku zote za ubatili wako kwa maana huo ni sehemu yako ya Maisha na katika taabu zako ulizozitaabika chini ya jua"*** (Mhubiri 9:9). Mstari huu unaonekana kutupa mambo kadhaa yatakayotusaidia kuwa na ndoa yenye mafanikio. Angalia mambo hayo:

**Kwanza,** mstari unaonyesha kwamba ndoa yenye mafanikio inahitaji mahaba. Tunapoendelea kuishi katika dunia ambayo inaamini katika upendo wa bure na usio na vizuizi katika tendo la ndoa, mara nyingi ndoa zinakosa ule ukaribu ambao Mungu anataka tuwe nao. Paulo alizungumzia jambo hili katika 1 Wakorintho 7:35.

**Pili,** mstari unaonyesha kwamba ndoa zenye mafanikio zinahitaji kuitafuta furaha. Watu wanahitaji kuweka mkazo zaidi katika kuhakikisha kwamba wenzi wao wanapata furaha kuliko kulalamika kwamba hawapati furaha kutoka kwa wenzi wao. Yesu alimaanisha nini aliposema, ***"Ni heri kutoa kuliko kupokea"*** (Matendo 20:35)? Inawezekana kwamba mtoaji ana furaha zaidi kuliko mpokeaji?

**Tatu,** mstari unaonyesha kwamba ndoa yenye mafanikio inahitaji kujitoa siku zote (siku zote za maisha yako ya ubatili). Tunaishi katika jamii ambayo inayakimbia matatizo yake badala ya kupambana nayo. Yesu alifundisha kwamba alichokiunganisha Mungu hakipaswi kutenganishwa (Mathayo 19:3-6). Ndoa zenye mafanikio zinahitaji watu wawili ambao wako tayari kuwa wagumu katika nyakati ngumu.

Wote tunaweza kuwa na ndoa zenye mafanikio pale tututakapokuwa tayari kukubaliana na matatizo na kutekeleza maelekezo yaliyovuviwa! "Ndoa kwa utaratibu wa Mungu" itampendeza Mungu na itawapendeza wanandoa pia.

# HAWAUZWI

Ken Tyler

Wanandoa waliovalia vizuri na kupendeza wakiwa na watoto wao wawili walienda katika duka la kuuza midoli. “Tunataka midoli ambayo itawaburudisha watoto wetu,” alisema mama. “Mimi na mume wangu wote tunafanya kazi na watoto mara nyingi wana wa peke.” Msichana aliyekuwa anauza dukani aliwaonyesha midoli mbalimbali na vifaa vya michezo lakini wazazi hawakuvipenda. “Mimi ninavyoona,” alizungumza mama kwa sauti ya upole “kwamba ungejua tunachokitafuta hasa ungeweza kuitafuta katika midoli hii.” Yule msichana muuzaji akasema, **“Samahani mama, lakini naamini kwamba kile unachokitafuta hasa-ambacho watoto wenu wanachokitaka ni baba na mama, na hao hatuwauzi hapa.”**

Hadithi hii fupi ya kushangaza inaelezea mgogoro ulioko katika jamii zetu. Akina baba na akina mama hawapatikani nyumbani ili wawalee watoto wao. Mambo ya dunia katika jamii zetu kupitia simu, compyuta na televisheni ndivyo vinavyowaburudisha watoto wetu na matokeo yake ni uharibifu kwa watoto wetu. Wazazi wana shughuli za kutafuta pesa kiasi kwamba wamesahau kuhusu kujenga tabia za watoto wao. Ni lazima jambo lifanyike hapa. Mitazamo na mikazo yetu lazima ibadilike. Biblia inasema ***“Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha hata atakapokuwa mzee”*** (Mithali 22:6*).* ***“ Nanyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana”*** ( Waefeso 6:4).

**Nawahamasisha akina baba na akina mama kufanya mafunzo ya kiroho kwa watoto wenu kuwa kipaumbele cha juu kabisa.** Miaka ijayo ndiyo itakayokuja kudhihirisha kwamba mlifanya uamuzi wa busara au la!

# WAFANYE WATOTO WAENDE KANISANI

Mwandishi Hajulikani

Jumapili moja asubuhi mama mmoja alienda kugonga hodi kwenye chumba cha kijana, mwanawe, ili aamke aende kanisani. Alipogonga mlango wa kijana wake, kijana alisema, "Siendi,""kwa nini huendi?" kijana alijibu "nitakupa sababu mbili nzuri, moja, hawanipendi mimi. Mbili, siwapendi." Mama yake akamjibu, "nitakupa sababu mbili nzuri kwa nini unapaswa kwenda kanisani. Moja, wewe una umri wa miaka 47. Mbili, wewe ni mhubiri."

Utani huu ulichekesha, lakini ukweli ni kwamba unapokwenda kumwamsha mtoto wako au kuwaamsha watoto ili wajiandae kwenda kwenye ibada halafu wakikwambia hawataki kwenda kanisani utasema nini au utafanya nini? Je, utawaacha wakose darasa la Biblia na ibada? Utawasisitiza waende kanisani ama wanataka au hawataki? Ni nani mzazina ni nani mtoto hapa?

Je, huwa unawahimiza watoto wako waende kwenye huduma za kanisa? Je, unawahimiza watoto wako waende shuleni? Ni lipi lililo muhimu zaidi- ibada au shule? Je, kazi za shule zitawasaidia watoto wako kwenda mbinguni? Je, kujifunza Neno la Mungu kutawaelekeza njia ya kwenda Mbinguni? Haya ni maswali muhimu ambayo sisi sote tunapaswa kuyajibu kwa ajili yetu wenyewe na kwa ajili ya watoto wetu.

# Hata Hivyo si Suala la Wokovu

Demar Elam

Mara nyingi, utamsikia mtu akisema, "Ah, si unajua hata hivyo si suala la wokovu." Sasa jambo hili huwa linazungumzwa kuhusu vitu ambavyo havihusiani na wokovu lakini vinaangukia eneo la vitu vyenye manufaa au maoni. Hata hivyo, baadhi ya watu hutumia kauli kama hiyo katika kila kitu ambacho Mungu ameamuru. Wengi husema "Ah, si unajua kitu kizuri kuhusu mambo kama hayo ni kwamba si suala la wokovu."

Kwa hiyo, tunachangamoto kuhusu wazo la mambo ya wokovu dhidi ya mambo yasiyo ya wokovu. Inahitajika kufahamika kwamba kuna mambo mengi yametajwa katika Biblia ambapo inaeleweka kwamba wokovu wa mtu unahusika juu ya mambo yaliyotajwa. Mara nyingi katika eneo la jambo lenye manufaa, huwa kuna njia nyingi za kufanya kitu, na tunahitaji kuwapa watu uhuru wa kufanya kile wanachopenda, ikiwa wanapenda kufanya kitu hicho. Lakini, baadhi ya watu wanatumia kauli hii, "Ah, hata hivyo si suala la wokovu" ikiwa ni nje ya mipaka yake na kuitumia katika kila amri kwenye Neno la Mungu. Hii itasababisha watu wapotee kwa kushindwa kufanya kile ambacho Mungu anataka wafanye. Yesu alisema, "***Mkinipenda mtazishika amri zangu***" (Yohana 14:15).

Tunapofasili Maandiko vizuri yaani kuchambua neno au kifungu cha Neno la Mungu tunahitaji kutambua kwamba kuna maeneo ya jambo lenye manufaa na maeneo mahususi. Kuna baadhi ya mambo ambayo ni mahususi na ni lazima yafanyike sawasawa kabisa na Mungu alivyoamuru. Halafu, kuna mambo ambayo ni ya jumla na

yanaweza kufanywa kwa njia mbalimbali tofauti. Tunapaswa kuwa na uhuru wa kufanya mambo pale njia ya kufanya amri hiyo inapokuwa njia ya jumla. Katika maeneo haya ya jambo linalofaa upendo wa Mkristo unahitajika sana. Yesu alifundisha kwamba ulimwengu unatakiwa kujua kwamba sisi ni wanafunzi wake kwa upendo mkuu tunaoonyeshana sisi kwa sisi (Yohana 13:34-35).

Ngoja nitumie mfano niliojifunza kutoka kwa mpendwa askari wa msalaba ambaye ni marehemu kwa sasa, Gus Nichols. Katika Marko 16:15-16 tunasoma, "***Akawaambia, 'enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe aaminiye na kubatizwa ataokoka asiyeamini atahukumiwa***.'" Tafadhali angalia neno "***Enendeni***" katika andiko hili ni neno mahususi. Wanafunzi wa Kristo, ili wawe watii kwa Kristo ni lazima "***waende."*** Neno "***Enendeni"*** katika mstari huu sio ombi au hiari. Wafuasi wa Kristo wanapaswa kwenda wapi? Wameamriwa kwenda "***ulimwenguni mwote***" (dunia nzima), hilo pia ni jambo mahususi na si jambo la jumla au hiari. Wanapaswa kufanya nini wanapokwenda? Je, kuna jambo mahususi wanalopaswa kufanya? Ndiyo, wanapaswa kuhubiri injili kwa kila kiumbe na kuwabatiza hao wanaoamini.

Tazama katika andiko hili haitajwi **njia**, kwa nini? Kwa sababu Mungu ameacha **namna** ya kwenda iwe juu ya hao wanaokwenda. Kwa hiyo, hili ni suala la jumla kwa asili yake. Leo, tunaweza kutembea kwa miguu, tunaweza kuendesha magari, tunaweza kupanda ndege, tunaweza kutumia meli, au kutumia njia nyingine za usafiri. Kama andiko lingesomeka hivi, *"enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri Injili kwa kila kiumbe kwa kutumia farasi,"* hapo jambo hilo lingekuwa ni mahususi na lingemaanisha kwamba njia pekee ya kutii amri hiyo ni kila tunapokwenda kuhubiri injili lazima tusafiri kwa kupanda farasi. Lakini, Biblia ni kitabu kitakatifu na hakuna makosa kama hayo yanayopatikana ndani yake. Isingewezekana kwenda ulimwenguni mwote kwa kutumia farasi, kwa sababu huwezi kuvuka bahari kwa kutumia farasi.

Kumbuka hili: Daima, ni lazima kuwe na amri juu ya jambo kabla ya kuangalia njia ya kimaandiko ya kulifanya jambo hilo. Jambo hilo halipaswi kufanyika na hakuna njia ya kimaandiko ya kufanya jambo hilo. Kama hakuna amri ya kufanya jambo hilo, basi lisifanyike kwa amri. Kwanza, tafuta mambo mahususi ya kufanya, kisha tafuta mambo ya jumla yatakayokuwezesha kutekeleza amri uliyopewa.

Wakristo wanapaswa kuliendea jambo hili kwa kuzingatia hali inayosema kuwa kama kuna uwezekano mdogo kwamba Mungu anataka nifanye jambo fulani, na nitalifanya kwa njia ile Mungu aliyotaka nilifanye. Hata hivyo, ikiwa Mungu hajazungumza au kuamuru jambo fulani kufanyika, nahitaji kuepuka kuongeza katika Neno lake (Kumbukumbu 4:2; Mithali 30:6; Ufunuo 22:18-19). Ukweli ni kwamba kauli, "Ah, hata hivyo si suala la wokovu" mara nyingi ni jambo linaloitwa "kughairi au kukwepa". Kauli hii inatumiwa na baadhi ya watu leo kukwepa kufanya kile anachokitaka Mungu.

"Masuala ya wokovu" ndiyo Neno la Mungu lipo kwayo. Tunahitaji kutazama kila kipengele cha Neno la Mungu kama kina umuhimu mkubwa na wa milele ndani yake. Kiini cha Maandiko ni kushughulika na mambo ya wokovu. Wakati inatakiwa itambulike kuwa kila kitu kinachopatikana ndani ya Biblia hakina matokeo ya milele yaliyoungamanishwa na utekelezaji wake, ieleweke kwamba mambo yote katika Biblia ni muhimu. Mtu atafanya kosa kubwa na labda la milele kwa kusema, "Ah, hata hivyo si suala la wokovu" wakati kiukweli jambo hilo linaumuhimu wa milele, na zaidi sana lina matokeo ya milele.

Mtu anaweza kujifanya ajisikie vizuri kwa kusema, "Ubatizo ni muhimu lakini Ah, hata hivyo si suala la wokovu." Kwa kusema tu ubatizo "si suala la wokovu" haifanyi ubatizo usiwe suala la wokovu. Ndivyo ilivyo kwa amri nyingi za Mungu katika Biblia nzima. Baadhi ya watu huwa na mawazo kwamba wakisema "Ah, hata hivyo si suala la wokovu" kwamba wamefanya jambo hilo lisiwe la wokovu kwa matamshi ya kauli hiyo. Ukweli ni kwamba kauli hizo hazibadilishi amri yoyote ya Mungu kwa namna yoyote ile. Biblia inafundisha wazi

kwamba ubatizo ni kwa ajili ya msamaha wa dhambi (Matendo 2:38; 1Petro 3:21; Marko 16:15-16).

Mtu anaweza kujifanya ajisikie vizuri kwa kusema kwamba ubatizo si suala lenye umuhimu wa milele na kwamba mtu anaweza kwenda mbinguni bila kubatizwa. Lakini, hiyo haimaanishi kwamba mafundisho ya Mungu kuhusu ubatizo yatabadilika kwa sababu mtu huyo anafikiri hivyo. Baadhi ya watu husema, "Kuna makanisa mengi na njia nyingi za kwenda Mbinguni na kwamba "hata hivyo si suala la wokovu." Lakini, hiyo haibadili ukweli kwamba Roho Mtakatifu aliwavuvia watu wa Mungu kuandika kwamba Kanisa ni mwili wa Kristo, na Kristo ni kichwa cha huo mwili (Waefeso 1:22-23; Wakolosai 1:18, na kwamba kuna mwili mmoja tu (Waefeso 4:4). Paulo aliwaelekeza Waefeso kwa maneno haya:

> ***"Lakini kama vile kanisa limtiivyo Kristo, vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo, Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa"*** (Waefeso 5:24-27)

Waliokombolewa wanaongezwa na Kristo katika mwili huo yaani kanisa, baada ya utii wa mapenzi yake, (Matendo 2:47). Ni hao tu ambao wameongezwa na Kristo mwenyewe katika mwili huo watakao okoka. Ukweli huu mkuu na mambo mengine yenye umuhimu wa milele, hayawezi kuondolewa au kupunguzwa yakawa si chochote kwa maelezo ya mtu kujisikia vizuri kama,"Hata hivyo si suala la wokovu."

Baadhi ya watu wanatoa hoja:

> Kwani kuna shida gani kulewa mara moja moja? Hata hivyo, hili si suala lenye umuhimu hivyo. Kuna shida gani

kufanya tendo la ndoa kidogo nje ya ndoa? Unajua si suala linalohusu wokovu. Kuna shida gani wanaume wawili wakiishi pamoja katika ushoga au wanawake wawili wakiishi pamoja kama wasagaji? Hayo, ni mambo yao, si ndivyo? Mbali na hivyo, hilo si suala la wokovu. Kuabudu kwa namna yoyote anayotamani mtu ni sawa tu mbele za Mungu, lakini, hata kama si sawa, mtu hapaswi kuwa na wasiwasi kwa sababu hata hivyo, hilo si suala la wokovu. Ukweli ni kwamba Mungu anapokea mfumo wowote wa ibada ikiwa mtu anamaanisha hasa. Hata hivyo, ibada haina umuhimu wa milele. Wokovu wa mtu usiingilie jambo la mtu mwingine.

Ijapokuwa watu wanaleta hoja kama hizo tulizozitaja hapo juu hawatabadili kile alichokisema Mungu na kuamuru katika maneno yake matakatifu, yaani Biblia. Watu watakaposimama mbele ya Kristo siku ya hukumu, ndipo watakapotambua kuwa kusema kwamba, "Hata hivyo si suala la wokovu" hakukubadilisha amri za Mungu kwa namna yoyote.

## HIVI NI KWELI JINA HALIJALISHI?

Shadrack S. Msambaza

Watu wa madhehebu mbalimbali wanasema kuwa "haijalishi ni jina gani utaliita kanisa au huduma yako ilimladi unafundisha ukweli." Je, ni sahihi kuliita kanisa la Mungu kwa jina lolote? Ikiwa utamuuliza mtu huyo kuwa, je, tunaweza kuandika jina lolote katika mali yako? Bila shaka atasema, **hapana**. Atakataa kwa sababu kwa kufanya hivyo kutaondoa haki yake ya umiliki, maana jina ni ishara ya umiliki. Maandiko yanasema kanisa ni mali ya Mungu (Mathayo 16:18; Matendo 20:28; Waebrania 3:6; 1 Timotheo 3:15). Paulo aliwakemea Wakoritho kwa sababu ya kujiita kwa majina ya watu (1 Wakorintho 1:11-13). Kisha akafikisha salamu, ***"Makanisa yote ya Kristo yawasalimu."*** (Warumi 16:16).

# Sayansi ya Kawaida ya Kutafsiri Maandiko

Cecil May, Jr

Amri mahususi inatoa mamlaka katika ukimya juu ya mambo yanayofanana, inakataza. Amri ya kiutume ni kuimba; ukimya kuhusu aina nyingine za muziki haziruhusiwi.

Huo ni utaratibu wa kawaida wa sayansi ya kutafsiri maneno tuliyojifunza kama watoto. Mama anaposema, “Nenda kacheze uani” neno “uani” lilikuwa mahususi. Lilimwamrisha mtoto aende kucheza katika eneo maalum analolifahamu. Tulijifunza kwa haraka kwamba ukimya wake kuhusu maeneo mengine ulikataza kwenda kucheza mitaani, ndani ya nyumba ya mtu aliye jirani, kwa mfano. Kwa nini tunaelewa mambo hayo kirahisi lakini hatufanyi vivyo hivyo katika Neno la Mungu?

**Jinsi Mungu Anavyoidhinisha!**

Jerry Bates

Wengi hushindwa kuelewa jinsi tunavyopata mamlaka kwa ajili ya matendo yetu, hususani ibada yetu. Kuna aina mbili za amri, amri ya jumla na amri bainishi. Amri ya jumla ni maelezo ya ujumla yanayoidhinisha utendaji wa jambo bila ya kubainisha jinsi linavyotakiwa lifanyike. Kwa upande mwingine, amri bainishi hubainisha sawasawa namna jambo linavyopaswa kutendeka. Tazama baadhi ya mifano ya kawaida. Mungu anatuamuru twende tukahubiri injili, ambayo ni amri ya ujumla kwa sababu haikubainishwa ni njia gani itumike katika kwenda kuhubiri iliyotajwa. Nuhu aliambiwa atengeneze Safina ya mti wa mvinje. Aina ya mti ilikuwa ni amri bainishi, hivyo alikatazwa kutumia aina nyingine ya mti. Muziki ni neno la ujumla ambalo hujumuisha aina zote za muziki. Kama Mungu angesema tu fanyeni muziki, Wakristo wangekuwa na uchaguzi wa kutumia aina yo yote ya muziki lakini Mungu amebainisha uimbaji ambao unaondoa aina nyingine zote za muziki. Hivyo, ala za muziki zimeondolewa, ingawa Mungu hakutuambia wazi kuwa tusitumie ala.

# Msaka Tonge

## Kupitia 1 Petro

**Rebecca Rushmore**

1. Matokeo ya mwisho ya imani yetu ni nini?
2. Neno la Bwana litavumilia mpaka lini?
3. Tunaitwa kutoka wapi?
4. Kusudi la serikali ni nini?
5. Wakristo wanajisikiaje wanapoteswa kwa ajili ya kutenda haki?
6. Ni roho ngapi ziliokolewa na maji siku za Nuhu?
7. Kitu gani kitafunika wingi wa dhambi?
8. Hukumu itaanzia wapi?
9. Wakristo wanatakiwa wafunikwe na nini?
10. Ibilisi anafananishwa na mnyama gani?

**(Tafadhali soma 1 Petro ili kujibu maswali haya)**

# Mariamu na Martha

Martha Lynn Rushmore

***"Ikawa katika kuenenda kwao aliingia katika kijiji kimoja; mwanamke mmoja jina lake Martha akamkaribisha nyumbani kwake. Naye alikuwa na umbu lake aitwaye Mariamu, aliyeketi miguuni pake Yesu, akasikiliza maneno yake, Lakini Martha alikuwa akihangaika kwa utumishi mwingi; akamwendea, akasema Bwana huoni vibaya hivyo ndugu yangu alivyoniacha nitumike peke yangu? Basi mwambie anisaidie, Bwana akajibu akamwambia Martha, Martha unasumbuka na kufadhaika kwa ajili ya vitu vingi; Lakini kinatakiwa kitu kimoja tu; na Mariamu amelichaguwa fungu lililo jema, ambalo hataondolewa"*** (Luka 10:38-42).

Mtazamo wa andiko hili si kwamba watu wasijishughulishe na mambo ya nyumbani, lakini hali halisi kuhusu Yesu ni kumsikiliza na kutii maneno yake. Tofauti kubwa ilionyeshwa kati ya dada hawa wawili. Mariamu aliketi na kumsikiliza Yesu, wakati Martha aliandaa chakula. Kirai [fungu la maneno lisilokamilisha sentensi ili ilete maana], ***"kinatakiwa kitu kimoja tu"*** (Luka 10:42) kinarejelea kusikiliza maneno ya Yesu, ambalo ndilo fungu alilolichagua Mariamu kulifanya. Maudhui hayohayo yanaonekana pia katika Luka 8:1-21.

Mariamu na Martha walikuwa ni dada zake Lazaro. Waliishi katika mji wa Bethania na Yesu alikwenda kuwatembelea. Martha alikuwa akiandaa chakula kwa ajili ya wageni wao. Martha alikuwa sawa na sisi tu. Marafiki wanapotutembelea tunataka kila kitu kiwe sawasawa. Lakini, Mariamu aliketi miguuni pa Yesu na kumsikiliza, na katika tukio lingine aliosha miguu ya Yesu kwa mafuta na kuikausha kwa nywele zake (Yohana 11:1-2). Katika maelezo ya Luka 10, Martha alilalamika kwa Bwana kwamba Mariamu alikuwa hamsaidii. Yesu akajibu kwamba, Martha alikuwa anashughulika na huduma nyingi. Mariamu alifanya uchaguzi bora, kumhudumia Bwana.

Yohana 11:1-12:12 inatupa habari za ziada kuhusu Mariamu, Martha na Lazaro. Lazaro, kaka yao Mariamu na Martha alikufa. Kama ilivyoelezwa, ndugu hawa waliishi katika mji wa Bethania. Mariamu na Martha walituma watu kwenda kumwita Yesu aje kwao kwa sababu Lazaro alikuwa mgonjwa. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba walihitajika kwenda Bethania. Wanafunzi hawakutaka Yesu aende kwa sababu Wayahudi walitaka kumwua. Hata hivyo, baada ya siku mbili, Yesu aliwaambia mitume wake kwamba kupitia kifo cha Lazaro wangeamini.

Martha alikwenda kumlaki Kristo na akamwambia kwamba kama angefika nyumbani kwao mapema, kaka yao Lazaro asingekufa. Akasema Lazaro amekufa siku nne zilizopita na sasa ***"ananuka"*** (Yohana 11:39). Ndipo Martha akaondoka kwenda kumtafuta Mariamu. Martha na Mariamu walikuwa katika majonzi makubwa, wakarudi kwa Yesu. Inaonekana kwamba Bwana wetu alilia kwa sababu ya huzuni ya rafiki zake na si kwa sababu ya kifo cha Lazaro.

Walipokuwa wanakwenda makaburini, Yesu alimwambia Martha kwamba kaka yake angefufuka tena. Yeye Martha alifikiri kwamba Yesu anazungumzia ufufuko wa siku ya mwisho. Lakini, Yesu alimfufua Lazaro kutoka kwa wafu saa ile ile.

Martha anaonekana kupata jina baya kwa sababu alikuwa anaandaa chakula cha kimwili kwa ajili ya Bwana badala ya kumruhusu Yesu amlishe chakula cha kiroho. Sisi pia tunafanya hivyo hivyo. Kama marafiki zetu watakuja, tunajitahidi kuhakikisha kwamba nyumba imefanyiwa usafi, vyombo vimeoshwa, tumepiga deki, na samani zetu zimesafishwa na chakula kimeandaliwa.

Sisi pia, tunapaswa kujifunza Neno la Mungu zaidi na kupata chakula chetu cha kiroho. Tunaonekana kama tunasahau ukweli kwamba Martha alikwenda kumlaki Yeau kwanza na ndipo akakimbia kwenda kumchukua Mariamu na kumpeleka kwa Bwana. Kwa upande wa wanawake kuna tabia za Martha na Mariamu, hebu tukumbuke kuweka vipaumbele vyetu sawa.

# Njia Sita Anazozitumia Shetani Kutushambulia

**(Imechukuliwa kutoka 2 Wafalme 18-19)**
**David Conley**

Shetani hafurahishwi na hali zetu nzuri. Kwa hakika anataka tushindwe katika kutembea kwetu na Mungu. Kuna njia nyingi ambazo Shetani anazitumia kutushambulia. Mfalme wa Yuda, Hezekia alishambuliwa na Shetani kwa kutumia majeshi ya mfalme wa Ashuru. Hizi ni njia sita kati ya nyingi ambazo Shetani alizitumia kumshambulia Hezekia na watu wa Yuda.

1. Alijaribu kuwashawishi kwamba wako peke yao.
2. Aligeuza ukweli.
3. Alidanganya kuhusu kile alichosema Mungu.
4. Alijaribu kuwafanya wagombane wao kwa wao kwa "kuzungumza lugha yao".
5. Alijaribu kuingia mapatano nao.
6. Alijaribu kuwashawishi kwamba hawawezi kumtegemea Mungu.

Shetani alimtumia Mfalme wa Ashuru dhidi ya Hezekia. Anaweza pia kuwatumia watu leo hii dhidi yetu. Yule mhubiri anapofundisha katika Televisheni, je, anafundisha Neno la Mungu? Hao wanafamilia wanapoweka shinikizo juu yetu, je, wanaongozwa na ukweli wa Neno la Mungu? Je, wale wenzetu pale kazini au shuleni wanapotualika tushiriki katika shughuli zao,ni shughuli zinazompendeza Mungu? Shetani anapotushambulia kwa kutumia njia hizi au nyingine tufanye kama alichofanya Hezekia. Alimgeukia Mungu ili kupata majibu.

## Wahusika katika Biblia

# Yosia, Alimtafuta Bwana katika Ujana Wake

John Stacy

Jina Yosia linamaanisha "Yehova anasaidia." Baba yake alikuwa ni Amoni, mfalme mwovu. Baba yake alitawala kwa miaka miwili katika mji wa Yerusalemu alifanya yaliyo maovu machoni pa Bwana. Alifuata njia ya baba yake na kuabudu sanamu. Amoni alimwacha Bwana, hakutembea katika njia ya Bwana. Watumishi wake walikula njama dhidi yake, wakamwua katika nyumba yake mwenyewe (2 Wafalme 21:19 -23). Babu yake Yosia alikuwa mwovu zaidi, aliitwa mfalme Manase.

Ina aminika kwamba wakati wa utawala wa Yosia manabii wafuatao walikuwa kazini kati ya watu wa Mungu. Manabii hao walikuwa Yeremia, Sefania, Nathani na Habakuki. Yosia alikuwa mfalme wa kumi na sita wa Yuda, na alitawala kwa miaka 31.

Kwanza kabisa, tunapoanza kujifunza maisha ya mfalme huyu, tunaona kuwa alipokuwa kijana alimtafuta Mungu. 2 Mambo ya Nyakati 34:1, inasema kwamba alikuwa na miaka 8 alipoanza kutawala. Mstari wa pili unasema, ***"Akafanya yaliyo mema machoni pa Bwana, akaziendea njia za Daudi babaye asigeuke kwa kuume wala kwa kushoto"*** Sulemani alisema mapema***, "Mkumbuke Muumba wako siku za ujana wako, kabla hazijaja siku zilizo mbaya, wala haijakaribia miaka utakaposema mimi sina furaha katika hiyo"*** (Mhubiri 12:1).

Angalia kwa makini 2 Nyakati 34:3. Kwa wakati huo Yosia alikuwa na umri wa takriban maika 16. ***"Kwa kuwa katika mwaka wa nane wa kutawala kwake, naye akali mchanga, alianza kumtafuta Mungu wa Daudi babaye; hata katika mwaka wa kumi na mbili akaanza kusafisha Yuda na Yerusalemu kwa kuondoa mahali pa juu, na kwa***

***kuondoa maashera na sanamu za kuchora nazo za kusubu"*** Tunaona bidii kubwa ya Yosia katika mistari miwili iliyofuata ***"Wakazibomoa madhabahu za mabaali machoni pake; na sanamu za juu, zilizoinuliwa juu yake, akazikata-kata; na maashera, na sanamu za kuchonga, nazo za kusubu, akazivunja-vunja, akaziponda kuwa mavumbi, akayamimina juu ya makaburi ya hao waliozichinjia dhabihu. Akaiteketeza mifupa ya makuhani madhabahuni mwao, akasafisha Yuda na Yerusalemu."***

Marejesho na uamsho wake ulifika mpaka Samaria, kama tunavyoona kwa kusoma 2 Nyakati 34:6-7. Kwa maoni yangu, tunaweza kumweka Yosia katika kundi la vijana wengine mashuhuri katika Biblia kama vile Danieli, Yusufu na vijana watatu wa Kiyahudi waliotupwa katika tanuru la moto.

**Pili,** tunapojifunza kuhusu Yosia tunaona kwamba katika umri wa miaka 26 alikarabati hekalu la Mungu. 2 Nyakati 34:8 inatuambia kwamba aliwatuma Shafani, Maasea na Yoa kukarabati nyumba ya Bwana Mungu wake. Inahuzunisha sana kufikiri kwamba nyumba ya Bwana ilikuwa imetelekezwa. Ilitelekezwa kwa muda mrefu kiasi kwamba kama isingekarabatiwa huenda ingebomoka kabisa. Vipi kuhusu nyumba ya Mungu leo hii? Nyumba ya Mungu ni kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na mwamba wa kweli (1 Timotheo 3:15).

Nabii Hagai aliizungumzia nyumba ya Bwana kwa watu wake, alisema, ***"Je, huu ndio wakati wa ninyi kukaa katika nyumba zenye mapambo ya mbao iwapo nyumba hii inakaa hali ya kuharibika?"*** (Hagai 1:4). Makanisa yetu mengi yamekufa au yanakufa kwa sababu tumeyatelekeza. Tunafikiri zaidi juu ya nyumba zetu? Gharama kubwa tunazozitumia kwenye nyumba zetu zinaonyesha ukweli huo. Labda tunahitaji kuuliza swali hili lililoulizwa na mwandishi wa Waebrania 2:3 **"*Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii*?"** Hakuna kupona ikiwa tunautelekeza. Tutazamie tu maangamizi.

Lilikuwa ni jambo la huzuni kuona nyumba ya Mungu katika hali ile mbaya, lakini kulikuwa na jambo baya zaidi ya hilo. Hilkia, kuhani alipata kitu kilichokuwa kimepotea. Alipata Kitabu cha Sheria ya Bwana

kilichotolewa na Musa. (2 Nyakati 34:14). Hebu fikiri juu ya jambo hilo. Biblia au sehemu yake imepotezwa katika nyumba ya Mungu wa kweli, aliye hai! Baadhi ya watu husema kuhani aliiona Torati (vile vitabu vitano vya kwanza vya Agano la Kale). Wengine wanasema kilikuwa kitabu cha Kumbukumbu la Torati pekee. Katika Matendo 17, tunasoma kuhusu Mungu asiyejulikana. Katika kizazi chetu tunazungumza juu ya kanisa lisilojulikana. Lakini hapa miongoni mwa watu wa Mungu wanazungumzia kitabu kisichojulikana, Biblia! Hii inaonyesha ni kiasi gani ukengeufu utamweka mtu mbali na Mungu.

Vipi kuhusu sisi? Je, Biblia ni kitabu kisichojulikana miongoni mwa watu wetu? Ni wangapi kati yetu tunasoma na kujifunza Biblia kila siku? Je, tunakijua kweli inachofundisha? Kuna mtu mmoja alisema, tunachokihitaji zaidi si mafundisho ya kibiblia. Tunahitaji kuitendea kazi Biblia kwa yale tunayoyajua. Amina katika hilo. Wengi miongoni mwetu hatuendi na Biblia kanisani. Hatujifunzi masomo ya vipindi vya Biblia kwa sababu shule ya Biblia ya Jumapili ni kitu kilichopitwa na wakati miongoni mwa watu wa leo. Wengi wa wahubiri wetu leo hii hawahubiri Biblia tena. Wanatoa Maandiko kidogo na hadithi nyingi. Au labda ni somo kuhusu matukio mapya katika ulimwengu huu au mchanganyiko wa masomo ya maadili na siasa. Kuwa na fikra chanya, afya na utajiri wa injili havina nafasi tena katika kuokoa roho za wanadamu. Ukweli ni kwamba hakuna kinachoweza kuchukua nafasi ya Injili (Warumi 1:16; 1 Wakorintho 1:18).

Katika 2 Nyakati 34:18, mwandishi alimsomea kitabu mfalme. Mfalme akararua mavazi yake akamwambia mwandishi pamoja na kuhani kwenda kwa Bwana kuuliza juu ya jambo hili. Mfalme alifadhaika sana na alionekana kuamini kuwa ghadhabu ya Mungu iko juu ya watu kwa kushindwa kwao kuishi sawasawa na jinsi alivyoagiza Mungu katika kitabu chake (1 Nyakati 43:20- 21).

Watu hawa hawakwenda kwa nabii Sefania. Baadhi ya watu wanafikiri kwamba kwa wakati huo nabii Sefania alikuwa ameshakufa. Pia hawakwenda kwa Yeremia kwa sababu inaaminika kwamba alikuwa katika mji wa Anathoth. Walienda kwa nabii mke Hulda

aliyekuwa anaishi Yerusalemu (2 Nyakati 34:22). Naye akasema Bwana angeleta uovu juu ya watu hawa kwa sababu ya kuabudu sanamu. Laana zilizopatikana katika kitabu zingemwagwa juu ya Yuda na zisingezimwa (2 Nyakati 34:24-25).

Moja ya sifa kuu alizopewa mfalme inapatikana katika 2 Nyakati 34:27. Nabii mke Hulda alizungumza kuhusu Yosia katika 2 Nyakati 34:27 ***"Kwa kuwa moyo wako ulikuwa mwororo nawe umejinyenyekeza mbele ya Mungu uliposikia maneno yake juu ya mahali hapa na juu ya wakaao, ukajinyenyekeza mbele zangu na kuyararua mavazi yako na kulia mbele zangu mimi nami nimekusikia asema Bwana."*** Mstari unaofuata unasema kwamba angekufa kwa amani na asingeishi hata kuona uovu ukija juu ya watu wake.

Katika hoja ya **Tatu**, tunaona Yosia anawasomea watu kitabu cha Bwana. Kama ingelikuwa Torati nzima ingemchukua saa kumi kuisoma. Wasomi wengi wa Biblia wanafikiri alisoma kitabu cha Kumbukumbu la Torati. Biblia inaeleza kwa kifupi tu ikisema*, **"…na akasoma katika masikio yao maneno yote ya kitabu cha agano kilichopatikana katika nyumba ya Bwana"*** 2 Nyakati 34:11, inasema alifanya agano na Bwana. Yeye na watu wake waliahidi kufuata mafundisho ya kitabu katika maisha yao. Kujitoa kwake kulifanywa kwa moyo wote na roho yote. Aliwaamuru watu wafanye mapenzi ya Mungu, nao walifanya. Siku zote za maisha yake hawakuacha kumtafuta Bwana, Mungu wa baba zao (2 Nyakati 34:29- 33).

Sura ya mwisho katika maisha ya Yosia iliishia na kifo chake (2 Nyakati 35:20-24). Andiko linatuambia kwamba mfalme wa Misri aliyeitwa Neko alikuja Kakameshi ili apigane na Wababeli. Kwa sababu fulani Yosia alifikiri kwamba alipaswa kupigana naye pia. Lakini, mfalme wa Misri alimwambia asingependa kupigana vita na Yuda. Pia alimwambia kwamba Mungu alimwambia akapigane na Wababeli. Yosia aliambiwa aachane na kazi ya Mungu. Hata hivyo, Yosisa alibadili mavazi yake na akaingia vitani. Alijeruhiwa vibaya na mpiga mishale katika bonde la Megido. Akarudishwa Yerusalemu na kuzikwa. Watu

wote wa Yuda walimwombolezea ikiwa ni pamoja na Yeremia (2 Nyakati 35:25).

Kutoka kwa Yosia tunajifunza kwamba mtu anaweza kuinuka zaidi kuliko watu wengine katika familia yake. Alimtumikia Bwana ukiachilia mbali umri wake kuwa mdogo. Akaharibu ibada za sanamu ambazo zilikuwa chukizo kubwa kwa Mungu. Akajenga nyumba ya Bwana na kuzingatia kitabu cha Mungu. Alikuwa mfalme wa marejesho na uamsho. Alimtumikia Mungu kwa moyo wake wote. Lakini, mwisho wa maisha yake alifanya kitu cha kijinga. Kwa kushindwa kufanya mapenzi ya Bwana, aliuawa.

# Rubi za Robison

Marko 6:34 ina tukio lisilotarajiwa. Inatuambia kwamba, "***Naye aliposhuka mashuani, akaona mkutano mkuu, akawahurumia; kwa sababu walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji***." Kwa hiyo, huruma yake ilimsukuma kuwafanyia nini makutano? Hapa ndipo jibu lisilotarajiwa linapokuja. Jibu ni hili ***"akaanza kuwafundisha mambo mengi".*** Hili si jambo la kushangaza? Huruma ilimsukuma Yesu kufundisha. Mara nyingi tunafikiri kwamba kuwa na huruma ni kushughulika na mahitaji ya kimwili ya watu, mfano kuwalisha wenye njaa, kuwahudumia wagonjwa n.k. Ni sawa, lakini Yesu anataka watu wafanye mambo hayo yote. Hata hivyo, hapa tunaona kwamba huruma ilimsukuma Yesu kufundisha. Mafundisho ya Kristo yanaambatana na huruma. Hivyo, watu wanapofundisha mafundisho ya Kristo wanapaswa kuwa na tabia ya Kristo, yaani huruma.

***Andy Robison***

# KWA NINI MAMBO MABAYA HUWAPATA WATU WEMA ?

Andy Robison

**Kwa nini mambo mabaya huwapata watu wema?** Hili ni swali la miaka na miaka. Ni moja ya hoja zinazochukua nafasi muhimu katika kujadili uwepo wa Mungu.

Wanaopinga uwepo wa Mungu wanabisha kwamba Mungu hana sifa zote tatu za desturi ambazo ni kwamba yeye: ni mwenye uwezo wote, anajua kila kitu na kwamba ana upendo wote (omnipotent, omniscient and omnibenevolent). Kwa kuwa kuna mateso, wanadai kwamba kuna sifa mojawapo kati ya hizo imepunguka kwa Mungu. "Kama ana uwezo kiasi cha kuyazuia mateso na anayajua, basi angeweza kuyazuia." Au kama ana upendo wa kutosha, basi atakuwa hayajui mateso. Pia wanadai, "Ikiwa anajua kuhusu mateso na anajali kiasi cha kuweza kuyazuia yasitokee, basi hana nguvu zote. Watu wamekuwa wakitumia hoja hizo potofu katika maeneo mbalimbali kama vile mitaani, vyuoni n.k, kushambulia uwepo wa Mungu. Hoja hizo zinaweza kujibiwaje? Tunawezaje kukabiliana nazo?

Kwanza, tutambue kwamba Mungu alipoumba kila kitu, kilikwa **"*chema sana*"** (Mwanzo 1:31). Mungu hakufanya kosa wala hakuleta maumivu. Mwanadamu alipewa utashi pale alipowekewa mti wa ujuzi wa mema na mabaya katika bustani, na mwanadamu alionywa [alipewa maelekezo juu ya anachotakiwa kukifanya na asichotakiwa kukifanya] (Mwanzo 2:16-17). Palipo na uchaguzi, lazima pawe na matokeo. Tunaona kwamba mwanadamu alichagua vibaya na matokeo yake kifo na mateso vikaingia katika maisha yake, (Warumi 5:12-14). Kuwepo kwa mateso katika dunia si kosa la Mungu, bali ni kosa la mwanadamu.

Kuna sababu mbalimbali zinazoweza kumfanya Mwanadamu ateseke, lakini zote chanzo chake ni dhambi. Kwanza, mtu anaweza kuteseka kwa sababu ya dhambi zake mwenyewe. Ijapokuwa si lazima iwe hivyo siku zote, lakini wakati mwingine inakuwa hivyo. Marafiki wa Ayubu walitaka kumfanya Ayubu kuwa mtenda dhambi mkubwa kwa sababu walikuwa wameshikilia nadharia inayosema kwamba yeyote yule anayeteseka ni lazima atakuwa amefanya dhambi. Mmoja wao alisema ***"Tena akaonyesha hizo siri za hekima, ya kuwa hufanikiwa katika kuyatimiza makusudi yake! Ujue basi ya kuwa Mungu akuachilia katika uovu wako"*** (Ayubu 11:6). Ni kweli tunajua kwamba mtu anaweza kujiletea mateso kutokana na dhambi zake mwenyewe. Kwa mfano, mlevi au mtumiaji wa madawa ya kulevya anajua maumivu aliyojiletea mwenyewe na magonjwa mbalimbali.

Pili, inawezekana kuteseka kwa sababu ya dhambi za mtu mwingine. Dereva aliyelewa anaweza kumwua mtu asiye na hatia. Familia iliyompoteza mpendwa wao itateseka kwa sababu ya dhambi ya mtu mwingine, yaani yule dereva aliyekuwa amelewa. Watu watalia wakisema hii "si haki" Ni kweli si haki, lakini mambo ndivyo yalivyo katika ulimwengu huu wenye uhuru wa kuchagua na utashi. Kama Mungu angeondoa matokeo (mateso na mambo mengine) maana yake ni kwamba angekuwa ameondoa uhuru wa kuchagua na utashi. Kama uchaguzi wangu usingekuwa na matokeo, je, huo ungekuwa uchaguzi? Je, mlevi angelewa kiasi cha kuua pasipo kukusudia?

Sheria za asili pia zinahusika hapo. Mungu ameweka sheria za asili katika maisha yetu. Katika historia, Mungu amewahi kuzisimamisha kwa muda tu sharia hizo za asili kwa ajili ya uthibitisho wa ujumbe wake kupitia miujiza (Kutoka 5-12; Marko 16:20; Waebrania 2:1-4). Matendo yote ya kimiujiza ya namna hiyo sasa yamefika mwisho (1 Wakorintho 13:8-13; Matendo 8:14-17). Kama wengine wanavyoonekana kutegemea, Mungu angesimamisha kisababishi cha sheria za asili pale ambapo kwa bahati mbaya (au kwa makusudi) kingemletea madhara mtu (kama vile matumizi mabaya ya moto au maji, tusingekuwa na ufahamu juu ya sheria za asili ambazo

tunapaswa kuzitegemea. Hata hivyo, tunazitegemea sharia nyingi za asili kwa ajili ya maisha yetu (matumizi ya moto, maji n.k).

Tatu, ***mtu anaweza kuteseka kwa sababu ya uwepo wa dhambi ulimwenguni***. Baada ya dhambi kuingia duniani mpangilio mpya kabisa wa mambo ulifuata. Kifo na magonjwa vikaingia. Wengine wanatoa ushahidi kwamba mabadiliko makubwa ya tabia ya nchi yamekuja baada ya gharika iliyotokea katika siku za Nuhu, ambayo ililetwa kwa sababu ya uovu wa mwanadamu (Mwanzo 6:5). ***"Ulimwengu uliokuwepo wakati ule ukaangamia"*** (2 Petro 3:16). Labda dunia iliyobadilika ndiyo chanzo cha hali mbaya ya hewa, vimbunga, elninyo n.k, ambavyo vinaathiri watu. Kwa maneno mengine, watu wasio na hatia wanaumizwa na majanga ya asili na magonjwa mbalimbali.

Hata hivyo, uwepo wa Mungu hauhitaji kuwa na maswali. Kuna ushahidi mwingi unaothibitisha (katika usanifu, sababu-na-matokeo) vinavyoelekeza uhalisia wa uwepo wa Mungu. Zaidi ya hayo, Mungu amefanya jambo kuhusu mateso. Hakuyaondoa mateso, kwa sababu kama angefanya hivyo, angetuondolea uhuru. Badala yake alikuja na akapata mateso pamoja nasi katika uwakilishi wa Mwanawe (1 Timotheo 3:16; Wafilipi 2:5-7). ***"Alijifunza utii kwa mateso yaliyompata"*** (Waebrania 5:8). Sasa, kwa kufufuliwa kwake katika wafu, amekaa mkono wa kuume wa Mungu kutupatanisha kwa niaba wale ambao bado wako duniani wanaoteswa (Waebrania 2:18; 7:25).

Mateso ni tatizo halisi. Na tuko sahihi kufanya yote tunayoweza ili kuyaepuka na kuyaondoa. Lakini, kumbuka, si kosa la Mungu. Iwe uwepo wake ama upendo wake haipaswi kutiliwa shaka kwa sababu ya mateso. Mungu anajidhihirisha kuwa, ***"ni Baba wa rehema, na Mungu wa faraja yote"*** (2 Wakorintho 1:3).

> ***"Mwanamke azaapo, yuna huzuni kwa kuwa saa yake imefika; lakini akiisha kuzaa mwana, haikumbuki tena ile dhiki, kwa sababu ya furaha ya kuzaliwa mtu ulimwenguni"*** (Yohana 16:21). Maneno hayo ya Yesu yanatufundisha kwamba ingawa masumbufu ya ulimwengu hayafurahishi lakini katika hayo masumbufu kuna matarajio ya jambo zuri zaidi. Furaha ishindayo maumivu. (Shadrack S. Msambaza)

## Maswali katika Biblia

# Je, Mvinyo Yenye Kileo Inapaswa Kutumika Katika Meza ya Bwana?

Kevin L. Moore

Tunasoma kwamba Yesu ndiye aliyeanzisha meza ya Bwana; Mathayo 26:26-30, Marko 14:22-26, Luka 22:14-20, 1 Wakorintho 11:23-26. Mkate usiotiwa chachu (Mathayo 26:17; Marko 14:12), unawakilisha mwili wa Kristo. Kikombe kilicho na ***"mzao wa mzabibu"*** (Mathayo 26:26; Marko 14:25; Luka 22:18 kinawakilisha damu ya Kristo iliyomwagika ***"kwa ajili ya ondoleo la dhambi"*** (Mathayo 26:28).

Chachu au hamira ilikatazwa katika dhabihu zote za nafaka kwa Mungu (Walawi 2:11; 6:14-17). Kwa sababu hamira au chachu inapenya na kuchachua, katika lugha ya picha inatumika katika kueneza (Mathayo 13:33; Luka 13:21) na kuharibu (Wagalatia 5:9). Yesu alionya kuhusu ***"chachu"*** au ushawishi mbaya wa Mafarisayo, Masadukayo na Herode [Antipas] (Mathayo 16:6,11,12; Luka 12:1, Marko 8:15; 3:6; 6:14-28; 12:13).

Neno la Kiyunani ambalo mara nyingi linatafsiriwa ***"mvinyo"*** katika Biblia zetu halitumiki kamwe linapohusu meza ya Bwana. Katika lugha ya Kiyunani tunapata maneno yafuatayo *'gennema tas ampelou'* ("*mzao wa mzabibu*"). Muktadha wake unamaanisha juisi au maji ya zabibu (Walawi 25:5; Ufunuo 14:18). Aina ileile ya chachu (*saccharomyces cerevisiae*) inabadili wanga kuwa hewa ya ukaa kwenye mkate (ikisababisha uumuke) na maji ya zabibu (kuyafanya kuwa kileo). Kwa kuona kuwa hamira (chachu) ilikatazwa katika mkate wa Pasaka (Kumbukumbu 16:3), hali kadhalika haikutakiwa kuwemo kwenye mzao wa mzabibu (maana yake haukutakiwa kuwa kileo).

## Maswali katika Biblia

# Je, Mafarisayo Walikuwa Viongozi Vipofu wa Vipofu wa Mwisho?

Ardron Hinton

Maelezo haya yalitolewa kuhusu Mafarisayo katika Mathayo 15:12-14. Hawakuwa wa kwanza wala wa mwisho kustahili kupewa jina hili. Ebu fikiria juu ya viongozi wetu wa kisiasa na kijamii katika nchi zetu. Pesa nyingi zinatumika katika kuboresha elimu lakini bado kuna matatizo katika mfumo wa elimu yetu. Pesa nyingi zimetumika na zinaendelea kutumika kupambana na umaskini lakini hali inazidi kuwa mbaya. Uhalifu umezidi katika nchi zetu katika maeneo mbalimbali. Je, hali hii haionyeshi kwamba wale wanaopaswa kutatua matatizo haya hawafanyi hivyo kwa kuwa ni viongozi vipofu?

Fedha haziwezi kutuletea usalama na maendeleo tunayoyataka. Kwa nini tudhanie kwamba kutumia fedha nyingi kutaleta mabadiliko ya kimaendeleo? Kwa urahisi tu huwa takwimu zinaonyesha wazi matatizo yaliyopo dhidi ya maendeleo yanayotakiwa katika jamii zetu wakati tatizo ni kuwa na viongozi vipofu? Upofu wao unasababisha madhara kama: (1) kuporomoka kwa maadili katika nyumba zetu, (2) kukubalika kwa maadili yasiyo ya kibiblia, (3) kuiondoa elimu kwenye mfumo wa kidini, (4) ongezeko la kujali mfumo wa dini zinazowafurahisha watu, (5) ongezeko la ukosefu wa akili ya uwajibikaji katika vyombo vya habari na (6) kukua kwa nguvu ya urasimu katika serikali. Hatuwezi kuwa na hali ya ukuaji bora wa mmea (jamii) bila kufanya marekebisho kwenye mizizi inayoupelekea chakula. Kama viongozi wetu ni vipofu kwenye matatizo halisi, sasa tutegemee nini?

# Imekwisha

**Jerry R. Kendall**

**Utangulizi**

1. Ilitamkwana mtu aliyedhihakiwa, aliyeachwa, aliyevikwa taji la miiba kichwani, aliyetokwa na damu, pia aliyekuwa anakata roho.
2. Kilio kutoka kwenye ukimya na giza; ni nini kilichokwisha (hapo ni kitu sio mtu).
3. Yesu Kristo alikuwa ameyafikisha mambo kwenye mwisho wao uliokusudiwa (Matendo 3:18).
4. Bwana alifanya tendo la mwisho katika utimilifu wa kusudi.

**Mjadala:**

I. **Mateso ya Kristo yalikwisha** (Luka 24:25-27).
   A. Mateso yake yanaonyesha ukuu wa mapenzi ya Mungu (Warumi 5:6-9)
   B. Unyonge wake uliisha; sasa ameinuliwa (Wafilipi 2:3-22).
   C. Utengano wake na Baba na Roho Mtakatifu ulikwisha (Yohana 7:9)
   D. Huduma yake kwa mapenzi ya Baba sasa yametimia (Luka 22:15, 44-44).

II. **Kazi ya Kristo ya upatanisho ilikwisha** (Waebrania 2:17).
   A. Dhabihu yake ilikamilika (Danieli 9:24; Waebrania 9:26;10:9-12).
   B. Gharama ililipwa kwa ajili ya ukombozi na msamaha (Waefeso 1:7; Wakolosai 1:14).

C. Mwana-kondoo wa Mungu alitoa (Yohana 1:29; 3:3-6; Yohana 6:6).
D. Hali yake ya kutokuwa na dhambi iliimaliza sheria (Wakolosai 1:20-23; Warumi 6:14, 8:3-4; 10:3-4; Wagalatia 3:13, 21-25, 4:4-5).
E. **Upatanisho** uliwezekana (2 Wakoritho 5:17-20; Wakolosai 1:20-23).
F. Nguvu kwa kila jaribu na ulinzi dhidi ya kila hatari (Wafilipi 4-13).

III. **Kristo alivunja ufalme wa Shetani** (Mathayo 12:29).

A. Vita dhidi ya Shetani na ufalme wake viliisha (Waefeso 6:10-17)
B. Uzao wa mwanamke uliponda kichwa cha nyoka (Mwanzo 3:15)
C. Tumaini letu lipo katika msingi wa mwisho wa kazi ya Kristo (Ufunuo 20:1, 17-18).

IV. **Kazi ya Kristo Iliyokamilika Imethibitika.**

A. Pazia la hekalu lilipasuka vipande viwili kutoka juu mpaka chini (Mathayo 27: 50-53).
B. Ufufuo wa Yesu-dhabihu yake ulikubalika.
C. Kristo ameinuliwa, amewekwa mkono wa kuume; thamani ya kazi ya Kristo.
D. Roho Mtakatifu alishuka katika siku ya Pentekoste (Yohana 14-16, Matendo 2).

V. **Kristo Alimaliza, Maana Yake Nini?**

A. Maelezo ya ahadi; deni lilipwa kikamilifu; malipo yalifanyika.
B. Kristo alisaini hati kwa damu yake.

C. Neno la kikuhani; Mwana-kondoo mkamilifu asiye na hila wala mawaa.
D. Kazi iliyo bora ilikamilika.
E. Aliyetumwa kazini, baada ya kumaliza alisema "TETELESTAI"- imekwisha.

**Hitimisho:**

1. Kazi ya Yesu imekwisha! Hakulia kama mwathirika, bali kama mshindi.
2. Wayunani waliamini kwamba hekima ya kweli ilikuwa inaweza kufafanua vizuri, walikuwa na shauku kwamba walimu watoe "bahari ya mambo kwenye tone la lugha". Yesu aliposema "imekwisha," alifanya hivyo tu. Hii haikuwa hali ya kukata tamaa. Hazikuwa kelele za kushindwa au kelele za bure tu. Zilikuwa ni kelele za ushindi! Haikuwa sauti ya maafa bali tangazo la ushindi. Alikuwa amemaliza kazi ya Baba yake, alikuwa Bwana Yesu akitangaza ukamilifu wa yote aliyokuja kuyafanya. Alikuwa amemfunua Mungu kwa wanadamu na alikuwa ametimiza sheria (torati). Sasa alikuwa analipa gharama ya wokovu. Hakuwa anazungumzia mwisho wa mateso peke yake, bali mwisho wa malengo yaliyokusudiwa, yaani ukombozi kwa wanadamu. Ilitokea kuwepo ushindi wa Shetani kwa muda, ambao ni tukio la kifo. Kristo alitandaza mkono wake mmoja kwenye nguzo ya dhambi na mwingine kwenye nguzo ya kifo, na ufalme wa shetani umekwisha! Alichokuwa anakielezea Bwana wetu kimejumuishwa katika "IMEKWISHA"! Kifo chake kikawa fidia kwa ajili ya dhambi, na kwa ujumla Baba aliridhishwa na kazi ya Kristo. Mungu atujalie sote kwa utiifu, tumkubali Kristo, kwa maana amemaliza huduma yake ya upatanisho.

# Mtazamo wa Huduma ya Gerezani ya Daryl Townsend

## *Kwa nini kuwe na huduma ya Magerezani?*



Agizo Kuu ndio msingi ambao katika huo jitihada za kiuinjilisti za kanisa zimewekwa. Agizo hili lililotolewa na Bwana wetu limewapeleka ndugu na fedha zao katika sehemu mbalimbali za ulimwengu kuwasaidia hao walio katika dhambi na wanaomhitaji Mwokozi. Jitihada zetu zimezaa matunda sana katika maeneo mengi, nyumbani na hata nje ya nchi. Hata hivyo naamini kwamba tumetelekeza moja ya maeneo muhimu sana ya kazi mahali popote ulimwenguni, magereza.

Yesu aliweka wazi katika Mathayo 25 kwamba namna tutakavyowatendea maskini, wagonjwa, wageni na wafungwa itakuwa

na mchango mkubwa sana katika Siku ya hukumu ya mwisho. Kwa kweli Yesu alitangaza, kuwasaidia watu kama hao ambao hawawezi kujisaidia wenyewe ni kumhudumia Bwana wetu na si hao tu walio katika hali ya uhitaji. Kuna hao walioko gerezani wanaomba mtu awapende vya kutosha kiasi cha kujifunza Injili pamoja nao. Tunawezaje kuendelea kuwatelekeleza watu hawa ambao wana hamu kubwa ya kusikia na kupokea Injili ili waweze kuwa huru mbali na dhambi zao? Je, si ukweli kwamba waliotenda uhalifu wametenda dhambi? Kwani ni nini maana ya Neno dhambi? Hivyo basi, suluhisho la kuzuia uhalifu unaosababisha watu waende gerezani ni kushughulika na dhambi zao katika maisha yao. Suluhisho pekee kwa ajili ya dhambi ni Injili.

## Hali ya Magereza

Kuna zaidi ya wanaume na wanawake 140,000 walio katika magereza sasa hivi katika jimbo la Florida. Ukweli ni kwamba idadi ya wafungwa katika magereza katika Jimbo la Florida imeongezeka maradufu kati ya mwaka 1995 na mwaka 2005 na idadi hiyo imeendelea kuongezeka ingawa kwa kasi ndogo. Kuna sababu nyingi zinazosababisha tatizo hili. Kwanza, idadi ya watu inakua kwa kasi katika mji wa Florida, na idadi ya watu inapoongezeka uhalifu nao unaongezeka. Zaidi ya hapo, wafungwa katika magereza ya Jimbo la Florida wanalazimika kutumikia 85% ya muda wa vifungo vyao. Sababu hizi na nyingine zimesababisha ongezeko kubwa la idadi ya wafungwa katika magereza ya jimbo la Florida. Sababu nyingine ni kwamba wafungwa wengi waliomaliza kutumikia vifungo vyao wanarudi tena gerezani baada ya miaka 5. Ni wazi kabisa kwamba adhabu pekee haitoshi kuwazuia wahalifu kurudia kufanya uhalifu. Tunajua kwamba ni Injili pekee ndiyo inayoweza kubadilisha tabia za wanadamu.

## Historia Yangu

Nililelewa katika kanisa la Bwana, na nimekuwa Mkristo kwa miaka 40 sasa. Inchini Marehemu baba yangu alihudumu kama mzee wa kanisa katika kanisa la Kristo Lakeshoe katika Mji wa Jacksonville,

Florida kwa muda wa miaka 22. Nilihitimu katika Chuo Kikuu cha Florida mwaka wa 1993 na nikapata Shahadi ya B.S katika kilimo na somo langu kuu lilikuwa ni Utunzaji wa Wanyama wa Maziwa (Dairy Management). Nilifanya kazi kwa miaka 20 ili kunoa ujuzi wangu kama meneja wa shamba la mifugo lililokuwa na ngo’mbe wapatao 1,500. Pia, nilifanya kazi kama mshauri wa nyumbani na wa kimataifa katika kiwanda cha maziwa. Katika mwaka 2004, niliwaacha ng’ombe nikaanza kumtumikia Mungu nikitumika kama Mwinjilisti katika Kanisa la Kristo Middleburg.

Ilikuwa ni katika mwaka ule wa kwanza nilipoanza huduma ya magerezani. Kazi yangu katika magereza ilianza kwa kumtembelea kijana wa mshirika wa zamani ambaye alifungwa katika gereza la kijijini. Miezi michache baadaye, nikawa nafundisha somo la Biblia katika gereza la watoto. Baada ya miezi michache, mmoja wa wanafunzi wangu alitaka kutii Injili. Hata hivyo, hapakuwa na miundo mbinu ya kubatizia katika gereza lile. Lakini baada ya muda mfupi, niliweza kumbatiza kijana yule katika sehemu ya mapokezi katika kituo cha afya kule Lake Butler, Florida. Hiyo ilikuwa safari yangu ya kwanza kuhudumu gerezani. Wakati nayafanya hayo, Gary Wyder ambaye tayari alikuwa akitoa huduma hapo. Ndugu Gary alikuwa akifanya kazi katika huduma ya gerezani kwa zaidi ya miaka 20. Shauku ya kuhusika kwangu kufanya huduma ya gerezani ikaongezeka kuanzia wakati ule.

Ndani ya miaka 2 niliacha kazi ya uinjilisti katika kusanyiko, nikaanza kufanya huduma ya gerezani muda wangu wote. Nikaanzisha mradi ulioitwa Off the Chain Ministries (huduma ya kufungua mnyororo). Huduma hii ni huduma ya bure si ya kutaka faida. Nikaomba misaada kutoka kwa watu binafsi na wafanya biashara ili kupata huduma za msingi pasipo kuhusisha kusanyiko. Nilifanya hivyo baada ya kuruhusiwa kutafuta misaada na wale wanaosimamia huduma zisizokuwa na faida. Nimejihusisha katika huduma hii kwa takribani miaka 13.

# *Malengo ya Huduma Ya Gerezani*

Malengo yangu katika huduma hii ya magerezani ni haya:

- **Kuwatia moyo washirika/Kuwarejesha washirika**: Bado sijapata gereza ambalo halinawashirika wa mwili wa Kristo. Wengi wameanguka katika imani na wametengwa na familia zao pamoja na makusanyiko yao. Watu hawa wanahitaji kurejeshwa kwa Mungu ndipo warejeshwe kwenye familia zao za kimwili na za kiroho.

- **Kuwafikia waliopotea gerezani:** Kama nilivyoeleza hapo juu, magereza ni eneo lenye rutuba la kufanyia kazi ya Bwana. Kwa kawaida tunabatiza watu 20 hadi 60 kwa kila mwaka. Hawa ni watu walioona udanganyifu wa shetani na injili za uongo katika maisha yao na hata wakiwa gerezani. Wanahitaji tumaini ambalo linawezekana kwa njia ya Yesu tu. Kila siku watu wa kujifunza nao madarasa ya Biblia wanaongezeka kuliko muda unavyoruhusu. Hakika mavuno yameiva, yako tayari kwa kuvunwa!

- **Kuujenga Mwili wa Kristo/Kuanzisha makusanyiko ya Bwana magerezani:** Wakristo wanahitaji Wakristo wenzao. Huu ndio utaratibu wa kibiblia. Wakristo wanahitaji kuabudu pamoja katika roho na kweli bila kujali wako gerezani au wako huru. Huduma ya siku ya kuabudu inahitajika ili wafungwa wapate kufanya ushirika katika chakula chake kila juma na kumwimbia Mungu kwa kutumia **"*tunda la midomo*"** tu (Waebrania 13:15). Na kusemezana wao kwa wao, pamoja na kusikia injili ya kweli ikihubiriwa katika kila gereza.

- **Mazingira Baada ya Magereza/Programu ya mpito kati ya wafungwa na kanisa:** Ili huduma katika magereza au kazi yoyote ya uinjilisti ifanikiwe ni lazima kuwe na ufuatiliaji na kujitoa [kama wafuasi]. Watu wanapotoka gerezani, ni lazima waunganishwe na makusanyiko yao ili wabaki kuwa waaminifu. Ni lazima wagundue familia mpya ambayo itachukua nafasi ya ushawishi hasi ambao

wameujua katika maisha yao ya miaka iliyopita. Makusanyiko ni lazima yafanye sehemu yao ili huduma ya gerezani iweze kuwa na ufanisi. Hivyo, ni lazima tuwe na makusanyiko ambayo yako tayari kuwafungulia milango yao watu hawa na kuwatia moyo waweze kusahau maisha yao yaliyopita. Watu hawa wanahitaji msamaha, rehema, uwajibikaji na uwanafunzi sawasawa na sisi sote tulio wakosefu. Mpaka hapo, tonaendesha nyumba mbili za mpito ambazo katika hizo tunawakaribisha watu walioongolewa wakiwa gerezani ili wakae humo kwa kipindi cha angalau miezi sita baada ya kufunguliwa kwao. Tunaweza kuwatunza hadi watu tisa. Watu hawa wanakubali kuwajibika kwa maisha yao pamoja na fedha zao, madarasa yanayotakiwa kama shughuli za ziada katika kusanyiko letu n.k. Tutawapatia msaada wa mahitaji ya msingi kama vile nguo, chakula, usafiri na gharama nyingine zinazohitajika katika jamii huru. Tutawasaidia kupata ajira na kuwapatia sehemu salama za kuishi. Hao ndugu walio katika programu hii, ambao wamepata ajira, watalipa kodi na gharama nyingine za maisha. Watu hawa wataruhusiwa kuishi katika nyumba hizi mpaka watakapokuwa tayari kuishi kwenye nyumba zao wenyewe. Watu wengine wanakaa kwenye nyumba zetu hata zaidi ya mwaka.

- **Kuzifikia familia za hao walioko gerezani**: Familia za wafungwa zinajua vizuri zaidi kuliko mtu mwingine yeyote gharama ya dhambi katika maisha ya wapendwa wao. Inanishangaza kuona ni ndoa ngapi ambazo bado zipo hai wakati wote huu. Kuna ripoti kwamba kuna baadhi ya wafungwa wanaume ambao wameoa baada ya kuwa mbali na wake zao. Kwa kawaida, familia hizi huwa zinakwepwa na marafiki, ndugu zao, kanisa, na jamii hivyo wanakuwa pekee yao. Aibu ya uhalifu uliotendwa na wapendwa wao inakuwa juu yao daima. Tumekuwa tukishiriki katika madarasa ya Biblia na wake, watoto na wazazi wa wafugwa. Familia hizi zinaweza kuwa ni eneo zuri sana la kufanyia kazi ya Bwana kuliko hata wafungwa wenyewe. Hivyo, ufuatiliaji wa kusanyiko kwa familia hizi ni muhimu sana.

## Umaalum wa Kazi Yangu

Kuna magereza 15 yenye zaidi ya wafungwa 12,000 yaliyo umbali wa mwendo wa saa moja kwa gari kutoka sehemu ninayoishi. Taasisi pekee ya "*marekebisho ya imani*" ulimwenguni iko ndani ya mile 20 kutoka nyumbani kwangu. Eneo hili limeiva kwa uinjilisti wa gerezani. Kimsingi nimekuwa nikifanya kazi na magereza mawili tu katika kipindi cha miaka 13.

Kazi ninazofanya katika siku ninayopewa katika gereza zinatofautiana, lakini mara nyingi nakuwa nikifundisha Injili ya Bwana wetu. Nina makundi kadhaa ya madarasa ya Biblia ambayo yanafanana na kile tunachokifanya katika kusanyiko. Ninaweza kujifunza na watu kati ya 3 au 4 au hata kundi la watu 25. Tunajifunza vitabu mahususi vya Biblia, mada mbalimbali tunazopenda wakati mwingine huwa tunashughulikia jambo maalum ambalo wanayoweza kuwa nalo. Pia, nafundisha kwa upana programu zinazohusu utumiaji wa dawa za kulevya, namna utu wa kibiblia ulivyo na namna ya kutumia pesa na mambo yahusuyo uzinzi.

Zaidi ya hapo najihusisha na vipindi vya kurekebisha tabia vijulikanavyo kama "*Vipindi vya Ushauri wa Kiroho.*" Katika vipindi hivi nakutana na mtu mmoja mmoja nikiwafundisha pamoja na kutoa ushauri. Kila mfungwa anapewa nafasi ya kujifunza na kupata ushauri kwa takribani saa mbili kwa kila wiki. Vipindi hivi ni muhimu kwa ajili ya watu kujadili mambo yao binafsi ambayo wanaweza kuwa nayo au kujibu maswali muhimu ya kimafundisho ambayo mtu anaweza kuwa nayo. Kuna watu wengi wanaopenda vipindi hivi zaidi ya ninaowaona. Mara nyingi naendesha vipindi hivi katika maeneo mbalimbali mengine licha ya magerezani pekee.

Mwisho kabisa huwa nahubiri na kuendesha ibada katika taasisi hizo. Ibada hizi, ni sawa kabisa na zile zinazofanyika katika makusanyiko yetu. Tunaruhusiwa kuja na vitu vyote vinavyohitajika katika ibada ili watu hawa waweze kushiriki meza ya Bwana. Tunaimba na kusali pamoja. Wafungwa waliobatizwa pia wanaweza kushiriki katika ibada hizo.

Nashirikiana na ndugu wengine katika Kristo kufanya huduma hii ambao wametoa muda wao na nguvu zao. Baadhi ya ndugu kwenye makusanyiko ya karibu pia huendesha huduma hii kwa namna mbalimbali. Pia kuna ndugu wengine ninaoshirikiana nao katika kazi hii ambao wametoa muda wao wote. Kama vile ilivyo kazi nyingine ya Mungu. Watu wanapaswa kushirikiana pamoja ili kukamilisha kazi yake Bwana.

## *Unaweza Kufanya Nini ili Kusaidia Huduma Hii*

Kwanza kabisa, naomba sala zako kwa ajili ya kazi hii. Naelewa wazi uongozi na majaliwa ya Mungu yalivyo kila siku katika huduma hii. Tuombeeni, mimi pamoja na wale wote ambao tayari wamefikiwa na injili na hao wanaojitahidi kutafuta njia bora ya maisha baada ya kutoka kwenye maisha yao mabaya. Pia, waombeeni wale waliomaliza vifungo vyao na kuachwa huru. Majaribu ya ulimwengu ulio huru yana nguvu sana juu ya watu hao.

Pia unaweza kusaidia huduma hii ya magerezani kwa kuhusika moja kwa moja na wanaume na wanawake walioko gerezani. Jambo hili linaweza kufanyika kwa njia mbalimbali zikiwemo:

Kuwaandikia barua. Gereza ni sehemu ya upweke sana kwa watu wengi. Baadhi ya wafungwa hawapati barua kabisa au vipeperushi kama wanavyopata watu wengine walio huru. Tumia muda wako na uwaandikie barua watu hao walioongezwa katika mwili wa Kristo au wale tunaojaribu kuwafikia kwa Injili. Labda huwezi kwenda gerezani, lakini unaweza kuandika barua za kuwatia moyo watu hawa na kujenga mahusiano nao. Fursa hii inaweza kuwa kwa wanaume au wanandoa kwa pamoja.

Tuma na tengeneza masomo ya Biblia kwa njia ya vipeperushi. Kwa hakika huwa siwaombi watu hawa wajiandikishe kuchukua vipeperushi vya kozi za Biblia kwa sababu wengi wao watajiandikisha, jambo ambalo ni jema, lakini sina watu wa kutosha wanaojitolea kusahihisha na kuendelea nao katika kozi hizo. Baadhi ya watu wanaochukua kozi hizo wanauliza maswali na wanataka majibu kutoka

kwa wale waliowapa. Kwa kweli jambo hili linachukua muda na jitihada kubwa.

Kuwa na madarasa ya Biblia gerezani. Labda kuna gereza karibu na wewe ambapo hakuna kanisa la Bwana linalotoa huduma hiyo. Angalia kama unaweza na uko tayari, jaribu kuomba kibali cha kufundisha watu katika gereza hilo. Kumbuka kwamba lengo letu ni kujaribu kuanzisha makusanyiko ya Bwana katika magereza.

Fanya kazi na familia za wafungwa. Kwa kweli, mtu anahitajika kuwasiliana na familia za wafungwa. Hii itakuwa ni rahisi kama vile tunavyowapigia watu wengine simu, kuwatembelea na kujifunza nao Neno la Mungu. Pia unaweza kuwaalika kuhudhuria ibada na vipindi vingine vya kanisa.

Fanya kazi na wafungwa waliotoka gerezani. Nimeeleza hapo juu jinsi ilivyo muhimu kuwafuatilia watu hawa baada ya kutoka gerezani na kuwa huru. Watahitaji kuunganishwa na kusanyiko, ambalo ni familia yao mpya. Wanahitaji ushauri, kujua wajibu wao, kupata kazi, kupata huduma za usafiri n.k. Ni watu wa Mungu watakaoweza kufanya kazi hii na kuwawezesha watu hawa katika maisha yao mapya.

Tafadhali saidia kazi hii. Toa msaada wa hali na fedha ili kuwezesha huduma ya kuwafikia wafungwa magerezani ifanyike.

Mwisho, kumbuka kuna watu katika magereza sasa hivi wanaoomba mtu awafikie na kuwapa tumaini la maisha bora. Je, ungependa kusaidia ili watu hawa waweze kupata Injili? Hili ni tumaini letu la kweli pekee!

